**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA SABA**

**Kikao cha Nane - Tarehe 14 Novemba, 2019**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Job Ndugai) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mkutano wetu wa Kumi na Saba, leo ni Kikao cha Nane. Katibu.

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:**

Maelezo ya Waziri wa Mifugo na Uvuvikuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa *FAO* wa Kuzuia Uvuvi Haramu kupitia Bandari za Nchi Wanachama.

**MHE. RITTA E. KABATI (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI):**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa *FAO* wa Kuzuia Uvuvi Haramu kupitia Bandari za Nchi Wanachama.

**MHE. TUNZA I. MALAPO (K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI):**

Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa *FAO* wa Kuzuia Uvuvi Haramu kupitia Bandari za Nchi Wanachama.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:**
Maelezo ya Waziri wa Nishati kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia kuanzishwa kwa Ushirikiano wa Kimataifa wa Nishati ya Jua.

**MHE. HAMIDA M. ABDALLAH (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI):**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia kuanzishwa kwa Ushirikiano wa Kimataifa wa Nishati ya Jua.

**MHE. TUNZA I. MALAPO (K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA NISHATI:**

Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Kuanzishwa kwa Ushirikiano wa Kimataifa wa Nishati ya Jua.

**SPIKA:** Ahsante sana. Katibu.

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:**

## MASWALI KWA WAZIRI MKUU

**SPIKA:** Maswali kwa Waziri Mkuu, tunakuomba sasa Mheshimiwa Waziri Mkuu usogee. Ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nawakumbusha kuhusu ufupi wa swali lako na kwamba lijielekeze kwenye sera na lisiwe linalohitaji takwimu za papo kwa papo, vinginevyo utakuwa umelifuta swali lako wewe mwenyewe.

Muuliza swali wetu wa kwanza kwa kifupi ni Mheshimiwa Allan Kiula. *(Makofi)*

**MHE. ALLAN J. KIULA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kumuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu swali la kwanza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kumekuwa na malalamiko katika maandalizi ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa ambao karibu unafanyika, wapo watu ambao wana hofu ya kukosa haki zao za msingi za kupiga kura au kupigiwa kupigiwa kura. Je, nini kauli ya Serikali?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu ya swali hilo, tafadhali.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kiula, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo tunafahamu kwamba tarehe 24 mwezi huu wa Novemba kutakuwa na uchaguzi kwenye ngazi ya Serikali za Mitaa. Uchaguzi huu ulisharatibiwa na uratibu wake ulianza kutoka kwenye kutengeneza kanuni za uchaguzi wenyewe lakini pia kulikuwa na maandalizi ya kujiandikisha, kuchukua fomu na kurudisha na muda umeshapita. Kinachofuata sasa ni tarehe 17 kuanza kampeni za wale wagombea ili kila mmoja akaeleze nia na namna akavyoweza kushirikiana na wananchi katika kuongoza kwenye nafasi aliyoiomba. Baada ya hapo sasa tarehe 24 Novemba Watanzania wote watatumia fursa na demokrasia yao kwenda kumchagua kiongozi wanayemtaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa utaratibu huu ambao pia unaongozwa na sheria, kanuni na taratibu, tunaamini kila mmoja atapata haki yake ya msingi, muhimu ni kuzingatia hizo kanuni, sheria na taratibu ili uweze kukamilisha azma yako ya kuchagua kiongozi ambaye unamtaka mahali ulipo kama ni kitongoji au kijiji. Nitoe wito kwa Watanzania kutumia fursa hii kwanza kipindi ambacho kinakuja watu waende kusikiliza

sera za wagombea hao na nia thabiti ya kuwaletea maendeleo kwenye maeneo yao na kila Mtanzania apate nafasi ya kumchagua kiongozi ambaye anamtaka.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa utaratibu huu na kwa namna ambavyo Mheshimiwa Mbunge amekuwa na hofu hiyo, kila mmoja atapata haki yake kwa sababu maelekezo yote yapo sahihi na kila mmoja sasa ni fursa yake yeye mwenyewe kwenda kufanya maamuzi ya kumchagua kiongozi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Juma Selemani Nkamia.

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kumuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu swali kwa mara ya kwanza katika historia ya maisha yangu hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, kiapo chetu kinatutaka tuwe wakweli na tutasema ukweli daima. Baadhi ya Mikoa hapa nchini ikiwemo ya Dodoma na Wilaya zake zote, Manyara, Singida inakabiliwa na tatizo kubwa la chakula. Baadhi ya Wenyeviti wa Kamati za Ulinzi na Usalama kwenye Wilaya na Mikoa inawezekana hawatoi taarifa sahihi kwa woga kutokana na pengine kutoelewa vizuri kauli ya Mheshimiwa Rais. Je, Serikali iko tayari sasa pengine kuunda Tume au Kamati Maalum ifanye utafiti ije na *data* zinazoonesha kuna upungufu gani wa chakula katika maeneo haya ili wananchi hawa wapelekewe chakula walau cha bei nafuu kwa sababu hali si shwari? *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimwia Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Juma Nkamia, Mbunge wa Chemba, kama ifuatavyo:-

Mheshmiwa Spika, jambo hili limekuwa likizungumzwa hapa mara kadhaa na Waheshimiwa Wabunge wakieleza

hali ya chakula kwenye maeneo yao. Upungufu wa chakula upo kwa baadhi ya Wilaya na maeneo kadhaa na hii ilitokana na tatizo la hali ya hewa kwamba yapo maeneo msimu uliopita hayakupata mvua za kutosha. Jambo hili linapotokea kule kwenye ngazi hiyo tunao viongozi na tumeweka utaratibu kama Serikali wa viongozi waliopo kwenye maeneo hayo kuratibu shughuli zote ikiwemo na hayo yanayotokea kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa na kusababisha kuwa na upungufu wa chakula.

Mheshimiwa Spika, Serikali tunacho chombo kinachonunua vyakula na vinahifadhiwa ambacho ni *NFRA. NFRA* inaponunua chakula ni kwa ajili ya maeneo ambayo hayana chakula na hukipeleka na kuwauzia na kurudisha zile fedha ili ziendelee kununua chakula kingine ili ile benki iendelee kuwepo. Kwa hiyo, tunachosubiri sasa ni viongozi wa maeneo hayo wakiwemo Wakuu wa Wilaya kuandika wao wenyewe kuonesha kwamba eneo lao lina upungufu wa chakula na mahitaji ni kiasi fulani ili sasa Wizara ya Kilimo inapoandikiwa taarifa hiyo itaratibu vizuri utaratibu wa namna ya kuwafikishia chakula lakini kwa kwenda kuwauzia ili tupate fedha za kununua chakula kingine ili benki yetu ya chakula iendelee kuwepo.

Mheshmiwa Spika, jambo hili limeshafafanuliwa sana na Waziri wa Kilimo. Hata hivyo, hofu ambayo Mheshimiwa Mbunge anayo kwamba labda Mheshimiwa Rais aliagiza ni pale ambapo hali ya hewa ni nzuri, kila mmoja ana nafasi ya kwenda kulima au kufanya kazi halafu kunakuwa hakuna chakula. Hapo sasa maelekezo yale ndiyo yanachukua nafasi yake kwamba viongozi waliopo kwenye maeneo hayo wanao wajibu wa kusimamia kuhakikisha kila mmoja anafanya kazi pamoja na kulima mazao ya chakula na biashara ili waweze kujipatia tija inapofikia kipindi kama hiki kila mmoja anakuwa na akiba yake. Sasa inapotokea hali ya hewa ni mbaya, Mkuu wa Wilaya akieleza atakuwa anaeleweka kwa sababu pia baada ya kutoa taarifa hiyo timu ya Wizara ya Kilimo itakwenda kuona hali halisi na kuweza kuzungumza na mamlaka ile ili iweze kupelekewa chakula cha bei nafuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia nitoe wito kwa wafanyabiashara wetu nchini, Tanzania maeneo yote haya yana hali ya hewa tofauti; yapo maeneo yamepata mvua nyingi na wamezalisha chakula cha kutosha na yapo maeneo hakuna mvua na hakuna chakula cha kutosha.

Kwa hiyo, ni jukumu la wafanyabiashara wetu kutumia fursa hiyo kufanya biashara; kuhamisha chakula kutoka eneo ambalo lina chakula cha kutosha na kupeleka mahali ambapo hakuna chakula ili waweze kujipatia pia uchumi. Kwa hiyo, ni muhimu hata pia Wakuu Wilaya, Wakuu wa Mikoa kwenye maeneo yao wanapoona jambo hili wakutane na wafanyabiashara wawashawishi kwenda kuchukua chakula eneo ambalo hakuna uhaba wa chakula walete hapo ili ku-*stabilize* soko na kuwa na chakula cha kutosha.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, bado ni muhimu kwa Mkuu wa Wilaya kwenye Wilaya ya Mheshimiwa Mbunge kuiandikia Wizara ya Kilimo kueleza mazingira hayo yaliyopo katika Wilaya yake. Kwa utaratibu wa Wizara Kilimo unaweza kwenda kwenye Wilaya hiyo kujionea na kujiridhisha hiyo takwimu iliyotolewa halafu waruhusu sasa chombo chetu kupeleka mahindi kwa kuuza ili wananchi waweze kununua. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea, niwakumbushe tu kwamba utaratibu wetu wa kipindi cha maswali kwa Waziri Mkuu, swali la kwanza kabisa huwa linakuwa *reserved* kwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni. Ndiyo utaratibu wetu kwenye *Commonwealth* huwa ni fursa pekee ambayo Upinzani wanapata nafasi ya kuuliza maswali. Kwa hiyo, Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni anaweza asiwepo Bungeni siku yoyote lakini siku ya Alhamisi ya Maswali kwa Waziri Mkuu anakuwepo.

Kwa hiyo, hatujapata swali lile kwa sababu Kiongozi wa Upinzani Bungeni hayupo, uwe wapi na wapi kama Spika

hana taarifa zako wewe ni mtoro tu. Kwa hiyo, ni mtoro na ndiyo maana leo mnaona kwamba hiyo fursa ambayo imewekwa kwenye Kanuni haijaweza kutumia. Ndiyo maana mnaona mara nyingi fursa hiyo inapotea kwa sababu ya utoro. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na maswali, Mheshimiwa Jasson Rweikiza. *(Makofi)*

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi kumuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu swali la papo kwa papo.

Mheshimiwa Spika, mpango wa Serikali yetu ni kwamba ifikapo mwaka 2021 vijiji vyote viwe na umeme Tanzania na ndivyo hata Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015 inavyosema lakini hadi leo 2019 inaisha vijiji vingi havijapata umeme na 2021 ni kesho kutwa tu bado mwaka mmoja tunafika 2021. Ni nini mpango wa Serikali kuhakikisha kwamba ifikapo mwaka 2021 vijiji vyote Tanzania vitakuwa na umeme? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu ya swali hilo, tafadhali.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rweikiza, Mbunge wa Bukoba Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imedhamiria kupeleka umeme kwa wananchi mpaka ngazi ya vijiji na Serikali kupitia Wizara ya Nishati kupitia Shirika letu la *TANESCO* na taasisi yetu ya *REA* kazi hiyo inaendelea kutekelezwa kwa awamu kama ambavyo wamejipangia. Mamlaka hii inayo taarifa na inayo maelekezo sahihi kutoka Serikalini kwamba tunataka kuona kila nyumba ya Mtanzania inawaka umeme. Hata Rais wetu wa nchi, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli wakati wote anapozungumza anaendelea kusisitiza kwamba anataka kuona kila nyumba ya Mtanzania inawaka umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kwamba kila nyumba ya Mtanzania inawaka umeme amepunguza na bei ili Watanzania wote mpaka wale wa vijijini wamudu kuvuta umeme kupeleka majumbani kwao kwa thamani ya shilingi 27,000 tu. Ameenda mbali zaidi kwamba Watanzania hawa ambao hawana uwezo wa kununua gharama za bidhaa nyingine za kupeleka umeme kwenye maeneo yao ikiwemo nguzo na nyaya bado Mtanzania akilipa shilingi 27,000 kule kijijini nguzo za kufika nyumbani kwake ni bure hakuna kulipa. Hata nyaya zenyewe ni bure mpaka nyumbani kwake. Kwa hiyo, Mtanzania anapaswa kulipa shilingi 27,000 tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, azma ya Serikali hii ambayo tumejipangia mpaka mwaka 2021 kwamba kila nyumba ya Mtanzania iweze kupata umeme tumejipanga vizuri na kazi hiyo inaendelea vizuri na taasisi yetu ya *REA.* Kila Wilaya tumepeleka wakandarasi na wanaendelea na kazi yao. Tulikuwa na tatizo la nguzo, tatizo hilo sasa limekwisha kwani tuna nguzo za kutosha kule Mufindi. Mimi mwenyewe nimeenda kushuhudia uwepo wa nguzo kwenye makampuni yanayozalisha nguzo.

Kwa hiyo, kazi zinaendelea vizuri na malengo yetu yatafikiwa. Kama itatokea kutakuwa na tatizo lolote hapa katikati tusiweze kumudu kufikia vijiji vyote ambavyo tumejipangia kufikia mwaka 2021, nataka niwahakikishie Watanzania kuwa zoezi la uwekaji umeme vijijini litaendelea kwa awamu nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka niwahakikishie Watanzania mpaka ngazi ya vijiji kwamba malengo ya Serikali ya kusambaza umeme mpaka kwenye nyumba zilizopo vijijini bado litafikiwa na kazi hiyo inaendelea. Kwa bahati nzuri kazi hiyo inasimamiwa vizuri sana na Wizara ya Nishati na ninyi wenyewe mnajua Waziri wa Nishati, Naibu Waziri wa Nishati wametoa maelezo hayo mara kadhaa kuwahakikishia Watanzania kwamba umeme utapatikana. Jambo la muhimu zaidi tupeane ushirikiano, tuwape fursa wakandarasi wafanye kazi yao vizuri, tuwape nafasi Watanzania washiriki kwenye ajira hizo ili wafanye kazi kwa bidii ili malengo haya

ya kufikisha umeme kwenye nyumba mpaka ngazi ya kijiji yaweze kufikiwa. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa tunahamia upande wa CHADEMA, Mheshimiwa Devotha Mathew Minja, uliza swali lako tafadhali.

**MHE. DEVOTHA M. MINJA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni kumekuwa na matamko mbalimbali kutoka kwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Naibu wake wakisisitiza kwamba Uchaguzi wa Serikali ya Mtaa upo pale pale tarehe 24 Novemba, 2019 licha ya Vyama vya Upinzani kujitoa. Aidha, Mawaziri hao wamekuwa wakisisitiza kwamba kujitoa...

**SPIKA:** Mheshimiwa Devotha, Kanuni zetu zinakataa Mbunge kuandikiwa swali huko, akaja hapa akaanza kutusomea. Kwa kuwa swali hilo linaonekana rasmi kwamba siyo la kwako. *(Makofi)*

**MHE. DEVOTHA M. MINJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapana

**SPIKA:** ...bali umeandikiwa na watu huko waliokutuma...

**MHE. DEVOTHA M. MINJA:** Mheshimiwa Spika, sijaandikiwa...

**SPIKA:** ...kwahiyo namuita Mheshimiwa Mussa Bakari Mbarouk...

**MHE. DEVOTHA M. MINJA:** Mheshimiwa Spika, aahh!!

**SPIKA:**...uliza swali lako.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Mimi kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu lakini

pia nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi. Swali langu Mheshimiwa Waziri Mkuu ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika tumekuwa na taratibu za kupewa bei za mafuta kila mwezi na hii Taasisi ya *EWURA,* lakini sasa kwa Mkoa wetu wa Tanga watu wamekuwa na malalamiko kidogo, kwamba mafuta ya *Petrol* na *Diesel* yamekuwa bei kubwa ilhali yanashushwa pale pale. kwa mfano, Tanga *Petrol* sasa hivi lita ni shilingi 2,300 na *Diesel* ni kama kwenye shilingi 2,200 ilhali hapa Dodoma, *Petrol* ilikuwa ni shilingi 2,153 na vilevile *Diesel* ikawa ni kama kwenye shilingi 2,100.

Mheshimiwa Spika, sasa nilikuwa nataka kujua, ni vigezo gani vinavyotumika kwa hii bei ya mafuta kwa baadhi ya Mikoa kama Tanga, ambako mafuta yanashushwa pale pale lakini bei iko kubwa kuliko Dodoma, kuliko Iringa, kuliko Singira na Mikoa mingine? Ahsante.

**SPIKA:** Najaribu kupima kama vigezo gani ni swali la Waziri Mkuu au ni swali linalotakiwa liende kwa Waziri wa sekta. Mheshimiwa Waziri Mkuu kama una jambo labda kidogo tu; limenipa tabu kidogo lakini karibu Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ahsante, ahsante.

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge wa Tanga Manispaa kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba swali hili linahusisha takwimu maana lazima nieleze kanuni iliyotumika kufanya *calculation* hiyo. Hata hivyo kimsingi mafuta haya yanaangizwa kutoka nje ya Tanzania na kufika nchini; na yanapofika nchini hawaangalii yametua kwenye bandari gani lakini gharama za kutoka huko yanakotoka mpaka Tanzania kuanzia hapo sasa kupitia kanuni hiyo ndiyo yanatoa mgao wa mikoa hii kupata hizo bei. Sina uhakika Tanga wananunua shilingi ngapi na huko Mwanza wananunua shilingi ngapi ili kukidhi matakwa yako; lakini muhimu zaidi Waziri wa Nishati yuko hapa, ameisikia na kama kweli Tanga wananunua gharama

hiyo, na kama mafuta yanafika Tanga bei ni hiyo atakuwa amesikia basi nimpe fursa Mheshimiwa Waziri baada ya kipindi hiki ukutane naye ili aweze kukuelewesha kwa manufaa ya wananchi wa Tanga ili tuweze kuondoa hilo jambo ambalo unaona kama vile haliwezekani na kwa maelezo utakayopata naamini pia utaridhika na wanunuzi pia nao wataridhika. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi uliza swali lako Mheshimiwa.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa nafasi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu sekta ya elimu na afya zina upungufu mkubwa sana wa watumishi; na hii imechangiwa hasa katika sekta ya afya kutokana na ujenzi wa hospitali za Wilaya 69 lakini pia ujenzi wa vituo vya afya 350 na zahanati karibia kila Kijiji Nchi nzima. Sasa ni upi mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba tunapata watumishi wa kutosha kwenda kuwahudumia Watanzania ili ile dhana nzima ya kupeleka huduma kwa Wananchi iweze kutimia? Ahsante.

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri Mkuu tafadhali.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Shangazi, Mbunge wa Mlalo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba sekta hizi mbili, ya elimu na afya zina mahitaji makubwa ya watumishi kwasababu pia tumepeleka maeneo ya utoaji huduma zake mpaka ngazi ya vitongoji. Vilevile ukweli mwingine ni kwamba wote ni mashahidi namna ambavyo tumefanya maboresho kama sera yetu inavyohitaji; kwamba kwenye sekta ya afya sera yetu inasema kila kijiji kiwe na zahanati na angalau kila kata kuwe na kituo cha afya na kila wilaya kuwe na hospitali ya wilaya. Kazi ambayo sasa inafanywa ni ya ujenzi wa zahanati kupitia wanakijiji wenyewe na halmashauri zao, vituo

vya afya kwa mpango wa Ofisi ya Rais, TAMISEMI wa ujenzi mzuri, mkubwa unaonedelea sasa wa vituo vya afya vyenye mahitaji makubwa ya madaktari; vivyo hivyo, kwenye sekta ya elimu.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa sera yetu kwenye sekta ya elimu tunapeleka huduma ya elimu mpaka kwenye vijiji kwa kujenga shule za msingi; na kwenye vitongoji vikubwa tuna zile shule zinazoitwa shule bebeshi *(satellite schools)* ambazo pia zinatakiwa zijengwe ili kuwarahisishia watoto kusafiri kwa umbali mfupi.

Mheshimiwa Spika, maeneo yote haya yanahitaji wataalam, walimu na waganga upanda wa afya. Nini Serikali inafanya; ni kuongeza watumishi kadri tunavyoongeza miundombinu; na watumishi hawa ni pamoja na vifaa vyake.

Mheshimiwa Spika, upande wa watumishi, Serikali imeanza kutoa vibali vya ajira kwa sekta hizi mbili za afya na elimu; na sasa tumeenda hata pia kwenye kilimo kwa kupata maafisa ugani kwenda vijijini kusaidia wakulima kulima vizuri kwa vigezo.

Mheshimiwa Spika, upande wa elimu tumeshaajiri kuanzia mwaka 2016, na mwaka jana tumeajiri kwa mara ya mwisho walimu 6,000 na sasa tuna kibali ambacho kitatoka hivi karibuni cha walimu 16,000 kwa upande wa sekondari na msingi. Kwahiyo, tunaamini kwenye sekta ya elimu baada ya ajira hii tutakuwa tumepunguza kwa kiasi kikubwa uhaba wa walimu kwenye shule za msingi.

Mheshimiwa Spika, hivyo hivyo kwenye sekta ya afya, huko ambako tunajenga vituo vya afya vingi, hospitali za wilaya lakini pia na hospitali za rufaa za mikoa na za kanda; kote huko lazima tuhakikishe tunapeleka watalam ili waweze kuhudumia Watanzania maeneo hayo. Kwahiyo mkakati wetu ni kutoa vibali kadri Wizara zinavyotoa taarifa na mahitaji yake na kadri ambavyo tuna uwezo wa kifedha tunatoa ajira hizo, na tunaendelea nazo. Kwahiyo nataka niwasihi Watanzania, mkakati wetu wa kujenga miundmbinu

hautaishia hapo, tutakwenda pia na kuleta wataalam kwa kuajiri. Kwahiyo wasomi wetu walioko vyuoni na wale ambao wako nje wanasubiri ajira tunayo matumaini tukitoa vibali watapata matangazo wajitokeze na kila mmoja akubali kupelekwa kwenye kituo anakopelekwa ili aweze kufanyakazi. Kwahiyo Mheshimiwa Mbunge utoaji wa vibali utaendelea, na tutapeleka watumishi wa afya mpaka Wilayani Lushoto na tutahakikisha tunapeleka mpka Mlalo kwenye vijiji vyako na kwenye kata zako ili kuwe na Watumishi watakaoweza kusaidiana na Wananchi katika kutoa huduma hii. Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Sikudhani Yassini Chikambo, uliza swali lako.

**MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO:** Mheshimiwa Spika, ahsante Mheshimiwa Waziri Mkuu miongoni mwa mazao ya biashara ambayo yamekuwa yakilipatia Pato Taifa letu ni pamoja na zao la korosho. Katika msimu wa mwaka 2018/ 2019 wakulima walitimiza wajibu wao, walilima korosho wakazipeleka ghalani lakini hawakupata pesa kwa wakati, na hii imepelekea kuwa na mashaka makubwa. Je, Serikali imejipangaje katika msimu huu ambao umeshaanza kuhakikisha wakulima wale wanapeleka korosho ghalani na wanapata pesa kwa wakati kulingana na Sheria ya minada inavyosema? Ahsante.

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri Mkuu tafadhali la wakulima wa korosho.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Chikambo, Mbunge wa Mkoa wa Ruvuma kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba msimu wa mwaka 2018/2019 mfumo uliotumika kununua zao la koroshgo haukuwa mfumo rasmi bali ilikuwa ni kuokoa mazingira yaliyojitokeza kutokana na tabia iliyoonyeshwa na baadhi ya wafanyabiashara ya kutaka kuhujumu zao hili na hasa kuwapunja wakulima. Kwahiyo Serikali kupitia Mheshimiwa

Rais alifanya maamuzi ya kununua kwa gharama ya shilingi 3,300 korosho zote; na msimu ule tulizalisha vizuri sana kwa tani zaidi ya 230,000, na koroshgo zote zimeendelea kulipiwa kwa wakulima.

Mheshimiwa Spika, kiwango cha mwiho kilichokuwa kimebaki ni bilioni 40 ambayo baada ya kukutana na Wakuu wa Mikoa wanaotoka kwneye Mikoa inayozalisha korosho walimpa taarifa Mheshimiwa Rais ya madai hayo ya wakulima kila mkoa. Yalipojumlishwa yalikuwa ni bilioni 40 na Mhehsimiwa Rais alitoa kibali kwa hazina kutoa bilioni 40 mara moja na bilioni 40 zote zimetoka na sasa kazi ya ulioaji inaendelea. Ninaamini mikoa mingine tilishamaliza kama ilikuwa na wakulima wachache ukiondoa Mkoa wa Mtwara ambao una wakulima wengi wa korosho kwahiyo tunaamini malipo haya yanaendelea.

Mheshimiwa Spika, sasa msimu wa mwaka huu 2019/ 2020 umeshaanza mwezi Oktoba na kazi ya manunu zi imeanza na tumeamua mfumo ule ule uliuokuwa unatumika kuuzia zao la korosho ambao ulikuwana tafrani hiyo unaendelea; na mfumo wetu ni wa Ushirika na ni kwa njia ya minada. Tangu tumeanza minada yetu mpaka leo hakuna tatizo lolote lile minada inaendelea. Naamini kuna idadi kubwaya minada imeshafanywa Mtwara, Mkoa wa Ruvuma na Mkoa wa Lindi ambako korosho zimeshaanza na hatujapata kelele.

Mheshimiwa Spika, kwahiyo, niseme tu kwamba seriakli imejipanga vizuri kusimamia minada hiyo kama ambavyo tumesimamia hii iliyoko tayari na wakulima watapata fedha zao. Tumeweka masharti, mnunuzi yoyote atakayepata *offer* ya ule mnada kwamba yeye ndiyo anapaswa kununua kama alivyoomba, tumempa siku nne tu za kisheria. Tumesimamia ndani ya siku nne awe ameshalipa fedha hiyo kwa chama kikuu cha ushirika; na chama kikuu cha ushirika kupeleka chama cha msingi cha ushirika na kumfikishia mkulima. Angalau tumetenga siku saba mpaka 10 mkulima awe ameshalipwa malipo yake yote.

Kwahiyo ni imani yangu hata minada iliyotangulia wakulima watakuwa wameshalipwa kutokana na usimamizi na Sheria hiiz ambazo tumejiwekea ambazo pia wanunuzi wenyewe walikubali walipokuwa wanasaini kukubali kununua mazao haya. Kwahiyo nataka niwaondolee mashaka Waheshimiwa Wabunge mnaotoka kwenye maeneo yanayolima korosho, niwaondolee mashaka pia wakulima ambao pia sasa korosho zenu mnapeleka kwenye masoko kwamba Serikali itasimamia kikamilifu kuhakikisha kwamba wakulima mnalipwa kwa wakati kama ambavyo tumekubaliana na wanunuzi na biashara itakwenda bila ya kuwa na mgogoro wowote ukiondoa ule utaratibu uliotumika mwaka jana ambao haukuwa wa kawaida. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Swali la mwisho kwa siku ya leo litaulizwa na Kamishina, Mary Pius Chatanda. Mheshimiwa Chatanda uliza swali lako tafadhali.

**MHE. MARY P. CHATANDA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, mvua ambazo zimeendelea kunyesha hapa nchini hususani Mikoa ya Pwani zimeathiri sana miundombinu ya barabara pamoja na vifo ambavyo vimetokea katika mikoa hiyo. Sasa basi, Serikali imejipangaje kuwasaidia *TARURA* na *TANROADS* kuwapa fedha za kutosha ili waweze kukamilisha barabara zile ambazo zimeharibiwa kabla ya mvua za masika?

Mheshimiwa Waziri Mkuu nashukuru sana.

**SPIKA:** Mvua zimekuwa kubwa sana Korogwe na Handeni mwaka huu. Mheshimiwa Waziri Mkuu majibu ya swali hilo tafadhali.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kamishina Chatanda, Mbunge wa Korogwe Mjini kama ifuatavyo:-

Kwanza nianze kwa kutoa pole nyingi sana kwa Waheshimiwa Wabunge na wakazi wa Mkoa wa Tanga ambao wamepata athari kubwa ya kuondokewa na wenzetu kufutia mvua kubwa zilizonyesha wiki moja, mbili zilizopita. Tuwaombee Mwenyezi Mungu azilaze roho zao mahali pema peponi, Amina.

Mheshimiwa Spika, kufuatia mvua hizi ambazo zinanyesha kwa wingi na kuharibu miundombinu yetu, Serikali tumejipanga; na mpango wetu kupitia *TARURA* na *TANROADS* kwenye maeneo yote nchini pamoja na kamati za maafa ambazo pia zinasimamiwa na Wakuu wa Wilaya, Wakuu wa Mikoa kwenye ngazi zao wanaendelea kufuatilia mwenendo wa mvua hizi na madhara yake. Pale ambapo kuna madhara hatua za haraka zitachukuliwa na Kamati zile za maafa na watashirikiana na taasisi zinazohusika na maafa hayo; ikiwemo na kuondolewa kwa miundombinu ya barabara kwa *TANROADS* na *TARURA*. Tayari maeneo ya Mkoa wa Tanga ambayo yamepata athari, *TARURA* na *TANROADS* wamefanyakazi yao.

Mheshimiwa Spika, utakumbuka lilipotokea suala la kuvunjika daraja linalounganisha kati ya Tanga na Pangani, Mheshimiwa Rais aliridhia Jeshi la Wananchi liende likafanyekazi hiyo kwa haraka sana ili kusaidia *TARURA* na *TANROADS* kurudisha miundombinu angalau kuwezesha wananchi kupita na kuendelea na huduma zao, huo ndiyo mkakati ambapo tunauweka.

Mheshimiwa Spika, pale ambapo inatokea tunapeleka huduma ya dharura halafu tunawaongezea bajeti watu wa *TARURA* na *TANROADS* kuendelea kuimarisha miundmbinu hiyo na kuirudisha katika hali yake ya kwaida. Kwahiyo Serikali imejipanga vizuri kwenye hili kwasababu inao utaratibu mzuri tu kuanzia huko mwanzo.

Mheshimiwa Spika, kufuatia bajeti inategemea mradi huo utagharimu kiasi gani, mwaka huu wa fedha walipanga kiasi gani, kama kuna mapungufu kwa umhimu huo tutawaongezea fedha ili waweze kukamilisha ujenzi wa

miundmbinu hiyo. Kwa hiyo, Serikali itaendelea kushirikiana na vyombo vyetu kwenye maeneo yote Nchini kusimamia utoaji huduma kwa Wananchi iwe ni kwa hali ya kwaida au panapotokea dharura na tutalichukua jambo hilo kwa dharura hiyo hiyo kuhakikisha kwamba tunaokoa miundombinu hiyo kwa haraka sana.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa maswali hayo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. Muda wa nusu saa wa maswali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu umekamilika. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa heshima uliyotupatia ya kuwepo na kuweza kujibu maswali ya Waheshimiwa Wabunge, naamini nchi nzima ilikuwa ikifuatilia na wananchi wamefaidika sana kwa maelezo yako ambayo pia ni maelezo ya Serikali.

Katibu!

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:**

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 100

**Mji wa Mombo Kuwa Halmashauri ya Mji**

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA** aliuliza:-

Mji wa Mombo umekidhi vigezo vyote vya kuwa Halmashauri ya Mji na maombi yalishawasilishwa Serikalini.

Je, ni lini Serikali itaipa Mji wa Mombo hadhi ya Halmashauri ya Mji?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MITAA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, TAMISEMI,naomba kujibu swali la Mheshimiwa Timetheo Paul Mnzava, Mbunge wa Korogwe Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwambamaombi ya kupandisha hadhi mamlaka ya Mji mdogo wa Mombo kuwa Halmashauri ya Mji yaliwasilishwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI Agosti, 2016. Timu ya kuhakiki kutoka Ofisi ya Rais, TAMISEMI ilifika Mombo kufanya uhakiki wa vigezo vinavyotakiwa ili kuupandisha mji huo hadhi.

Mheshimiwa Spika, taarifa ya uhakiki inaonesha kuwa kulingana na Mwongozo wa Kuanzisha Maeneo ya Utawala wa Mwaka 2014, Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mombo haukukidhi vigezo vya kupanda hadhi na kuwa Halmashauri ya Mji, na walijulishwa kwa barua yenye Kumb. Na. CCB.132/394/01/16. Baadhi ya vigezo ilivyoshindwa kukidhi ni pamoja na idadi ya watu wasiopungua 150,000, eneo lenye ukubwa usiopungua kilomita za mraba 300 na kata zisizopungua 12. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mnzava umesima, tafadhali.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, masharti ambayo tulipewa tukishayafanyiakazi na yalishakaa vizuri. Hata hivyo naomba niulize maswali madogo mawili ya nyongeza:-

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; kwa kuwa majibu haya hayaoneshi matumaini ya Mji Mdogo wa Mombo kuwa Halmashauri ya Mji. Mheshimiwa Waziri unajua kwamba eneo likishatangazwa kuwa mamlaka ya Mji Mdogo, vijiji vinafutwa; jambo linalosababisha kubadilika kwa taratibu za uendeshaji ikiwemo ukusanyaji wa mapato na utumiaji wake; na inasimamiwa moja kwa moja na Halmashauri ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, nataka kujua Serikali haioni kwamba iko haja sasa ya kupitia upya taratibu za uendeshaji

wa mamlaka za miji midogo ili kuweze kuboresha na kusaidia mamlaka ili ziweze kufanyakazi zake vizuri?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; Jiografia na ukubwa wa Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe imekuwa ni changamoto, jambo linalosababisha migogoro kwneye eneo la kujenga hospitali ya wilaya lakini pia hata sasa kwenye eneo la kujenga Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya. Pamoja na kwamba Baraza la Madiwani limeshafanya maamuzi, ni lini Serikali itakuwa tayari kupitia upya mipaka ya maeneo ya Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe na Halmashauri ya Mji wa Korogwe ili kuondoa changamoto hizi kwa wananchi wetu?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo tafadhali Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MITAA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Spika, ahsante.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Timetheo Mnzava, Mbunge wa Korogwe Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tumepokea hoja za Mheshimiwa Mbunge. Hata hivyo, kama nilivyosema kwenye jibu la msingi, ni kwamba tulipotuma timu kutoka TAMISEMI ikaenda kule Korogwe baadhi ya vigezo vilikuwa havijakamilika. Kwa maelezo yake ni kwamba vigezo vimekamilika na anazungumza habari ya ukubwa wa eneo na mipaka ya eneo hilo. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tutachukua mawazo yake, tutayafanyiakazi, tushirikiane pale itakapowezekana Serikali iweze kuchukua hatua. Lengo la Serikali ni kwamba maeneo haya yasimamiwe vizuri wananchi wetu waweze kupata huduma kirahisi na kupunguza migogoro katika maeneo yetu ya kiutawala. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Hasna Mwilima nimekuona, swali la nyongeza tafadhali.

**MHE. HASNA S. MWILIMA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa ruhusa yako, naomba kabla sijauliza swali la nyongeza, tarehe 7 Novemba, 2019 nikiwa hapa Bungeni wakati nachangia Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano nilichangia jambo ambalo kwa namna moja au nyingine inaweza ikawa limewagusa sana Watanzania lakini pia baadhi ya Waheshimiwa Wabunge humu ndani ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilifanya vile kwa kutaka kuboresha Shirika letu la *ATCL,* lakini kwa kuwa inawezekana kwa namna moja au nyingine nikawa nimewakwaza Watanzania hasa wanawake wenzangu, naomba nichukue nafasi hii kuomba radhi kwa kauli yangu ile ambayo niliitoa hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuwaomba radhi Watanzania hasa wanawake wenzangu, naomba sasa niulize…

**SPIKA:** Mheshimiwa Hasna kabla hujaendelea nataka kuwaambia Waheshimiwa Wabunge, huo ndiyo uungwana! *(Makofi)*

Tumeipokea radhi hiyo. Mheshimiwa, endelea kuuliza swali.

**MHE. HASNA S. MWILIMA:** Mheshimiwa Spika, naomba sasa niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Mji wangu wa Nguruka ambao una vijiji viwili tumeshaomba sana TAMISEMI Mji ule uweze kukuzwa na uwe Mamlaka ya Mji Mdogo, lakini kwa mujibu wa vigezo lazima Kata ya Nguruka, Kata ya Itebula zipewe mamlaka ya kuongeza vijiji na kuongeza vitongoji ili waweze kukidhi haja. Kwa kuwa Mji ule una watu zaidi ya 100,000 niombe sasa Serikali ya TAMISEMI.

Je, iko tayari kutupa ruhusa ya kufanya mchakato wa kuongeza vijiji na vitongoji ili tuweze kukidhi haja ya kuwa na Mji Mdogo wa Mamlaka ya Nguruka. Nakushukuru.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri TAMISEMI, Mheshimiwa Mwita Waitara, majibu kuhusu Mji wa Nguruka.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Spika, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Hasna Mwilima, Mbunge wa Uvinza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge mwenyewe kwamba tayari eneo lake halikidhi vigezo vya eneo hili kuwa mji mdogo kwa maana ya Mamlaka, lakini tunaomba tupokee maoni yake tutayafanyia kazi na pale ambapo itakuwa imekidhi vigezo, basi tutaona namna ya kuboresha eneo hili. Ni kweli kwamba Mji wa Nguruka ni Mji mkubwa, ukipata hadhi unaweza ukawa wa kwanza kiuchumi, lakini pia kupeleka karibu huduma za wananchi. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na swali 101 na Mheshimiwa Upendo Furaha Peneza, Mbunge wa Viti Maalum. Nimekuona Mheshimiwa Susan Lyimo.

Na. 101

**Kuwahamisha Wananchi Walio Karibu na Mgodi wa *GGM***

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO (K.n.y. MHE. UPENDO F. PENEZA)** aliuliza:-

Wananchi wa maeneo ya Katoma Kompaundi, Nyakabale wameathirika sana na shughuli za mgodi wa GGM na Serikali ilikwishatoa maelekezo kwamba wananchi wa maeneo hayo wahamishwe:-

Je, ni lini sasa wananchi hao watahamishwa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA)** alijibu:

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Upendo Furaha Peneza, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kifungu cha 95(b) cha Sheria ya Madini, mgodi unapaswa kulipa fidia kwa wananchi wanaomiliki maeneo yanayozunguka eneo la uchimbaji lenye umbali wa mita 200. Hata hivyo, mwaka 2013, Mgodi wa *GGM* ulilipa fidia kwa wananchi walioko katika eneo lenye kipenyo cha mita 500 katika Mitaa ya Katoma Kompaundi na Nyamalembo ambapo wananchi 155 walilipwa kiasi cha shilingi bilioni 6.83. Aidha, kwa upande wa Nyakabale, Mgodi haukuwalipa wananchi fidia kwa kuwa maeneo yao yapo zaidi ya umbali wa mita 200 kutoka eneo la mgodi.

Mheshimiwa Spika, wananchi wote 155 waliolipwa fidia mwaka 2013 wanapaswa kuachia maeneo hayo yaliyofidiwa ili kupisha shughuli za uchimbaji. Naielekeza Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Geita kusimamia zoezi la kuwahamisha wananchi hao. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante. Endelea Mheshimiwa Suzan Lyimo.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, katika viwango vya Kimataifa huwa wanapima maeneo ambayo hayatapata athari hizo. Swali la kwanza, je, Serikali iko tayari sasa kuunda Tume au Kamati yoyote kupima maeneo hayo ili wannachi wasije wakajenga nyumba karibu na maeneo hayo ambayo yanaweza kupata mitetemo pale ambapo migodi hiyo inapasua miamba?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa kauli mbiu ya Awamu ya Tano ni Hapa Kazi Tu na kwa kuwa wananchi

wengi katika maeneo haya wanapokuwa wanahamishwa maana yake wanapata madhara ya kisaikolojia na kwa maana hiyo wanashindwa hata kufanya kazi. Je, Serikali haioni kutokuwahamisha kwa wakati kutapoteza dhana hiyo ya Hapa Kazi Tu?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Mwita Waitara, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Spika, naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Susan Lyimo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza ametoa ushauri tunaomba tuupokee. Tutaangalia kiutaalam sheria zinasemaje kwa sababu tuna sheria za uchimbaji hapa nchini. Kama zitaonekana zinafaa basi zitafanyiwa kazi. Hilo la kupima maeneo ya mitetemo ili kutoathiri nyumba za watu.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili kama nilivyoelekeza kwenye jibu langu la msingi na kimsingi hii imekuwa ni maeneo mengi kwamba kunakuwa na fidia zinaandaliwa watu wanalipwa halafu wanahama au wakati mwingine wanachukua muda mwingi sana. Sasa hivi tumeshaelekeza kwamba Mkuu wa Mkoa wa eneo hili aweze kuchukua hatua kuwahamisha wananchi ambao kimsingi wameshalipwa fidia na hawadai ili wapishe eneo hilo wale wenye shughuli zao za uchimbaji waende kufanya kazi zao bila vikwazo na kuondoa migogoro.

Mheshimiwa Spika, pia nitoe wito kwa wananchi wetu wa Tanzania wenyewe kwamba kama kuna eneo linachukua shughuli ya kiuchumi kama ya machimbo na tayari mtu alishalipwa fidia ni muhimu ahame katika eneo hilo kwa sababu anaendelea kukaa pale kwa muda mrefu, halafu ukienda kuwaondoa wanaanza malalamiko na migogoro, utakuta gharama ya vitu inapanda bei. Kwa hiyo wenyewe wachukue hatua, tumeshakulipa fedha upishe eneo lile

ukaanzishe maisha mengine ili kuepuka migogoro mbalimbali katika maeneo haya. Ahsante.

**SPIKA:** Nimekuona Mheshimiwa Devotha Minja, uliza swali lako tafadhali.

**MHE. DEVOTHA M. MINJA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Mheshimiwa Naibu Waziri amesikika akisisitiza kwamba hata kama Vyama Vya Upinzani vimejitoa kwenye uchaguzi wa Serikali za Mitaa haviwezi kuzuia uchaguzi kwa kuwa Serikali ina-*deal* moja kwa moja na wagombea na sio Vyama vya Upinzani.

Mheshimiwa Spika, naomba kumuuliza Mheshimiwa Waziri, hivi…

**SPIKA:** Mheshimiwa Devotha, leo umeamka kushoto kabisa. *(Kicheko)*

Swali la nyongeza lazima liendane na swali la msingi. Swali la msingi linahusu wananchi wa Katoma, Nyakabale na wengine ambao wamethirika na shughuli za mgodi wa *GGM,* sasa swali lako la nyongeza liko nje kabisa. Ni bahati mbaya sana. Tunaendelea, Mheshimiwa Naibu Waziri…

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila kufuata utaratibu)*

**SPIKA:** Hapana, swali nimeli-*disqualify…*

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, nilikuwa nataka niboreshe katika lile swali la nyongeza alilouliza Mheshimiwa Lyimo.

**SPIKA:** Ok, haya hilo nakuruhusu.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Katika swali la kwanza la Mheshimiwa Lyimo ni kwamba kwa mujibu wa Sheria ya Uchimbaji sehemu yoyote ambayo ni *active mining area* yaani sehemu ambapo kuna

shughuli za uchimbaji zinafanyika, Mwekezaji anatakiwa a-*compensate* mita 200 zaidi ya lile eneo ambalo ni *active area* kwa maana ya *buffer area* ili kuwaondoa hawa watu wasiwe karibu na maeneo ambayo wanaweza wakapata mitetemo na nyumba zikapata nyufa.

Kwa hiyo wanatakiwa wakishalipwa *compensation* mita 200 watoke lile eneo kwa maana ya kuzuia hiyo mitetemo na hii imepimwa kitaalam na ni sheria na ndiyo utaratibu wa uchimbaji. Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Joram Ismail Hongoli, Mbunge wa Lupembe. Bado tupo TAMISEMI. Mheshimiwa Hongoli uliza swali lako

Na. 102

**Fedha kwa Ajili ya Ukarabati wa Vituo vya Afya**

**MHE. JORAM I. HONGOLI** aliuliza:-

Halmashauri ya Wilaya ya Njombe ndiyo Halmashauri pekee iliyokosa fedha kwa ajili ya ukarabati wa Vituo vya Afya:-

Je, ni lini Serikali itatoa fedha kwa ajili ya ukarabati wa Vituo vya Afya katika Jimbo la Lupembe ikiwemo Kichiwa, Lupembe, Sovi na Kituo cha Afya Ikina ambacho wananchi wamejenga *OPD* bado majengo mengine ili kukamilika?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE)** alijibu:

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joram Ismael Hongoli, Mbunge wa Lupembe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2019/2020, Serikali imeidhinisha kiasi cha shilingi milioni 200 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa Kituo cha Afya Kichiwa kilichopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Njombe. Aidha, Kituo cha Afya Lupembe kimeidhinishiwa shilingi milioni 25 kupitia Mfuko wa Pamoja wa Afya kwa ajili ya ukarabati ili kukiwezesha kutoa huduma za dharura na upasuaji.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hongoli, swali la nyongeza.

**MHE. JORAM I. HONGOLI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza nianze kuishukuru Serikali kwa kutenga hizi fedha milioni 200 na milioni 25, lakini pia nishukuru kwa kutupatia bilioni 1.5 kwa ajili ya ujenzi wa hospitali ya wilaya.

Mheshimiwa Spika, nina swali moja tu la nyongeza; kwa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe kupitia mapato yake ya ndani na nguvu za wananchi imeweza kujenga Kituo cha Afya cha Ikuna lakini hatujafanikiwa kujenga wodi kwa ajili ya wagonjwa. Pia halmashauri na kupitia nguvu za wananchi imeweza kujenga jengo la mama na mtoto pale Lupembe, imeweza pia kukarabati chumba kwa ajili ya upasuaji na upasuaji ulishaanza toka mwaka 2017. Tatizo tulilonalo pale hatuna mawodi ya kutosha, je, Serikali ipo tayari kusaidia kuhakikisha kwamba kunakuwa na wodi za kutosha ili wananchi wakipata *operation* waweze kupata huduma nzuri zaidi kwa ajili ya kupumzika na kupata huduma? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu kwa maswali hayo mawili, Mheshimiwa Naibu Waziri TAMISEMI, Mheshimiwa Kandege, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Spika, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Hongoli kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, niruhusu kipekee nimpongeze Mheshimiwa Hongoli na wananchi wake. Kama kuna maeneo ambayo wananchi wanajitolea kwa kufanya kazi

ni pamoja na jimbo lake, lakini pia yeye mwenyewe amekuwa mfuatiliaji mkubwa sana kuhakikisha kwamba wananchi wake wanapata zahanati, vituo vya afya pamoja na hospitali za halmashauri. Naomba nimhakikishie ni azma ya Serikali kuwaunga mkono wananchi popote pale ambapo wanaonesha nguvu yao na sisi kama TAMISEMI tutahakikisha kwamba tunaunga mkono ili wodi ziweze kujengwa wananchi waweze kupumzika baada ya kupata matibabu.

**SPIKA:** Ahsante sana. Nataka tu kusema kwamba Serikali inafanya kazi nzuri sana ya kujenga zahanati, vituo vya afya na kadhalika nzuri sana, lakini katika matumizi ya dawa kwenye zahanati na vituo vya afya, makusanyo yale kupitia *user fee* yamekuwa ni madogo sana ambayo yanakuwa *realized.* Makusanyo yale ni muhimu katika kuviboresha vituo vya afya kiuendeshaji. Yamekuwa ni madogo sana kwa sababu ya mfumo unaotumika, unaitwa sijui *GoT-HoMIS,* sijui unaitwaje, lakini huo mfumo kuununua kwa kituo cha afya ni milioni 14.

Sasa fikiria vituo vya afya Tanzania milioni 14, 14 zahanati milioni 14, 14 ni kwa nini vituo vya afya, huduma za afya zitumie mfumo huo ambao ni ghali sana badala ya kutumia mfumo mwingine wowote ambao ni rahisi tena mfumo wenyewe hauingiliani na mifumo ya halmashauri. Kwa hiyo vituo vingi viko havina mfumo wowote, wanajikusanyia hela wanajilia. Naomba Serikali ikaangalie habari ya huo mfumo unaotumika kwenye huduma za afya, huo unaoitwa *GoT-HoMIS* huo yaani mapato mengi mno yanapotea kupitia eneo hilo. *(Makofi)*

Tunaendelea na Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, swali la Amina Saleh Mollel, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 103

**Mipango ya Usafiri kwa Watumishi wa Umma Wenye Ulemavu**

**MHE. AMINA S. MOLLEL** aliuliza:-

Mwongozo wa huduma kwa Watumishi wa Umma Wenye Ulemavu unawaelekeza waajiri kuweka mipango ya usafiri wa kuwawezesha Watumishi Wenye Ulemavu kwenda na kurudi kazini:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia mafuta ya gari kwa Mtumishi ambaye ana chombo chake cha usafiri?

(b) Je, Serikali imeweka mkakati gani wa kuwakopesha vyombo vya usafiri?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo muhimu sana Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Amina Saleh Mollel, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua changamoto za usafiri wanazokumbana nazo watumishi wenye ulemavu wakati wa kwenda na kurudi kazini au wanapohitaji usafiri kwa shughuli nyingine za kikazi. Ili kuhakikisha kuwa watumishi hao wanatekeleza majukumu yao kwa ufanisi, Taasisi zote za Umma zimeelekezwa kupitia Mwongozo wa Huduma kwa Watumishi wa Umma Wenye Ulemavu (2008), Sura ya tatu kifungu 3.15(a) kuhakikisha pale hali inaporuhusu, wawapatie watumishi hao usafiri au walipie gharama za mafuta kwenda na kurudi kazini kwa watumishi ambao wana vyombo binafsi vya usafiri. Waajiri kupitia Mwongozo huo wamekuwa wakitoa huduma kulingana na mahitaji ya watumishi wa kundi hili.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Waraka wa Watumishi wa Serikali Na.3 Kumb.Na. C/AC.7/228/01/16 wa tarehe 30 Juni, 2011, kuhusu utaratibu wa kukopehsa fedha taslimu watumishi wa Serikali kwa ajili ya kununulia magari/

pikipiki, samani na matengenezo ya magari na pikipiki iliweka mkakati wa kuwapatia watumishi wake wote wakiwemo watumishi wenye ulemavu mikopo kwa ajili ya kujinunulia vyombo vya usafiri yakiwemo magari na pikipiki. Utekelezaji wa waraka huo umekuwa ukifanyika kwa usawa kwa watumishi wote bila kujali jinsi, hali ya kimaumbile kwa watumishi wanaokidhi vigezo vya ukopaji. Waajiri wote wanakumbushwa kutoa kipaumbele kwa Watumishi wenye ulemavu ambao wanakidhi vigezo vya kukopa wakati wa utekelezaji wa waraka huu. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Amina Mollel, swali la nyongeza tafadhali.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Awali ya yote kwanza niruhusu nikupongeze wewe mwenyewe kwa kuwa Taasisi yako unayoiongoza imekuwa mstari wa mbele kujali haki za watu wenye ulemavu tukiwemo sisi Wabunge wenye ulemavu. Naomba ifahamike kwamba sisi wote ni walemavu watarajiwa. Pia nimpongeze *Iron Lady* Dkt. Mwanjelwa kwa kuwa nimekuwa msumbufu mkubwa kwake kufuatilia haki za watu wenye ulemavu hasa watumishi kutokana na changamoto wanazokutana nazo.

Mheshimiwa Spika, sasa nina maswali mawili ya nyongeza. La kwanza, ni kweli kuwa taasisi nyingi hazitumii mwongozo huu na miongozo hii inatokana na haki za watu wenye ulemavu ambazo nchi imeridhia mikataba mbalimbali ya Kimataifa. Mimi nilikuwa muajiriwa na sikuwahi kuona hili likifanyika na maeneo mengi nimepata malalamiko haya ya watumishi. Sasa naomba kufahamu kutoka kwa Serikali ni nini tamko lao hasa kwa zile Taasisi za Serikali ambazo hazitimizi kabisa sheria hii? Naomba kujua tamko la Serikali.

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, ningependa kufahamu kwamba ni kweli kwamba Waraka huo Na.3 ambao unaruhusu watumishi wa Serikali kupewa mikopo kupitia HAZINA. Ningependa kufahamu kipaumbele kwa watu wenye ulemavu kutokana na changamoto na kama nilivyosema sisi wote ni walemavu watarajiwa na hasa ajali

siku hizi zimekuwa ni changamoto kubwa. Sasa, je, ni mkakati gani mahsusi unaandaliwa ili basi watu wenye ulemavu wakapewa kipaumbele kwa sababu inasemwa tu ila ukienda kwenye maandishi hamna?

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mollel. Umeeleweka. Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa, majibu ya swali hilo tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali madogo mawili ya nyongeza yote kwa pamoja ya Mheshimiwa mdogo wangu Amina Mollel, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kipekee naomba nimpongeze sana yeye kama mwakilishi wa walemavu hapa Bungeni kwa jinsi amnbavyo anafuatilia sana kwa karibu masuala yote yanayohusu walemavu nchini, lakini vile vile naomba niliambie Bunge lako tukufu kwamba kila binadamu ana ulemavu unaoonekana na usionekana na kila binadamu pia ni mlemavu mtarajiwa.

Mheshimiwa Spika, nikianza kujibu hayo maswali yake mawili madogo ya nyongeza kwa pamoja, amezungumzia Serikali tuna mikakati gani. Naomba niliambie Bunge lako Tukufu kwamba Miongozo yote inayotolewa na Serikali iko kisheria, kisera, kikanuni mbalimbali katika kuboresha ufanisi wa kazi Serikalini. Kwa maana hiyo, kama tamko la Serikali niwaagize waajiri wote nchini kuhakikisha kwamba wanazingatia hii miongozo yote ambayo inatolewa na Serikali kwa maana ya kwamba iko kikanuni, kisheria na sera mbalimbali na wasipozingatia hivyo watachukuliwa hatua kali za kisheria. Nasema hivyo, kwa sababu sisi kama Serikali sasa hivi tumejipanga kuhakikisha kwamba tunatumia *Monitoring and Evaluation (M&E)* kuhakikisha wale ambao hawafuatilii hii miongozo wanajitafsiria wenyewe wanavyotaka au labda hii miongozo hawafuati basi watachukuliwa hatua kali za kisheria.

Mheshimiwa Spika, vile vile naomba niseme kabisa kwamba, kama Serikali katika ile Kanuni ya Sekretarieti ya Ajira Kanuni ile ya mwaka 2019 tumezingatia sana walemavu kwamba hata kama ni kwenye ajira, endapo huyu mlemavu amegongana katika usaili na mtu ambaye hana ulemavu basi huyu mwenye ulemavu atapewa kipaumbele.

Vilevile hata kama kuna ajira yoyote, huyu mlemavu anatakiwa anapo-*apply on line* anatakiwa kuzungumza nini ulemavu wake ili mazingira rafiki yaweze kufanywa. Taasisi yoyote ambayo ina watumishi zaidi ya 20, basi tumewaagiza kutokana na Mwongozo kwamba watenge asilia tatu kwa ajili ya walemavu na haya yote pia yanafanyika hata katika ule mkopo ambao ni wa Mfuko Maalum kwa watumishi wa Serikali. Ahsante.

Mheshimiwa Spika, vilevile hata kama kuna ajira yoyote huyu mlemavu anatakiwa anapo *apply on line* anatakiwa kuzungumza nini ulemavu wake ili mazingira rafiki yaweze kufanywa. Na Taasisi yoyote ambayo ina watumishi zaidi ya 20 basi tumewaagiza kutokana na Mwongozo kwamba watenge asilia tatu kwa ajili ya walemavu na haya yote pia yanafanyika hata katika ule mkopo ambao ni wa mfuko maalum kwa watumishi wa Serikali, ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri an Serikali kwa ujumla, ulemavu upo katika makundi mengi, na kuna ulemavu ambao sasa hivi ni tatizo ni janga na hasa kwa mfano vijana wa kiume matatizo mengi, sasa hizi sera ziwaguse pia na hilo kundi maalum, nafikiri mmenielewa Waheshimiwa Wabunge. Sasa tunaye Balozi wa walemavu hapa nchini Mheshimiwa Mwamoto uliza swali lako.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi, Serikali inapoajiri hasa watu wasioona inajua kabisa wanahitaji wasaidizi, lakini wakati wa kulipawa mishahara huwa hawalipwi na Serikali bali wanalipwa na wale watu wenye ulemavu.

Sasa haioni sasa imefikia wakati aidha, kutunga sera au kuwaweka hao wasaidizi wa watu wenye wasioona ili walipwe nao mshahara?

**SPIKA:** Swali hilo hilo ni muhimu na ni zuri sana sisi Bunge tukiwa na Mbunge katika wasiyoona tunampa msaidizi, kwanini Serikali haifanyi hivyo, majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa kaka yangu Venance Mwamoto, Balozi wa walemavu nchini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli swali lake ni la muhimu sana kwa walemavu wote wenye wasaidizi ambao huwa wanatoa pesa yao wenyewe kuwalipa hao wasaidizi na walemavu wenyewe unakuta kwamba wengine hawaoni. Lakini naomba niseme kama nilivyojibu kwenye maswali yangu mawili ya nyongeza kwamba tunaandaa miongozo mingine katika kuboresha na tayari tumekutana na wadau mbalimbali na Wizara mbalimbali ikiwemo Ofisi ya Waziri Mkuu (Wenye Ulemavu), Wizara ya Elimu, Wizara ya Afya na sisi wenyewe Utumishi kuona na kuangalia ni jinsi gani tunavyoweza kuboresha kanuni, Sheria mbalimbali ili tuweze kuangalia hata hilo ambalo Mheshimiwa Mwamoto amesema kwa sababu na lenyewe ni la muhimu na tunalipokea kwamba tutaliweka katika ajenda ambazo vikao vinaendelea, ahsante.

**SPIKA:** tunaenda Viwanda na Biashara Waheshimiwa Wabunge swali linauliza na Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed upande wa CUF, Mheshimiwa Rukia uliza swali lako tafadhali.

Na.104

**40% Kuajiriwa Sekta ya Viwanda Ifikapo 2020**

**MHE. RUKIA AHMED KASSIM** aliuliza:-

Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alisema kwamba ifikapo 2020 asilimia 40 ya Watu wawe wameajiriwa katika sekta ya Viwanda na sasa hivi ni mwaka 2018.

Je, Serikali ina mpango gani wa kutekeleza kauli hiyo kwa wakati?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara majibu tafadhali.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kutokana na takwimu zilizotolewa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu yaani *NBS* kwenye Kitabu cha Hali ya Uchumi cha mwaka 2018 zinaonyesha kuwa ajira katika Sekta ya Viwanda imeongezeka kutoka watu 254,786 mwaka 2015 hadi kufikia watu 306,180 mwaka 2018, ikiwa ni ongezeko la watu 51,395 sawa na asilimia 20.17. Hata hivyo, ajira hizo ni za moja kwa moja mbali na zile zinazotokana na mnyororo mzima wa thamani kama vile; usafirishaji, huduma za vyakula na malazi. Ni imani yangu kuwa ajira zitaendelea kuongezeka kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, ili kuweza kuongeza kasi ya Ajira kutokana na mchango wa Sekta ya Viwanda, Wizara yangu imeelekeza nguvu kubwa katika uhamasishaji wa uanzishwaji na uendelezaji wa viwanda vidogo, vya kati na vikubwa katika mnyororo wa thamani. Aidha, Serikali itaendelea kuweka mazingira wezeshi pamoja na kubuni mikakati mbalimbali ili kuwezesha wajasiliamali wa ngazi zote na hivyo kuchangia ipasavyo katika kuongeza ajira.

**SPIKA:** Mheshimiwa Bashungwa siku hizi tunaenda na teknolojia na wewe ni Waziri kijana tunatumaini itakuwa mara

ya mwisho kuja na *hard copies*, Mheshimiwa Rukia swali la nyongeza.

**MHE. RUKIA AHMED KASSIM:** Mheshimiwa Spika, ahsante pamoja na majibu mazuri ya Mheshimwia Naibu Waziri, lakini bado nina maswali mawili ya nyongeza. Sekta ya Viwanda ni sekta ambayo ina ajiri watu wengi na inategemewa sana, lakini kuna baadhi ya viwanda vinafungwa kutokana na ongezeko la kodi pamoja na sababu nyingine.

Je, Serikali ina mkakati gani ya kuhakikisha viwanda vyote ambavyo vinatoa ajira kubwa kwa watu wetu vinaendelea kufanya kazi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili watanzania walio wengi wajasiliamali wana nia ya dhati ya kuanzisha viwanda vidogo vidogo mbalimbali, lakini wanashindwa kufanya hivyo kutokana na changamoto ambazo zinawakabili kama vile kukosa mitaji, pamoja na mikopo ambayo inakuwa na masharti magumu.

Je, Serikali ina mkakati gani kuhakikisha watanzania hawa wajasiliamali wanatimiza ndoto zao?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri tafadhali.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza la Mheshimiwa Rukia ni kwamba zipo changamoto za utitili wa kodi katika kufungua viwanda, na nipende kumwambia Mheshimiwa Rukia pamoja na Waheshimiwa Wabunge kwamba Serikali imelitambua hilo na ukiangalia *blue print* mkakati wa *blue print action plan* yake utitili wa kodi na kodi kero zote zimeorodheshwa katika mpango huo na Serikali tayari imeshaondoa kwenye bajeti ya mwaka wa fedha 2019/2020

kodi 54 zimeshaondolewa na tunaendelea na jitihada ya kuhakikisha maeneo ambayo yameainishwa ambayo ni kero kwa viwanda na wafanyabiashara nchini kwenye *blue print* tutawaletea *bill,* Muswada wa Sheria hapa Bungeni ambao unajulikana kwa *business facilitation bill* ili kuweza kuchukua yale maeneo ambayo yako kwenye *blue print* yaingie kwenye Sheria ili tuzidi kuweka mazingira mazuri ya kujenga viwanda na kufanya biashara nchini.

Mheshimiwa Spika, swali la pili ni kuhusu changamoto za wajasiliamali hasa hasa kwenye mitaji na mikopo, pamoja na Waheshimiwa Wabunge jambo hili Serikali inalifanyia kazi kupitia Taasisi mbalimbali Benki ya Kilimo, Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Ofisi ya Waziri Mkuu na zile asilimia kumi kwenye halmashauri zetu ambapo kuna asilimia mbili za watu wenye ulemavu, asilimia nne ya wakinamama na asilimia nne ya vijana.

Pia ndani ya Serikali tunaangalia namna bora ya *scronize* mifuko hii ili iweze kuwasaidia vijana na akinamama katika kuwapatia mikopo yenye riba nafuu, nashukuru.

**SPIKA:** Ahsante sana tunaendelea na Wizara ya Ujenzi Uchukuzi na Mawasiliano, swali linauliza na Mheshimiwa Alex Raphael Gashaza Mbunge wa Ngara.

Na. 105

**Barabara Inayounganisha Rwanda na Tanzania**

**MHE. ALEX R. GASHAZA** aliuliza:-

Barabara ya Rusumo mpakani – Murukulazo – Ngara mjini yenye urefu wa km. 24 ni barabara inayounganisha nchi jirani ya Rwanda na Tanzania hususani Makao makuu ya Wilaya ya Ngara kwa upande wa Tanzania.

Je, ni lini Serikali itajenga barabara hii muhimu kwa kiwango ikiwa ni pamoja na ujenzi wa daraja eneo la mto Ruvuvu unaokatiza katika barabara hiyo eneo la Rusumo feri.

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Mheshimiwa Elias John Kwandikwa tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Alex Raphael Gashaza, Mbunge wa Ngara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Rusumo mpakani–Murukulazo hadi Ngara mjini ni barabara ya mkoa inayosimamiwa na Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)* Mkoa wa Kagera. Barabara hii ina urefu wa kilometa 22.65 ambapo kilometa 21.62 ni za kiwango cha changarawe na kilometa 1.03 katika eneo la Ngara mjini ni za kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa barabara hii kiuchumi na kijamii. Kwa kutambua umuhimu huo, Serikali imekuwa ikitoa fedha kila mwaka kuhakikisha kuwa barabara hiyo inafanyiwa matengenezo ili iwe inapitika wakati wote. Katika mwaka wa fedha 2019/2020, Serikali imetenga jumla ya Shilingi milioni 127.966 ili kufanya matengenezo mbalimbali katika barabara hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Wizara yangu haina mpango wa karibuni wa kujenga Daraja la Mto Ruvuvu na barabara hiyo kwa kiwango cha lami. Aidha, Wizara yangu kupitia Wakala wa Ufundi na Umeme *(TEMESA)* itaendelea kukihudumia kivuko kilichopo cha Mv Ruvuvu ili kiendelee kutoa huduma kwa wananchi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Gashaza Serikali haina mpango wa kujenga daraja swali la nyongeza.

**MHE. ALEX R. GASHAZA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza, ni kweli kwamba barabara hii kipande cha kilometa 22.65 kiko

chini ya wakala wa barabara *TANROAD*. Lakini barabara hii inaweza kuwa barabara ya kimataifa kwa sababu inaunganisha nchi tatu, nchi ya Rwanda, Nchi ya Tanzania kupitia Makao Makao Makuu ya Wilaya Ngara na Nchi ya Burundi kupitia *border* ya Rwanda ni *shortcut* kilometa 50 tu, ukilinganisha na mzunguko uliopo wa kutoka Rusumo, Benako, Ngara Mjini kwenda Kabanga kilometa 84, Serikali haioni kwamba upo umuhimu kutokana na sera ya kuunganisha barabara zinazounganisha nchi na nchi kwa kiwango cha lami kwamba kipande hiki kilichobaki cha kilometa 21 kijengwe kwa kiwango cha lami? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili kwa kuwa kipo kivuko hiki cha MV Ruvuvu ambacho sasa kinatoa huduma mpaka saa moja za jioni, Serikali kupitia Wakala wa Ufundi na Umeme *(TEMESA)* hawaoni kwamba upo umuhimu wa kuongeza sasa masaa ya kivuko hiki kitoe huduma mpaka saa tano ukizingatia kwamba upo mradi mkubwa unaoendelea wa umeme Rusumo na *movement* za watu ni kubwa wanapata shida hasa kivuko kinapofunga huduma mapema?

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Gashaza, majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Elias Kwandika.

**NAIBU WAZIRI, UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Gashaza kwa juhudi kubwa anazozifanya. Nikianza na swali lake la kwanza la kuhusu kivuko, tumeweka kivuko kipya pale Ruvuvu kama nilivyosema katika jibu langu la msingi na kuna kivuko kilikuwepo zamani ambacho kimsingi Mheshimiwa Gashaza pamoja na wananchi wa Ngara wamefanya juhudi ya kutengeneza barabara ili kivuko cha zamani tukipeleke maeneo ya Mayenzi Kanyenye. Kwa hiyo nakupongeza sana kwa juhudi hizo na sisi kama Serikali tuna kuunga mkono kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuongeza safari pale kwenye kivuko cha Ruvuvu tulishatoa maelekezo kwamba tuongeze safari pale ili huduma ziwe nyingi zaidi na hasa

wakati usiku na pia tulitoa maelekezo kwamba tufunge taa pale ili sasa huduma za usiku zikifanyike pia pawe salama zaidi. Kwa hiyo, tutaendelea kulisimamia hili kwa haraka tuweze kufanya hivyo ili huduma ziongezeke katika hilo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara hii utakubaliana na mimi kwamba barabara iko kwenye kiwango kikubwa sana ni kizuri hata wewe mweyewe wakati nimekuja kutembea maeneo haya ulitumia dakika kumi tu Ngara Mjini kuja kule kwenye kivuko, kwa maana ya kwamba tunaendelea kukifanyia matengenezo makubwa.

Mheshimiwa Spika, niseme kuhusu kuboresha na kufanya barabara hii itumike kama barabara ya kuunganisha kati ya Burundi na Rwanda na kwa sababu pia kuna maeneo kumekuwa na changamoto ya kupitisha magari makubwa sehemu za Mjini, na naomba ukubaliane na mimi kwamba barabara ya kutoka Ngara kwenda Benako iendelee kutumika na magari makubwa yale ambayo yanatoka Burundi na kwa maana hiyo tukiboresha barabara hii hata kwa kiwango cha lami siku za usoni lakini magari magodo yapite kwenye eneo hili ili tusiwe na usumbufu eneo la Mjini ya kupitia magari makubwa na imejitokeza changamoto nyingi kama magari makubwa yatapita pale Mjini kunaweza kuwa na hatari kubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo tutaendelea kusimamia barabara kutoka Ngara kwenda Benako iwe nzuri wenzetu wanaotoka Burundi wapiti vizuri na magari mengine madogo yanaweza kupita kwenye kivuko hiko, ahsante sana.

**SPIKA:** Nilikuwa Mheshimiwa Sesili Pareso na Mheshimiwa Nchambi utafuata.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza, kuna barabara ya muda mrefu ambayo inaunganisha Mkoa wa Manyara na Mkoa wa Arusha ambayo inatokea Karatu, Kilimakunda mpaka Mbulu haijajengwa kwa kiwango cha lami.

Je, ni lini barabara hii itajengwa kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Karatu, Mbulu haina lami tafadhali Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Spika, ni kweli muda mrefu barabara jitihada ya kuitengeneza kiwango cha lami ipo, na ukweli kwamba barabara hii imefanyiwa usanifu na kuna kazi ilikuwa inaendelea kukamilishwa ili kutoka Karatu, Kilimapunda, Mbulu, Dongobeshi, Haydom ipite Sibiti iende mpaka Mwanza. Na niseme katika Bunge lako tumepisha fedha kuanza ujenzi sehemu ile ya Mbulu kuja Haydom, kuja Dongobeshi itaanza kujengwa; kwa maana hiyo sasa tunatambua umuhimu kadri tunavyopata pesa tutaendelea kuijenga barabara hii yote ili iweze kuwa kwa kiwango cha lami.

**SPIKA:** Nilikutaka Mheshimiwa Nchambi swali fupi.

**MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa niaba ya wananchi Shapu wa Jimbo la Kishapu kwa kuwa Serikali imekuwa na ahadi ya muda mrefu ya ujenzi wa barabara ya kutoka Kolandoto kwenda Kishapu.

Je, Mheshimiwa Waziri uko tayari sasa kunipatia majibu yenye matumaini kwa wananchi Shapu wa Kishapu juu ya ujenzi wa barabara ya lami kutoka Kolandoto kwenda Kishapu?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Kolandoto Kishapu, Mheshimiwa Naibu Waziri Ujenzi.

**NAIBU WAZIRI, UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Nchambi kwa juhudi kubwa sana anazozifanya katika kusimamia mambo mbalimbali na eneo hili la Kishapu linazalisha sana mazao pamba, pia linazalisha almasi, lakini juhudi za Mheshimiwa Mbunge

zinaonekana. Niseme tu barabara hii anayoitaja Mheshimiwa Mbunge kutoka Mwangongo, Kaulandoto itakuwa ni sehemu ya barabara hii ambayo inayopita Sibiti kwa maana tuna kipande cha kuja Kolandoto kwenda mpaka Sibiti lakini kiko kipande kingine kutoka Mwananuzi kuja Maswa. Kwa hiyo ni sehemu ya barabara hii ambayo ni muda mfupi nimejibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Paresso.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Nchambi nikuhakikishie tu kwamba hizi kilometa 50 na kidogo kutoka Mwangongo kuja Kolandoto tutaanza kufanya ujenzi kidogo kidogo kadri tunapopata pesa, na tumejipanga na pia kufanya maboresho makubwa kwenye Mji wa Kishapu kwa sababu ni Makao Makuu haina barabara ya lami pale tumejipanga tutaanza na kilometa kadhaa pale nafikiri tuonane baadaye kwa sababu ni Mbunge wa Shinyanga mwezangu ili saa nyingine uone pia kwa ukubwa wake tumejipangaje kuboresha Mji wa Kishapu pamoja na barabara hii uliyoitaja, ahsante sana.

**SPIKA:** Nilikuwa Mheshimiwa Dkt. Stephen Kiruswa swali la mwisho la nyongeza kwenye eneo hili.

**MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza na pamoja na swali naomba nitumie fursa hii kuishukuru Serikali kwa sababu ya ujenzi wa barabara ya lami inayotoka Sanya Juu Wilaya ya Siha kuelekea Rombo kupitia Vijiji sita vya Wilaya ya Longido ikiwepo Eleray ambayo imeshafikiwa na lami hilo Olomoloko, Nyalan'gwa, Kitenten, likwaswa na Kamwanga swali langu ni kwamba.

Je, barabara yenye kilometa 56 inayounganisha Wilaya ya Longido na Wilaya ya Siha ambayo sasa inapitiwa na hiyo barabara West Kilimanjaro ambayo ni moja ya barabara iliyohaidiwa katika ilani ya chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015/2020 itaanza kujengwa lini?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo kwa kifupi itaanza kujengwa lini barabara hiyo sijui kama umeshafika huko Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, UJENZI, UCHUKUZI NAMAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Spika, ni kweli nimeshafika maeneo haya na nimekagua barabara hii kutoka Aleray Kamwanga, tumebakiza kilometa 44 tufike Kamwanga na Mheshimiwa Mbunge utakubaliana na mimi. Lakini na kile kipande cha kutoka maeneo hayo kwenda Longido kiko kwenye mpango, nafikiri hata kwenye bajeti kitabu chetu ninacho hapa Mheshimiwa Mbunge tuonane tu ili tupitie. Lakini tunajipanga tulikuwa tunakwenda hatua kwa hatua baada ya kukamilisha ujenzi wa barabara hii mpaka Aleray tunakuja sasa kwenda hatua nyingine kujenga barabara hii Mheshimiwa Mbunge unayoitaja.

**SPIKA:** Tunaenda Wizara ya Maji swali linaulizwa na Mheshimiwa Fratei Gregory Massay Mbunge wa Mbulu Vijijini uliza swali lako Mheshimiwa.

Na. 106

**Utekelezaji wa Ahadi ya Kuchimba Kisima Hydom**

**MHE. FLATEI G. MASSAY** aliuliza:-

Serikali iliahidi kuchimba kisima katika Mji mdogo wa Hydom na kumalizia miradi ya Visima Jimbo la Mbulu Vijijini. Je, ni lini Serikali itatimiza ahadi hiyo ili kumtua Mama ndoo kichwani.

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Maji, Mheshimiwa Jumaa Hamidu Haweso.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Flatei Gregory Massay Mbunge wa Jimbo la Mbulu Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mji wa Hydom unapata maji kutoka vyanzo vya visima virefu vitatu (kimoja kinaendeshwa kwa jenereta na visima viwili kwa umeme wa *TANESCO)*. Kupitia vyanzo hivyo yamejengwa matenki ya kuhifadhia maji matatu yenye jumla ya ujazo wa lita 555,000, vituo vya kuchotea maji 36, vinywesheo vya mifugo vitatu (3), na mtandao wa mabomba wenye urefu kilomita 34.12. Mradi huu unanufaisha watu binafsi 399 na Taasisi 14.

Mheshimiwa Spika, Serikali ipo katika harakati za kuongeza upatikanaji wa maji katika mji mdogo wa Hydom. Hivi sasa, Wakala wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini *(RUWASA)* ipo kwenye hatua za mwisho za kukamilisha uchimbaji wa visima virefu sita vya maji katika vijiji vya Ng'orati, Genda, Maretadu Juu, Labay, Garbabi na Endahagichan ambapo kazi ya uchimbaji imefanyika na kazi iliyobaki ni kusafisha kisima cha Garbabi pamoja na kufanya *pump test* na kupima ubora wa maji katika visima hivyo. Mradi huu unategemea kukamilika mwezi Januari, 2020.

Mheshimiwa Spika, mipango iliyopo ni kuendelea kutafuta vyanzo zaidi vya maji ili kuongeza kiwango cha upatikanaji wa maji kufikia asilimia 85% ifikapo 2020. Wizara kupitia Wakala wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (*RUWASA*) itatuma wataalam wa kufanya utafiti wa maji chini ya ardhi, ikifuatiwa na kufanya usanifu wa mradi ili kufahamu gharama za ujenzi*. (Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Massay, nimekuona. Swali la nyongeza tafadhali.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *DDCA* walikuja wakachimba visima sita na bado hawajaweka *pump* na sasa pia *DDCA* wamepata visima nane na je, lini watafanya au kumaliza kazi hiyo ya kumalizia visima hivi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili Jimbo la Mbulu Vijijini liko juu ya Bonde la Ufa na vijiji vingi vina shida sana ya maji: Je, Serikali itakuja na mpango gani ili kuhakikisha ya kwamba

tunatimiza ile *slogan* ya kumtoa au kumtua mama ndoo kichwani? *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, nampongeza Mheshimiwa Mbunge, amekuwa mfuatiliaji mkubwa sana katika suala la maji kana kwamba ni Mhandisi wa Maji. Kikubwa ambacho nataka kusema, utekelezaji wa miradi ya maji unategemeana na fedha.

Mheshimiwa Spika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tumepata fedha zaidi ya shilingi bilioni 20 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji katika mikoa 17 na Mkoa wa Manyara ni moja ya Mkoa wa wanufaika. Katika Jimbo lake, zaidi ya shilingi bilioni 1.3 tumeshazipeleka kwa ajili ya kutatua tatizo la maji katika maeneo matatu.

Moja, katika Kijiji cha Maganga Juu na Kijiji cha Dongobeshi. Yote ni katika kuhakikisha tunapeleka huduma hii ya maji. Pia tumewapa fedha zaidi ya shilingi milioni 135 kwa ajili ya kukarabati vituo ambavyo havitoi maji ili wananchi wapate maji.

Mheshimiwa Spika, kubwa, namsisitiza Mhandisi wa Maji wa Mbulu afanye kazi kwa sababu fedha ipo, kama akishindwa, basi tutamtafutia kazi ya kufanya. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu nimekuona.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Moja ya Wilaya yenye matatizo makubwa ya maji ni Wilaya ya Hanang na kuna wakati Serikali ilikuwa imetenga shilingi bilioni 1.2 kwa ajili ya maji ya Maskta, Maskaroda na Malama, lakini mpaka leo sidhani hata kama shilingi milioni moja imepelekwa.

Mheshimiwa Spika, naomba sana Mheshimiwa Waziri anieleze, badala ya kwenda kwenye Bonde ambalo ni karibu na ule mradi uliotengwa: Je, ni lini sasa zile hela zilizotengwa na Serikali katika bajeti iliyopita italetwa ili watu wa Malama waweze kupata maji?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, sijui kama umeshafika huko Maskata, Maskaroda.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nikiri nimeshafika katika Jimbo la Mheshimiwa Mbunge na anafanya kazi kubwa na nzuri katika Jimbo lake. Kama nilivyozungumza awali, utekelezaji wa miradi ya maji inategemeana na fedha na tumepata fedha kutoka Benki ya Dunia zaidi ya shilingi bilioni 120 na mmoja wa mkoa wa wanufaika ni Mkoa wa Manyara.

Mheshimiwa Spika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba fedha tumeshashazipeleka na ninaomba tuonane baada ya hapa ili tufanye mawasiliano katika kuhakikisha anazifuatilia na kwenda kutekeleza kazi kama ilivyopangwa.

**SPIKA:** Bado tuko Wizara ya Maji, Swali la Mheshimiwa Omari Kigua. Waheshimiwa kwa sababu ya muda ndiyo maana tuwiane radhi.

Na. 107

**Kutatua Changamoto ya Maji - Kilindi**

**MHE. OMARI M. KIGUA** aliuliza:-

Wilaya ya Kilindi yenye Vitongoji 613 na Vijiji 613 haina mto wala ziwa:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuipatia Wilaya hiyo mradi mkubwa wa maji kutoka Mto Pangani ili kutatua changamoto ya maji?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo la wana Kilindi Mheshimiwa Naibu Waziri Maji, nakukumbusha pia masuala ya *e-parliament* Waziri kijana.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua, Mbunge wa Kilindi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua tatizo kubwa la huduma ya maji linaloikabili Wilaya ya Kilindi kutokana na kutokuwa na mito wala maziwa yanayotumika kwa ajili ya shughuli za binadamu na wanyama kwa kipindi cha mwaka mzima na vyanzo vikuu vya maji katika Halmashauri hiyo ni maji yaliyopo chini ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na changamoto hiyo, Serikali ilichimba visima vinne katika Miji ya Songe na Bokwa ambapo katika Mji wa Bokwa tayari huduma ya maji inapatikana kwa wananchi waishio maeneo hayo na katika Mji wa Songe tayari usanifu umekamilika ili kujenga miundombinu ya usambazaji maji. Aidha, kwa upande wa huduma ya maji vijijini kuna visima vifupi 67 na visima virefu 13 vinavyotoa huduma ya maji kwa maeneo mbalimbali ya vijiji pamoja na malambo 12 ya maji.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali inakarabati mradi mkubwa wa Kitaifa wa *HTM* unaotoa maji Mto Pangani ili kuendelea kuboresha upatikanaji wa huduma ya maji kwa wakazi wa Wilaya ya Handeni na baadhi ya Vijiji vya Wilaya ya Korogwe. Serikali itafanya tathmini ya kina kuangalia uwezekano wa ukarabati wa mradi huo endapo baadaye utaweza kuwanufaisha wananchi wanaoishi Wilaya ya Kilindi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Omari Kigua, swali la nyongeza tafadhali.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Namshukuru Naibu Waziri kwa majibu ambayo kwa kweli

kimsingi hayajaniridhisha hata kidogo. Kwa sababu swali la msingi ilikuwa ni kuomba mradi mkubwa wa maji, lakini majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri hayaoneshi wala hayatoi matumaini kabisa kwamba Serikali inaweza kutoa maji kutoka Mto Pangani hadi Kilindi kwa sababu idadi ya visima ambavyo vimeainishwa hapa, hili ni suala la muda tu:-

Je, Serikali haionai kwamba kuna ulazima wa kuchukua maji kutoka Mto Pangani hadi Kilindi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, namwomba Mheshimiwa Naibu Waziri aangalie namna ya kufanya *verification* ya hivi vijiji 67 kwamba vinatoa maji. Ni kwamba majibu haya siyo sahihi hata kidogo. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu. Umeambiwa majibu ya mwanzo siyo sahihi Mheshimiwa.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kazi nzuri anayoifanya, lakini nami pia ni miongoni mwa kijana wa Mkoa wa Tanga, sipo tayari katika kuhakikisha kwamba tunawaumiza wananchi wa Mkoa wa Tanga.

Mheshimiwa Spika, sisi kama Wizara ya Maji, tunatekeleza mradi wa kuyatoa maji Pangani na kuyapeleka Handeni. Ninachotaka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge, hii ni safari moja na safari moja huanzisha nyingine. Maji yatakapofika Handeni, lazima tuyapeleke Kilindi na mpango wa Wizara yetu ya Maji ni kuhakikisha tunatumia vyanzo vikubwa katika kuhakikisha tunatatua tatizo maji kabisa.

Mheshimiwa Spika, namwagiza Katibu Mkuu kuhakikisha wanafanya tathmini ya Mradi wa Mto Pangani ili wananchi wa Kilindi waweze kupata maji safi, salama na yenye kutosheleza. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa, muda uliobaki ni mdogo sana na tuna maswali mawili ya kumalizia, naomba tusameheane. Tunaelekea Wizara ya Afya, Maendeleo ya

Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ambayo ina maswali mawili ya kujibu. Kwanza swali la Mheshimiwa Ritta Enespher Kabati, Mbunge wa Viti Maalum Iringa, uliza swali lako Mheshimiwa.

Na. 108

**Kuwapatia Watu Wenye Ulemavu Matibabu Bure**

**MHE. RITTA E. KABATI** aliuliza:-

Kundi kubwa la Watu Wenye Ulemavu wana vipato duni:-

Je, Serikali haioni sasa ni muda muafaka kuwatambua na kuwapatia vitambulisho ili waweze kutibiwa bure kama wazee?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Dkt. Ndugulile tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ritta Enespher Kabati, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara imefanya mapitio ya Sera ya Afya ya mwaka 2007 na kuandaa mapendekezo ya Sera Mpya ya Afya ya Mwaka 2019. Katika mapitio ya Sera ya Afya ya Mwaka 2007, changamoto mbalimbali za matitabu kwa makundi ya misamaha ziliibuliwa na watoa huduma pamoja na watumiaji wa huduma hizo.

Mheshimiwa Spika, moja ya changamoto iliyojitokeza ni hospitali zetu kuwa na wagonjwa wengi wa msamaha na hivyo kushindwa kuboresha huduma za afya. Kutokana na changamoto hiyo ya kuwa na makundi mengi ya msamaha, Wizara yangu iliona ni vyema ikaboresha utaratibu wa

misamaha kwa kuhakikisha kuwa wananchi wasio na uwezo tu ndio wanaopatiwa msamaha.

Mheshimiwa Spika, katika mapendekezo ya Sera Mpya ya 2019 kila mwananchi mwenye uwezo atapaswa kugharamia huduma za afya. Sera pendekezwa inaainisha njia mahususi zitakazowezesha Serikali kubaini wananchi wote wenye uwezo ili waweze kuchangia gharama kabla ya kupokea huduma. Kwani ni wazi kuwa siyo kila mlemavu ana kipato duni. Hivyo, wananchi watakaothibitika katika maeneo yao kuwa hawana uwezo wa kuchangia ikiwemo walemavu, wataendelea kupata matibabu pasipo wao kuchangia.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa, Serikali inaendelea na maandalizi ya Bima ya Afya kwa wananchi wote. Pindi taratibu zikikamilika, Muswada utawasilishwa Bungeni.

**SPIKA:** Mheshimiwa, swali linahusu kuwatambua na kuwapatia vitambulisho walemavu. Swali la nyongeza Mheshimiwa Ritta Kabati.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali madogo ya nyongeza. Kwanza kabisa nina imani na Serikali hii ya Awamu ya Tano kwamba yote yanawezekana siku moja watu wenye ulemavu basi wataweza kupatiwa hivyo vitambulisho. Pia nawapongeza Waheshimiwa Mawaziri kwa kazi nzuri. Naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mahitaji makubwa sana kwa watu wenye ulemavu hasa wale wa ngozi ni mafuta maalum ambayo yamekuwa yakiuzwa bei ghali sana katika maduka na kushindwa kumudu gharama ya hayo mafuta; na kwa kuwa Serikali ilitoa agizo kuwa Halmashauri zinapoagiza dawa *MSD* ziagize na hayo mafuta:-

Je, nini kauli ya Serikali kwa Halmashauri ambazo zimekuwa hazitii agizo hilo? Kwa sababu watu wenye

ulemavu wamekuwa wakipata mpaka *cancer* kutokana na kukosekana kwa hayo mafuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, kwa kuwa vitanda vya kujifungulia wajawazito siyo rafiki kabisa na watu wenye ulemavu na walemavu wanapokwenda kujifungua wamekuwa wakipata mateso makubwa sana na wengine kupoteza maisha:-

Je, Serikali ina mkakati gani kuhakikisha kwamba inaweka vitanda rafiki vya kujifungulia watu wenye ulemavu kuanzia ngazi ya Zahanati mpaka Hospitali ya Rufaa ili kuwatendea haki watu wenye ulemavu? *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo muhimu, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, ni kweli walemavu wa ngozi wapo katika hatari zaidi ya kupata saratani ya ngozi kutokana na kutokuwa na ile kinga nzuri ya mionzi ya jua. Kama Serikali katika Hospitali ya *KCMC* pale kuna kiwanda kizuri nami nimepata fursa ya kukitembelea ambapo mafuta haya yanatengenezwa kwa ajili ya walemavu. Siku za nyuma katika Bunge lako Tukufu tulishawahi kutoa maelekezo kwa Halmashauri kwamba waweke utaratibu wa kuagiza mafuta haya kupitia katika bajeti zao za dawa na vifaa tiba ambazo wanazipata.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie tena fursa hii kupitia Bunge lako Tukufu kuzikumbusha Halmashauri kubaini mahitji ya walemavu wa ngozi katika maeneo yao na kuhakikisha kwamba mafuta haya ambayo yanawakinga walemavu wa ngozi, basi yanakuwa ni moja ya sehemu ya vitu ambavyo wanaagiza kupitia bohari ya dawa.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili, ameuliza kuhusiana na vitanda ambavyo siyo rafiki sana kwa wajawazito walemavu. Kwanza, napenda sana kumpongeza Mheshimiwa Ritta Kabati, amekuwa ni Balozi mzuri sana na

amekuwa anawasemea watu wenye ulemavu. Hili tumelipokea kama Serikali na tulishatoa maelekezo kwa *MSD* kuhakikisha kwamba vitanda vya kujifungulia ambavyo tunavinunua viweze kukidhi mahitaji ya watu wote, wale wenye uemavu na wale wasiokuwa na ulemavu. Hili tunalo na tunaendelea kulisisitiza kupitia bohari ya madawa.

**SPIKA:** Ahsante Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Waziri hii ya kuwapatia vitambulisho walemavu wote, Mheshimiwa Almasi Maige aliwahi kunipa taarifa wakati fulani kwamba liko tatizo kubwa sana la ulemavu wa upungufu wa nguvu za kiume miongoni mwa Wanyamwezi. Sasa mwandae vitambulisho kwa Wanyamwezi kule wote wenye matatizo hayo wapate vitambulisho. Mheshimiwa Maige hiyo huwezi kujibu tena, nimekuwahi leo. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Catherine Nyakao Ruge, uliza swali lako tafadhali na ndiyo swali la mwisho leo.

Na. 109

**Kupungua Vifo vya Akina Mama**

**MHE. CATHERINE N. RUGE** aliuliza:-

Kwa mujibu wa Ripoti ya *TGHS-MIS* ya 2015/2016 ya masuala ya afya, vifo vya akina mama wakati wa kujifungua *(Maternal Mortality Rate)* vimeongezeka kufikia akina mama 556 kati ya kina watoto 100,000 waliozaliwa hai.

Je, ni nini mkakati mahususi wa Serikali katika kupunguza vifo hivi ikizingatia kuwa bajeti ya Serikali kwa Wizara ya Afya kwa mwaka 2018/2019 imepungua kwa zaidi ya asilimia 19.6?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo tafadhali, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mheshimiwa Dkt. Ndugulile, tafadhali.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Catherine Nyakao Ruge, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto inaendelea na juhudi mbalimbali za kuboresha huduma za Afya ya Uzazi na Mtoto. Kupunguza vifo vitokanavo na uzazi na watoto wachanga ni suala linalopewa kipaumbele katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, dhamira hii inaonekana na kuthibitishwa katika miongozo mbalimbali ya Serikali kama vile, Sera ya Taifa ya Afya ya Mwaka 2007, Dira ya Maendeleo ya Taifa ya Mwaka 2025, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA), Mpango Mkakati wa Nne wa Afya *(Health Sector Strategic Plan IV),* Mkakati wa Kupunguza na Kuimarisha Afya ya Uzazi, Watoto na Vijana *(National Road Map to Improve Reproductive, Maternal, Newborn, Child & Adolescent Health in Tanzania (One plan II)* na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2015.

Mheshimiwa Spika, lengo la Wizara ni kupunguza vifo vya akina mama na watoto vitokanavyo na uzazi kutoka 556 kwa kila vizazi hai 100,000 hadi 292 kwa kila vizazi hai 100,000 na kupunguza vifo vya watoto kutoka 21 kwa kila vizazi hai 1,000 hadi 16 kwa kila vizazi hai 1,000 ifikapo mwaka 2020.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza mikakati hii, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI imeboresha Vituo vya Afya zaidi ya 352 na vingine kujengwa upya ili viweze kutoa huduma za afya ya uzazi kabla, wakati wa ujauzito na wakati wa kujifungua ikiwepo kumtoa mtoto tumboni kwa njia ya operesheni na kuzijengea uwezo wa kuweza kutoa huduma za damu salama kwa watakaohitaji. Aidha, Hospitali mpya 67 za Halmashauri zinajengwa ili huduma ziweze

kuwafikia wananchi wote wa vijijini na mjini kwa usawa na urahisi.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kwamba upatikanaji wa dawa na vifaa tiba vinakuwepo muda wote, Serikali imeongeza zaidi ya mara tisa bajeti ya dawa na vifaa tiba, kutoka shillingi bilioni 31 mwaka 2015/2016 hadi shilingi bilioni 270 mwaka 2018/2019**.** Ongezeko hili la kibajeti na usimamizi imara wa rasilimali vimeongeza upatikanaji wa dawa muhimu katika vituo vya kutolea huduma kutoka asilimia 53% (2015/2016) hadi kufikia asilimia 94% (2018/2019).

Aidha, juhudi hizi zimewezesha wajawazito kuendelea kupata huduma za afya ya uzazi na mtoto ikiwemo kinga tiba dhidi ya Malaria *(SP), Fefol* ambayo ni kinga tiba dhidi ya upungufu wa damu, vipimo vya shinikizo la damu, kaswende, wingi wa damu, sukari na kadhalika. Huduma hizi hupatikana kila siku wajawazito wanapohudhuria Kliniki.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2019 kuelekea 2020 Serikali ina mpango wa kuendelea kuboresha huduma za afya ya uzazi na mtoto kwa kutoa mafunzo kazini kwa watoa huduma ya afya juu ya namna bora ya kutibu matatizo yatokanayo na uzazi na watoto wachanga, kuanzisha benki ya damu salama katika mikoa ambayo vituo vipya vya upasuaji vya kumtoa mtoto tumboni vimejengwa na kuimarisha mpango wa kutoa huduma kamili ya afya ya uzazi na mtoto katika zahanati zote nchini.

Mheshimiwa Spika, tarehe 6 Novemba, 2018 Jijini Dodoma Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan alizindua kampeni ya Jiongeze Tuwavushe Salama ambayo ni kampeni ya Kitaifa inayolenga kuzuia vifo vitokanavyo na uzazi na vifo vya watoto wachanga nchini.

Mheshimiwa Spika, madhumuni ya kampeni hii ni kuhamasisha viongozi wa Serikali, dini, Mashirika yasiyo ya kiserikali, wadau wa maendeleo watoa huduma za afya, familia na jamii kwa ujumla ili kuchangia katika juhudi za Taifa

za kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi na watoto wachanga. Wakuu wote wa Mikoa walisainishwa mikataba ya utekelezaji na ufuatiliaji katika Mikoa yao.

**SPIKA:** Wizara ya Afya, majibu yanakuwa marefu sana. Mheshimiwa Ruge uliza swali.

**MHE. CATHERINE N. RUGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Mwaka 2017 Serikali kupitia Wizara ya Afya ilipata pesa kutoka Benki ya Dunia kwa ajili ya kuboresha vituo 100 nchini ili kupunguza vifo vya akina mama na watoto. Kituo cha Afya Iramba kilichopo Wilaya ya Serengeti kilitengewa shilingi milioni 400 lakini mpaka sasa pesa hizo hazijapelekwa.

Mheshimiwa Spika, napenda kupata majibu, ni lini sasa Serikali itapeleka pesa hizo ili kuweza kukarabati chumba cha kujifungulia pamoja na maabara ya damu ili kupunguza vifo vya akina mama na watoto wa vijiji vya Kinyamonta, Nyagasense, Iramba, Misaga pamoja na Heki?

Mheshimiwa Spika, swali la pili Wizara ya Afya imekuwa ikiwatumia watoa huduma ngazi ya jamii kwa maana ya *WAJA Community Health Workers* katika harakati za kupunguza vifo vya akina mama wakati wa kujifungua pamoja na watoto; kwa kutambua hilo, Serikali iliamua kurasimisha kada hii kwa kuanzisha kozi ya mwaka mmoja kwa ajili ya *(Community Health Workers)* ili kuajiri…

**SPIKA:** Mheshimiwa na wewe tena unaanza tena maswali marefu!

**MHE. CATHERINE N. RUGE:** Mheshimiwa Spika, ili kuwaajiri *WAJA Community Health Workers* lakini *program* hii imesitishwa:-

Je, Serikali haioni haya ni matumizi mabaya ya fedha za walipakodi kwa kuanzisha *program* na kuisitisha kabla ya kutimiza malengo yake?

**SPIKA:** Ahsante sana. Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, tafadhali

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Catherine Ruge, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli hapo awali Kituo hiki cha Afya cha Iramba katika Jimbo/Wilaya ya Serengeti kiliainishwa katika moja ya vituo ambavyo vilitakiwa kupata fedha kwa ajili ya maboresho ili kuweza kutoa huduma za afya ya uzazi. Hata hivyo, baada ya kufanya mapitio na kiwango cha fedha tulichokuwa nacho kituo hiki kilitolewa katika orodha hii. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba bado tunaendelea na uboreshaji wa vituo hivi vya afya na katika awamu ya tano basi kituo hiki nacho kitafikiriwa.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili ameulizia suala la matumizi ya *Community Health Workers. Community Health Workers (*watu wa afya wa jamii) kwetu ni watu muhimu sana, hususan katika mipango yetu ya Serikali. Leo tunafanya uzinduzi wa Mpango wa Kitaifa wa Magonjwa Yasiyoambukiza lakini tuna mipango ya ugonjwa wa UKIMWI, Malaria na Kifua Kikuu na magonjwa mengi. Sisi kama Serikali sasa hivi tuko katika hatua za mwisho kabisa za kukamilisha muundo, taratibu wa jinsi gani ya kuweza kuwatumia hawa *Community Health Workers.* Utaratibu utakapokamilika tutatoa taarifa kwa umma.

**SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, mkiangalia muda wetu mtaona tunapaswa kuendelea na shughuli inayofuata. Naomba niwatambue wageni lakini kabla sijawatambua wageni naomba niwakumbushe Waheshimiwa Mawaziri na Manaibu Waziri naomba mtuunge mkono sana katika matumizi ya mfumo wetu wa *e-parliament.* Kwa hiyo, unapokuja kujibu maswali karatasi mnakuja nazo kama

*backup incase* mtandao wako umeleta shida vinginevyo hatu-*encourage* kuja na makaratasi hapa, hapana. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tunaenda kwenye matangazo yetu. Kwanza naomba kuwatambulisha wageni 24 wa Mheshimiwa Luhaga Mpina, Waziri wa Mifugo na Uvuvi ambao ni Watendaji Wakuu wa Wizara hiyo ambao wamekuja kushuhudia kuwasilishwa kwa Mkataba wa Kimataifa wa *FAO* wa Kuzuia Uvuvi Haramu kupitia bandari za nchi wanachama. Wageni hao ni Katibu Mkuu wa Uvuvi, Dkt. Rashid Tamatamah; Mkurugenzi wa Ukuzaji Viumbe Maji, Dkt. Nazael Madalla; Mkurugenzi wa *TAFIRI,* Dkt. Semvua Mzighani; Mkurugenzi wa Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu *(DSFA),* Dkt. Islam Nchenga; Mkurugenzi wa Sera na Mipango (Uvuvi) Ndugu Sayi Magessa na Mkurugenzi wa Uvuvi, Ndugu Magese Bulayi, naona yeye hajaja, ahsanteni sana na karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri, huyu Magese Bulayi kule Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam tukiwa mwaka wa kwanza tulikuwa tunalala wote chini, tulipewa magodoro ya kulala chini. Aliyetupatia magodoro ni Mheshimiwa Susan Lyimo, alikuwa kule *janitor* kwenye mabweni ya chuo. Kwa hiyo, ka-Susan Lyimo kazamani nako haka. *(Kicheko)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge ni wageni watatu wa Mheshimiwa Doto Biteko, Waziri wa Madini ambao ni wapiga kura wake kutoka Jimbo la Bukombe, Ndugu Benjamin Ngaiwa, Ndugu Mbula Charles na Ndugu Merikizedeck Ndabagoye. Karibuni sana pale mlipo. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Musukuma Kasheku ambao ni Waheshimiwa Madiwani wa Jimbo la Geita; Diwani Kata ya Kakubilo Mheshimiwa Nyanda Igayo na Diwani wa Kata ya Isurwa, Mheshimiwa Maweda Gwesandilyi. Karibuni sana Waheshimiwa Madiwani. *(Makofi)*

Wageni 20 wa Mheshimiwa Hassan Masala ambao ni marafiki zake na walimu kutoka mikoa mbalimbali Tanzania

wakiongozwa na Ndugu Zawadi Sanga. Ooh, karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Wageni watano wa Mheshimiwa George Lubeleje ambao ni walimu na viongozi wa Chama cha Mapinduzi kutoka Mpwapwa, Mkoa wa Dodoma wakiongozwa na Mwenyekiti wa CCM wa Kata ya Chunyu, Ndugu Peter Chilagane. Wale wa kutoka Chunyu karibuni sana na mkirudi Chunyu basi msalimieni Diwani, Mheshimiwa Kongowa Dodo na Mheshimiwa Mbunge wenu Lubeleje yuko amejaa hapa tele. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Zubeir Kuchauka ambaye ni mpiga kura wake mkulima kutoka Liwale Mkoa wa Lindi, Ndugu Juma Lipenga. Karibu sana Juma kutoka Liwale, tusalimie Liwale. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Wilfred Lwakatare ambaye ni mtoto wake kutoka Jijini Dar-es-Salaam Ndugu Lovelet Lwakatare. Ahsante sana Lovelet. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Zainab Mwamwindi ambao ni viongozi wa CCM kutoka Iringa Mjini wakiongozwa na Ndugu Joseph Nzala, Ndugu Salvatory Ngerera na Ndugu Shadrack Masanika. Karibuni sana wageni kutoka Iringa. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Flatei Massay ambao ni madaktari wa Hospitali ya Haydom iliyoko Mbulu, Ndugu Yeconia Zacharia na Ndugu Leokadia Fissoo. Karibuni sana, wale kule wageni wetu toka Hospitali Maarufu ya Haydom. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Hamida Abdallah ambaye ni mume wake kutoka Mkoa wa Lindi, Ndugu Hitesh Mehta. Leo tarehe 14 Novemba, 2019 wanatimiza miaka 30 ya ndoa. Karibu sana Ndugu Hitesh Meta na Mheshimiwa Hamida amekaa upande gani, karibu sana Ndugu Hitesh kutoka kule Lindi. *(Makofi/Vigelegele)*

Wageni waliopo Bungeni kwa ajili ya mafunzo ni madaktari watano kutoka Hospitali ya Taifa ya Muhimbili ambao wameletwa na Ofisi ya Bunge kwa ajili ya kutoa huduma ya afya kwa Waheshimiwa Wabunge na Watumishi wa Bunge katika kipindi hiki cha Bunge wakiongozwa na Dkt. Kennedy Nchimbi. Madaktari karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, madaktari hawa wamekuwepo kwenye kituo chetu cha afya hapa wanatoa huduma za vipimo mbalimbali. Ukiwa unajisikia kuna mahali kidogo panaleta shida tafadhali fika tu pale na wapo hadi kesho. Kwa hiyo, nawaomba tuonane na madaktari wetu hawa wapendwa. *(Makofi)*

Ahsante sana, sasa tuendelee.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Mwongozo, nimekuona Mheshimiwa Goodluck Mlinga.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba Mwongozo kwa busara zako, jana niliomba Mwongozo kuhusiana na gharama halisi za uunganishwaji wa umeme wa *REA,* umeme jazilizi na umeme mwingineo. Kwa kuwa, kumekuwa na kauli za viongozi wetu wakuu akiwemo Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu, hata Mheshimiwa Waziri wa Nishati kuwa gharama ambayo mwananchi anatakiwa alipe ni shilingi 27,000 tu, lakini wananchi wetu wanapoenda katika Ofisi za *TANESCO* wanapotaka kuunganishiwa umeme wanaambiwa gharama tofauti kuanzia shilingi 200,000 hadi shilingi 1,000,000. Waziri bado anasisitiza gharama halisi ni shilingi 27,000 sasa kuna gharama inaitwa *service charge,* hiyo *service charge* wanapima umbali tangu umeme unapotokea mpaka kwenye nyumba yako, yaani wanahesabu zile nguzo lakini wanakwambia nguzo hailipiwi, mita hailipiwi, wala waya haulipiwi. Tunataka kujua kwa maandishi yaani hiyo shilingi

27,000 anayosema Mheshimiwa Waziri iandikwe na mwananchi apewe barua kuwa pesa halisi anayotakiwa kulipa ili apate umeme iwe hiyo, hii *service line* iondoke tupate maandiko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba mwongozo wako kwa mamlaka yako, Waziri atoe maandishi hapa tuondoke nayo. Mimi nitawasaidia hata kuzisambaza hizo barua. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waziri wa Nishati, natumaini umemsikia Mheshimiwa Mbunge, yeye anachosema tu kwamba hebu tupatieni Wabunge wote andiko halisi ili tunapoenda majimboni, kwa sababu ni kweli kuna usumbufu, mnasema kila mahali lakini unapoenda huko utekelezaji tofauti. Tupeni maandishi kama Wabunge ukishalipa shilingi 27,000 hakuna cha nguzo, waya wala vikombe Wabunge ile ndiyo iwe silaha yetu sasa, ndio hoja ya Mheshimiwa.

Mheshimiwa Waziri, kama kuna maelezo tafadhali?

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine tena niendelee kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa hoja hii mahsusi sana yenye manufaa makubwa kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, kwanza *circular* na nyaraka zimeshasambazwa kwa Mameneja wote wa Kanda, Mikoa na Wilaya. Kwa kuwa Wabunge wote wako katika Wilaya ni matumaini yetu kwamba watapata nyaraka hizo. Napenda kutoa maelekezo sasa kwamba Mameneja wote wa Wilaya, Mikoa na Kanda katika maeneo yao wawasilishe nyaraka hizo kwa kila Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Madiwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakubaliana pia na hoja ya kuwapa maandishi Waheshimiwa Wabunge. Hayo maelekezo uliyotoa Mheshimiwa Spika tutayatoa kila Mbunge atatoka na barua hiyo ili anakokwenda aweze kulisimamia vizuri. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Mimi nitalifuatilia jambo hilo kabla ya kesho kuahirisha hapa nitawauliza Wabunge kama kila mmoja tayari ameshapata barua yake kwa sababu jambo hili ni muhimu kweli kwa wananchi na ukifanya mkutano wowote lazima siku hizi utaulizwa maswali yanayohusu umeme.

Sasa Wabunge ni kujikanyaga tu maana huna hakika ukisema hiki huenda labda ni kinyume na mwelekeo wa Serikali sasa ni vizuri wawe na kitu fulani ambacho kinawaongoza waweze kusema *with authority.* Kwa hiyo, mjitahidi *by* kesho tunapoahirisha Bunge kila Mbunge awe na barua yake kabisa inayofafanua ni kitu gani *exactly.*

Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Nishati, tunakushukuru mno kwa hilo. Mheshimiwa Waziri Mkuu pia amejibu swali hapa asubuhi ameeleza kwa ufafanuzi mambo hayohayo, ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, Katibu.

**NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:**

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

Muswada wa Sheria kwa ajili ya Kufanya Marekebisho katika Sheria Mbalimbali zipatazo Kumi na Nne (14) kwa lengo la kuondoa upungufu ambao umejitokeza katika Sheria hizo wakati wa utekelezaji wa baadhi ya masharti katika Sheria hizo *[A bill for An Act to Ammend Certain Written Laws]*

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Baada ya Muswada huo Kusomwa kwa Mara ya Kwanza, sasa natangaza moja kwa moja kwamba Katibu utaupeleka kwenye Kamati ya Katiba na Sheria kwa hatua zinazofuata ili uweze kufanyiwa kazi.

Katibu usome shughuli inayofuata.

**NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**MAAZIMIO**

**Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa *FAO* wa Kuzuia Uvuvi Haramu kupitia Bandari za Nchi Wanachama**

**SPIKA:** Moja kwa moja, naomba nikuite Waziri wa Mifugo na Uvuvi ili uwasilishe Azimio lako. Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Luhaga Mpina, karibu tafadhali.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa *FAO* wa Kuzuia Uvuvi Haramu Kupitia Bandari za Nchi Wanachama *(The Agreement on Port State Measures to Prevent, Deter and Eliminate Illegal, Unreported and Unregulated Fishing-PSMA)*.

KWA KUWA Tanzania ni mwanachama wa Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa *(Food and Agricultural Organisation of The United Nations – FAO)* tangu mwaka 1962 ambalo linaongoza juhudi za kuongeza usalama wa chakula na lishe duniani.

KWA KUWA katika kutekeleza majukumu yake, mwaka 2001 liliandaa mpango mahsusi *(International Plan of Action)* wa kuzuia, kudhoofisha na kuondoa uvuvi haramu katika ukanda wa uchumi wa bahari kuu ambao umetokana na ongezeko la matukio ya uvuvi haramu unaosababisha uharibifu wa ikolojia, upotevu wa rasilimali za uvuvi na kuathiri maisha ya wavuvi na usalama wa chakula na lishe duniani.

NA KWA KUWA kwa kutambua umuhimu wa bandari za nchi wanachama wa *FAO* na kwa kuzingatia uhitaji wa nchi zinazoendelea katika kukabiliana na uvuvi haramu katika ukanda wa uchumi wa bahari kuu, nchi wanachama ziliafikiana kuchukua hatua madhubuti za pamoja

kukabiliana na uvuvi haramu usiotolewa taarifa na usiodhibitiwa kwa kutumia bandari.

NA KWA KUWA yapo baadhi ya mataifa ya kigeni na kampuni zinazokiuka masharti ya kujihusisha na uvuvi haramu kwa kificho kwa kufanya uvuvi usiotolewa taarifa na usiodhibitiwa.

NA KWA KUWA Mkataba wa Kimataifa wa Kuzuia Uvuvi Haramu Usiotolewa Taarifa na Usiodhibitiwa kwa Kutumia Bandari *(The Agreement on Port State Measures to Prevent, Deter and Eliminate Illegal, Unreported and Unregulated Fishing-PSMA)* uliandaliwa na kukubaliwa na nchi wanachama kwa ajili ya kuzuia uvuvi haramu duniani.

NA KWA KUWA lengo la kuzuia uvuvi haramu ni kulinda rasilimali za uvuvi ili kuwa na uendelevu na kuleta faida kwa Taifa husika na kuhakikisha usalama wa chakula na lishe kupitia mkataba wa *PSMA* uliopitishwa katika kikao cha 137 cha Baraza la *FAO* mwezi Oktoba, 2009 na kuridhiwa na nchi wanachama katika Kongamano Na.36 la *FAO* lililofanyika tarehe 18 mpaka 23 Novemba, 2009 Roma, Italia.

NA KWA KUWA Mkataba wa *PSMA* ni muhimu kwa ajili ya kulinda rasilimali za uvuvi zilizopo nchini katika maeneo ya maji ya bahari eneo ambalo linajumuisha maji ya Kitaifa *(Territory Sea)* lenye kilometa za mraba zipatazo 64,000 na Ukanda wa Uchumi wa Bahari Kuu *(Exclussive Economic Zone – EEZ)* lenye kilometa za mraba zipatazo 223,000.

NA KWA KUWA kwa kuridhia mkataba huu nchi itapata manufaa ya kupunguza upotevu wa rasilimali za uvuvi, uharibifu wa mazingira ya bahari kutokana na kuimarika kwa udhibiti wa uvuvi haramu na usimamizi wa matumizi endelevu wa raslimali za uvuvi, kuongeza mchango kwa sekta ya uvuvi katika pato la Taifa, upatikanaji wa masoko ya uhakika ya kimataifa kwa mazao ya uvuvi yanayotoka baharini, kuimarika kwa ushirikiano wa kikanda na kimataifa katika uendelezaji wa rasilimali za uvuvi, kuongezeka kwa fursa za uwekezaji katika sekta za uvuvi na

hivyo kutoa fursa za ajira, kuimarika kwa ukusanyaji na upatikanaji wa takwimu na taarifa mbalimbali zinazohusu uvuvi katika bahari kuu, kuwezesha udhibiti wa uvuvi haramu kati ya nchi wanachama na kuijengea nchi uwezo wa kulinda rasilimali za uvuvi.

NA KWA KUWA nchi zaidi ya 60 duniani zimesharidhia Mkataba huu na Nchi wa Ukanda wa Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi zinazojumuisha Nchi ya Reunion, Kenya, Madagascar, Maldives, Mauritius, Msumbiji, Seychelles, Somalia na Afrika Kusini zimesharidhia mkataba huu.

NA KWA KUWA mkataba unaopendekezwa kuridhiwa unaendana na sheria na miongozo ya kimataifa inayohusu usimamizi wa rasilimali za uvuvi ambazo Tanzania inazitekeleza ikiwemo *United Nations Convention on the Law of the Sea – UNCLOS* ya mwaka 1982, *FAO Code of Conduct for Responsible Fisheries, Indian Ocean Tuna Commission – IOTC* na Malengo Endelevu – *Sustainable Development Goals,* Lengo Na.14, Itifaki ya *SADC* kuhusu Uvuvi, Tamko la Jakarta kuhusu Uchumi wa Bahari Kuu, Mkataba wa *PSMA* na miongozo hiyo inalenga kulinda, kuendeleza, kuhakikisha kuwa rasilimali za uvuvi zinakuwa endelevu kwa ajili ya uhakika wa chakula, lishe pamoja na manufaa ya kiuchumi kwa nchi wanachama.

NA KWA KUWA mkataba huu unaendana na Sera ya Taifa ya Uvuvi ya Mwaka 2015 na Sheria ya Uvuvi, Sura 279 na Sheria ya Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu, Sura 388.

HIVYO BASI kwa kuzingatia manufaa yatokanayo na Mkataba huu kwa Tanzania na kwa nchi wanachama, Bunge hili katika Mkutano wa Kumi na Saba na kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, sasa linaazimia kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa *FAO* wa Kuzuia Uvuvi Haramu Kupitia Bandari za Nchi Wanachama *(The Agreement on Port State Measures to Prevent, Deter and Eliminate Illegal, Unreported and Unregulated Fishing-PSMA)*.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono; tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mheshimiwa Luhaga Mpina kwa wasilisho zuri kuhusiana na azimio tajwa la masuala ya uvuvi. Sasa naomba nimuite Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Kilimo, Mifugo na Maji ili awasilishe taarifa ya Kamati kuhusu azimio hilo. Mheshimiwa Dkt Christine Ishengoma, Makamu Mwenyekiti.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA - MAKAMU MWENYEKITI KAMATI YA KUDUMU YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa mujibu wa Kanuni ya 53 (6) (e) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016 kwa niaba ya wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, naomba kuwasilisha Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu Mapendekezo ya Serikali Kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa *(FAO)* wa Kuzuia Uvuvi Haramu Kupitia Bandari za Nchi Wanachama *(Agreement on Port State Measures to Prevent, Deter and Eliminate Illegal, Unreported and Unregulated Fishing – PSMA).*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuipatia Kamati kazi ya kushughulikia mkataba huu kama ilivyo ada, Kamati ilianza kuchambua mkataba husika kwa kushirikiana na wadau mbalimbali waliofika mbele ya Kamati na wale waliotuma maoni yao kwa njia ya maandishi ili kuweza kufahamu chimbuko la mkataba, vipengele muhimu vilivyoko kwenye mkataba na manufaa yatakayopatikana kwa taifa na kwa nchi wanachama kuridhia mkataba husika.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Tanzania ni miongoni mwa nchi wanachama wa Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa *(Food and Agriculture Organization of the United Nation- FAO*), na kwa kuwa Tanzania ni moja ya nchi zinazopakana na bahari, mwaka 1985 iliridhia Mkataba wa Kimataifa wa Sheria ya Bahari ya Mwaka 1982 (*The United*

*Nation Convention on the Law of the Sea – UNCLOS* 1982), ambao unatoa fursa kwa nchi zinazopakana na bahari kutangaza mipaka ya maeneo ya bahari. Fursa hii inatoa haki kwa nchi hizo kutafuta, kutumia, kuhifadhi na kusimamia rasilimali hai na zisizo hai hadi maili za bahari (N*autical Mile*) 200 kutoka ufukweni.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 1989 Bunge lako Tukufu lilitunga Sheria ya Bahari ya Kitaifa ya Ukanda Maalumu wa Uchumi *(Territorial Sea and Exclusive Economic Zone Act of* 1989; ambayo ilitambua kuwepo kwa maeneo matatu ya Bahari ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Maeneo hayo ni Bahari ya Ndani (*Inner Sea*), Bahari ya Kitaifa (*Territorial Sea*) na Ukanda Maalum wa Uchumi wa Bahari *(Exclusive Economic Zone* EEZ).

Mheshimiwa Spika, Eneo Maalum la Uchumi wa Bahari Kuu *(Exclusive Economic Zone EEZ)* ambapo hufanyika shughuli za uvuvi wa Bahari Kuu na samaki wa asili wanaopatikana katika eneo hili ni wa aina ya Jodari na jamii zake husifika kwa tabia ya kuhama kwa kasi kubwa tena katika makundi kutoka eneo moja la maji ya bahari hadi eneo lingine.

Mheshimiwa Spika, hali hii imepelekea baadhi ya nchi zinazoendelea, kushindwa kunufaika ipasavyo na Uvuvi wa Bahari Kuu kutokana na uwekezaji mkubwa unaohitajika kwenye Uvuvi wa Bahari Kuu. Changamoto nyingine zinazokabili Uvuvi wa Bahari Kuu ni gharama kubwa katika kuendeleza, kusimamia na kudhibiti shughuli za uvuvi ikiwemo Uvuvi Haramu Usiotolewa Taarifa na Kuratibiwa (*Illegal, Unreported and Unregulated – IUU – fishing*).

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua changamoto hii na kwa kuzingatia uhitaji wa nchi zinazoendelea katika kukabiliana na Uvuvi Haramu sehemu za Ukanda wa Uchumi na Bahari Kuu, Nchi Wanachama zikiongozwa na Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (*Food and Agriculture Organization of the United Nation – FAO*) ziliafikiana kuchukua

hatua madhubuti za pamoja za kukabiliana na uvuvi haramu, usiotolewa taarifa na usiodhibitiwa kwa kutumia bandari.

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza adhima hiyo, Mkataba wa Kimataifa wa Kuzuia Uvuvi Haramu, Usiotolewa Taarifa na Usiodhibitiwa kwa Kutumia Bandari (*The Agreement on Port State Measures to Prevent, Deter and Eliminate Illegal, Unregulated Fishing- PSMA*) uliandaliwa na kukubaliwa. Mwaka 2009 mwezi Oktoba uliridhiwa na nchi wanachama kwa ajili ya uzuiaji wa uvuvi haramu.

Mheshimiwa Spika, Madhumuni na Faida za Mkataba wa Kimataifa wa *FAO* wa Kuzuia Uvuvi Haramu Kupitia Bandari za Nchi Wanachama. Lengo kuu la kuzuia uvuvi haramu ni kulinda rasilimali za uvuvi ili kuwa na uvuvi endelevu na kuleta faida kwa taifa husika, na kuhakikisha usalama wa chakula na lishe kupitia Mkataba wa *FAO-PSMA*. Aidha, Mkataba huu ni muhimu kwa ajili ya kulinda rasilimali za uvuvi zilizopo nchini katika maeneo ya maji ya bahari.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Tanzania, Bunge likiridhia Mkataba huu, manufaa yatakayopatikana ni pamoja na:-

(a) Kupungua kwa upotevu wa rasilimali za uvuvi na uharibifu wa mazingira ya bahari kutokana na kuimarika kwa udhibiti wa uvuvi haramu na usimamizi wa matumizi endelevu ya rasilimali za uvuvi.

(b) Kuongezeka kwa mchango wa Pato la Taifa.

(c) Upatikanaji wa masoko ya uhakika ya kimataifa katika uendelezaji wa rasilimali za uvuvi.

(d) Kuongezeka kwa fursa za uwekezaji katika Sekta ya Uvuvi na hivyo kutoa fursa za ajira, kuimarika kwa ukusanyaji na upatikanaji wa takwimu na taarifa mbalimbali zinazohusu uvuvi katika Bahari Kuu.

(e) Kuwezesha udhibiti wa uvuvi haramu kati ya Nchi Wanachama.

(f) Kuijengea Nchi uwezo wa kulinda rasilimali za uvuvi zilizoko ndani ya mipaka ya bahari katika eneo letu.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa itifaki Mkataba wa Kimataifa wa *FAO* wa kuzuia Uvuvi Haramu kupitia Bandari umegawanyika katika sehemu kuu kumi (10) zenye jumla ya Ibara 37; naomba ziorodheshwe kwenye hansard kama zilivyoandikwa.

Maelezo yafuatayo yatafafanua kwa ufupi vipengele muhimu vilivyochambuliwa na Kamati.

Ibara ya Pili; Ibara hii inaelezea madhumuni ya Mkataba wa *FAO-PSMA* kuwa ni kuzuia, kudhoofisha na kutokomeza uvuvi haramu usiotolewa taarifa na usiodhibitiwa ili kuhakikisha uhifadhi na matumizi endelevu ya rasilimali za baharini na kulinda ikolojia.

Ibara ya Nne; Ibara hii inaelezea uhusiano wa Mkataba wa *FAO-PSMA* na Sheria za Kimataifa pasipo kuathiri sheria za nchi husika. Hivyo Mkataba huu hautazuia nchi kujiamulia mambo yake.

Ibara ya Tano; Inaelezea ushirikiano na uratibu katika ngazi ya Kitaifa katika utekelezaji wa Mkataba wa *FAO-PSMA.*

Ibara ya Sita; Inaelezea ushirikiano katika kubadilishana taarifa zinazohusu usimamizi wa rasilimali za uvuvi baharini kati ya nchi wanachama, *FAO* na mashirika ya Kikanda na Kimataifa.

Ibara ya Saba; Inaeleza wajibu wa nchi wanachama kubainisha bandari zenye sifa stahiki ambazo zitatambulika kwa ajili ya shughuli za ukaguzi katika utekelezaji wa Mkataba wa *FAO-PSMA.*

Ibara ya Nane na Tisa; Zinaelezea utaratibu unaopaswa kuzingatiwa na meli za uvuvi za kigeni kupata kibali cha kuingia bandarini na kukaguliwa. Iwapo itathibitika kuwa meli inayoomba kibali cha kuingia bandarini imehusika na uvuvi haramu haitaruhusiwa kuingia wala kupata huduma yoyote.

Ibara ya Kumi; Inaeleza mazingira ambayo meli inayohusika na uvuvi haramu itaruhusiwa kuingia bandarini na kupata huduma za dharura hususan zile zinazohusu afya/ uhai wa binadamu.

Ibara ya Kumi na Moja; Inaeleza huduma ambazo hazitapaswa kutolewa bandarini kwa kuzingatia sheria na kanuni za nchi husika na sheria za kimataifa kwa meli ambayo taarifa zake za ukaguzi zitathibitishwa kuwa inajihusisha na uvuvi haramu.

Ibara ya Kumi na Mbili, Kumi na Tatu, Kumi na Nne, Kumi na Tano na Kumi na Sita; Ibara hizi zinaeleza taratibu za kuzingatia katika kufanya ukaguzi wa meli kwa mujibu wa Mkataba wa *FAO-PSMA*, taratibu za uandaaji wa ripoti na namna ya kubadilishana taarifa za ukaguzi baina ya nchi wanachama.

Ibara ya 17 na Ishirini na Moja; Zinaeleza kuhusu kujengewa uwezo kwa wakaguzi wa meli, kubadilishana uzoefu baina ya nchi wanachama, kupata misaada ya kitaalam na kuwezesha utekelezaji wa Mkataba wa *FAO-PSMA.*

Ibara ya Ishirini; Inaeleza wajibu wa meli inayopeperusha bendera ya nchi mwanachama kutoa ushirikiano, kufuatilia na kuhakikisha vyombo vyao vinafuata masharti kwa mujibu wa sheria za nchi na za Kimataifa.

Ibara ya Ishirini na Mbili; Inaeleza kuhusu upatikanaji wa suluhu pindi nchi wanachama zinapoingia katika migogoro.

Aidha, Mkataba umeruhusu migogoro inapojitokeza kutatuliwa kwa njia ya majadiliano kabla ya kufikia ngazi za mahakama za Kimataifa.

Ibara ya Thelathini na Tatu; Ibara hii inatoa fursa kwa nchi mwanachama kupendekeza mkataba kufanyiwa marekebisho endapo kuna haja ya kufanya hivyo.

Ibara ya Thelathini na Tano; Inaeleza kuhusu nchi mwanachama kujitoa katika Mkataba wa *FAO-PSMA.* Mktaba huu unatoa fursa kwa nchi mwanachama kujitoa muda wowote baada ya mwaka mmoja tangu tarehe ya kuridhiwa kwa mkataba husika.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako kuwa, hoja zilizoibuliwa na Wabunge zilipata maelezo ya kuridhisha kutoka kwa Serikali na wadau kama ifuatavyo: -

(i) Tanzania haina sababu ya kutoridhia kwa kuwa kipindi cha *Ratification* kimeshapita baada ya idadi ya wanachama wa *FAO* wa kuridhia ilipotimia. Hivyo Tanzania *by Default* haiwezi kukwepa kutekeleza makubaliano hayo kwani kwa kutofanya hivyo kunaiondolea sifa Tanzania na kuonyesha ni nchi inayosaidia kuendelea kuwepo kwa uvuvi haramu na uharamia mwingine baharini.

(ii) Pamoja na kwamba nchi yetu bado haijaridhia makubaliano hayo, hata hivyo imeendelea kutekeleza makubaliano hayo kwa vitendo kwa kufuatilia na kufanya ukaguzi wa meli za nje zinazokuja kwenye bandari zetu ili kuhakikisha kuwa ni meli halali na mizigo iliyobeba ni ile iliyoruhusiwa kimataifa.

(iii) Kwa muda mrefu hatua za kuridhia zilikwama kutokana na ukweli na ugumu wa kutopata maoni ya wadau kutoka pande zote mbili za muungano.

Kwa sasa pande zote mbili za Muungano zimejiridhisha faida zinazoambatana na Mkataba huu na hivyo zimekubaliana nchi yetu iridhie Mkataba wa *FAO-PSMA.*

Mheshimiwa Spika, mbali na ufafanuzi huo uliotolewa, faida zingine zinazoambatana na kuridhiwa kwa Mkataba wa *FAO-PSMA* ni pamoja na:-

(i) Nchi yetu itanufaika kwa kutolipa kwa gharama zozote zinazoambatana na uanachama *(Accession ni costless*);

(ii) Wataalamu wetu watapatiwa mafunzo bure kwenye Idara mbalimbali zinazojihusisha na shughuli za uvuvi na mazao ya uvuvi kama Bandari, Askari wa Majini kupitia Jeshi la Wanamaji, Idara ya Uvuvi, Shirika la Viwango Tanzania, Mamlaka ya kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu;

(iii) Nchi yetu kupitia mwamvuli wa *FAO* itapata misaada mingine mingi inayopitia Umoja wa Mataifa, hususan misaada inayoendana na udhibiti wa uharamia kwenye maji yote yaliyoko eneo la Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Maoni na Ushauri wa Kamati. Baada ya kufanya uchambuzi wa Mkataba wa Kimataifa wa *FAO - PSMA* wa kuzuia uvuvi haramu kupitia bandari za nchi wanachama, Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Serikali kulingana na dhamira njema ya Mkataba huu kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio yatakayopatikana, Kamati ina maoni na ushauri ufuatao:-

Ili nchi iweze kunufaika ipasavyo na Mkataba wa Kimataifa wa *FAO – PSMA* na kuwezesha utekelezaji wa mapendekezo yaliyomo kwenye mkataba ni vyema Serikali:-

(i) Ikaziwezesha ipasavyo Wizara za Uvuvi na Mifugo za Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar kwa kutenga bajeti zinazowezesha Wizara hizi zitekeleze majukumu yake ipasavyo, ikiwa ni pamoja na kuiwezesha kifedha na kuipatia rasilimali watu ya kutosha Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu;

(ii) Kuimarisha Shirika la Uvuvi Tanzania Bara (TAFICO) na Shirika la Uvuvi Zanzibar *(ZAFICO);*

(iii) Kujengwa kwa Bandari za Uvuvi;

(iv) Kuanzishwa kwa viwanda vya kuchakata samaki katika ukanda wa bahari na;

(v) Ununuzi wa meli za kitaifa kubwa zenye uwezo wa kuvua eneo la Ukanda wa Bahari na hivyo kuwezesha uvuvi wa kibiashara.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaamini kuridhiwa kwa Mkataba wa FAO - PSMA pamoja na kuimarisha uwekezaji kwenye Ukanda wa Bahari Kuu kutawezesha nchi yetu kuzifikia, na kuzimiliki rasilimali za uvuvi katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari Kuu kutokana na ushirikiano wa nchi wanachama kudhibiti uvuvi haramu na hivyo kunufaika na rasilimali hizo zilizopo eneo la Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Hitimisho. Napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kumpongeza na kumshukuru Waziri wa Mifugo Mhe. Luhaga J. Mpina, (Mb) na Naibu Waziri Mhe. Abdalla Ulega (Mb), Katibu Mkuu Uvuvi Dkt. Rashid Tamatama pamoja na Wataalamu wote wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa ushirikiano walioipa Kamati wakati ikichambua na kujadili Mkataba wa *FAO - PSMA.*

Mheshimiwa Spika**,** kipekee nawashukuru wadau wote waliotoa michango yao kwa maandishi na kwa kufika mbele ya Kamati. Michango yao ilisaidia kuijengea uwezo Kamati na hivyo kuwawezesha Wajumbe kuwa na uelewa kuhusiana na Mkataba huu.

Mheshimiwa Spika, kwa dhati kabisa napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano na

michango yao waliyoitoa wakati wa kupitia na kuchambua mkataba huu pamoja na kuandaa taarifa hii hadi kukamilika kwake. Naomba majina yao yote yaweze kuingia kwenye hansard.

Mheshimiwa Spika, mwisho napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndg. Stephen Kagaigai, Ndg. Michael Chikokoto Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge kwa kuisaidia na kuiwezesha Kamati hii kutekeleza majukumu yake kwa weledi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee nawashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge wakiongozwa na Sekreterieti ya Kamati ambao ni Ndg. Virgil Mtui na Ndg. Rachel Nyega pamoja na msaidizi wa Kamati Ndg. Mwimbe John kwa kuihudumia Kamati ikiwa ni pamoja na kukamilisha taarifa hii kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naliomba sasa Bunge lako lipokee, lijadili na liridhie Mkataba wa Kimataifa wa *FAO - PSMA* wa kuzuia uvuvi haramu kupitia bandari za nchi wanachama.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha, ahsante sana.

## MAONI YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI KUHUSU AZIMIO LA BUNGE LA KURIDHIA MKATABA WA KIMATAIFA WA FAO WA KUZUIA UVUVI HARAMU KUPITIA BANDARI ZA NCHI WANACHAMA – KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI

### 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 53(6)(b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016. Kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, naomba kuwasilisha Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu Mapendekezo ya Serikali Kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa

Mataifa (FAO) wa Kuzuia Uvuvi Haramu Kupitia Bandari za Nchi Wanachama (*Agreement on Port State Measures to Prevent, Deter and Eliminate Illegal, Unreported and Unregulated Fishing* – PSMA).

**Mheshimiwa Spika,** Nyongeza ya Nane Kifungu cha 7(1) (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, inazipa Kamati za Kisekta ikiwemo Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji jukumu la kushughulikia Miswada ya Sheria, Maazimio na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara inazozisimamia. Aidha, jukumu hili pia ni jukumu la Kikatiba chini ya Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kuipatia Kamati kazi ya kushughulikia mkataba huu kama ilivyo ada, Kamati ilianza kuchambua Mkataba husika kwa kushirikiana na Wadau mbalimbali waliofika mbele ya Kamati na wale waliotuma maoni yao kwa njia ya maandishi ili kuweza kufahamu Chimbuko la Mkataba, Vipengele muhimu vilivyoko kwenye Mkataba na manufaa yatakayopatikana kwa Taifa na kwa nchi Wanachama kuridhia Mkataba husika.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa Tanzania ni miongoni mwa nchi wanachama wa Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa *(Food and Agriculture Organization of the United Nation- FAO*) na kwa kuwa Tanzania ni moja ya nchi zinazopakana na bahari, mwaka 1985 iliridhia Mkataba wa Kimataifa wa Sheria ya Bahari ya Mwaka 1982 (United *Nation Convention on the Law of the Sea – UNCLOS* 1982) ambao unatoa fursa kwa nchi zinazopakana na bahari kutangaza mipaka ya maeneo ya bahari. Fursa hii inatoa haki kwa nchi hizo kutafuta, kutumia, kuhifadhi na kusimamia rasilimali hai na zisizo hai hadi maili za bahari (N*autical Mile*) 200 kutoka ufukweni.

**Mheshimiwa Spika,** mwaka 1989 Bunge lako Tukufu lilitunga Sheria ya Bahari ya Kitaifa ya Ukanda Maalumu wa Uchumi (*Territorial Sea and Exclusive Economic Zone Act of* 1989; ambayo ilitambua kuwepo kwa maeneo matatu ya Bahari

ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Maeneo hayo ni: Bahari ya Ndani (*Inner Sea*), Bahari ya Kitaifa (*Territorial Sea*) na Ukanda Maalum wa Uchumi wa Bahari *(Exclusive Economic Zone* EEZ).

**Mheshimiwa Spika,** eneo Maalum la Uchumi wa Bahari *(Exclusive Economic Zone* EEZ) ambapo hufanyika shughuli za uvuvi wa Bahari Kuu na samaki wa asili wanaopatikana katika eneo hili ni wa aina ya Jodari na jamii zake husifika kwa tabia ya kuhama kwa kasi kubwa tena katika makundi kutoka eneo moja la maji ya bahari hadi eneo lingine.

**Mheshimiwa Spika,** hali hii imepelekea baadhi ya nchi zinazoendelea, kushindwa kunufaika ipasavyo na Uvuvi wa Bahari Kuu kutokana na uwekezaji mkubwa unaohitajika kwenye Uvuvi wa Bahari Kuu. Changamoto nyingine zinazokabili Uvuvi wa Bahari Kuu ni gharama kubwa katika kuendeleza, kusimamia na kudhibiti shughuli za uvuvi ikiwemo Uvuvi Haramu, Usiotolewa Taarifa na Kuratibiwa (*Illegal, Unreported and Unregulated – IUU- fishing*).

**Mheshimiwa Spika,** kwa kutambua changamoto hii na kwa kuzingatia uhitaji wa nchi zinazoendelea katika kukabiliana na Uvuvi Haramu sehemu za Ukanda wa Uchumi na Bahari Kuu, Nchi Wanachama zikiongozwa na Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (*Food and Agriculture Organization of the United Nation – FAO*) ziliafikiana kuchukua hatua madhubuti za pamoja za kukabiliana na uvuvi haramu, usiotolewa taarifa na usiodhibitiwa kwa kutumia bandari.

**Mheshimiwa Spika,** Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (*Food and Agriculture Organization of the United Nation* – FAO) pamoja na mambo mengine linaongoza juhudi za kuongeza usalama wa chakula na lishe duniani. Katika kutekeleza majukumu yake, mwaka 2001 FAO iliandaa Mpango Mahsusi (*International Plan of Action*) wa kuzuia, kudhoofisha na kuondoa uvuvi haramu katika Ukanda wa Uchumi na Bahari Kuu ambao umetokana na ongezeko la matukio ya uvuvi haramu unaosababisha uharibifu wa

ikolojia, upotevu wa rasilimali za uvuvi na kuathiri maisha ya wavuvi na usalama wa chakula na lishe duniani.

**Mheshimiwa Spika,** ili kutekeleza adhima hiyo, Mkataba wa Kimataifa wa Kuzuia Uvuvi Haramu, Usiotolewa Taarifa na Usiodhibitiwa kwa Kutumia Bandari (*The Agreement on Port State Measures to Prevent, Deter and Eliminate Illegal, Unregulated Fishing- PSMA*) uliandaliwa na kukubaliwa. Mwaka 2009 mwezi Oktoba uliridhiwa na nchi Wanachama kwa ajili ya kuzui uvuvi haramu duniani.

## 2.0 MADHUMUNI NA FAIDA ZA MKATABA WA KIMATAIFA WA FAO WA KUZUIA UVUVI HARAMU KUPITIA BANDARI ZA NCHI WANACHAMA

**Mheshimiwa Spika**, lengo kuu la kuzuia uvuvi haramu ni kulinda rasilimali za uvuvi ili kuwa na uvuvi endelevu na kuleta faida kwa taifa husika na kuhakikisha usalama wa chakula na lishe kupitia Mkataba wa FAO - PSMA. Aidha, Mkataba huu ni muhimu kwa ajili ya kulinda rasilimali za uvuvi zilizopo nchini katika maeneo ya maji ya bahari.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Tanzania, Bunge likiridhia Mkataba huu, manufaa yatakayopatikana ni pamoja na: -

(i) Kupungua kwa upotevu wa rasilimali za uvuvi na uharibifu wa mazingira ya bahari kutokana na kuimarika kwa udhibiti wa uvuvi haramu na usimamizi wa matumizi endelevu ya rasilimali za uvuvi.

(ii) Kuongezeka kwa mchango wa Pato la Taifa.

(iii) Upatikanaji wa masoko ya uhakika ya kimataifa katika uendelezaji wa rasilimali za uvuvi.

(iv) Kuongezeka kwa fursa za uwekezaji katika Sekta ya Uvuvi na hivyo kutoa fursa za ajira, kuimarika kwa ukusanyaji na upatikanaji wa takwimu na taarifa mbalimbali zinazohusu uvuvi katika Bahari Kuu.

(v) Kuwezesha udhibiti wa uvuvi haramu kati ya Nchi Wanachama.

(vi) Kuijengea Nchi uwezo wa kulinda rasilimali za uvuvi zilizoko ndani ya mipaka ya bahari katika eneo letu.

## 3.0 UCHAMBUZI WA ITIFAKI

**Mheshimiwa Spika,** Mkataba wa Kimataifa wa FAO wa kuzuia Uvuvi Haramu kupitia Bandari umegawanyika katika sehemu kuu kumi (10) zenye jumla ya Ibara 37. Maelezo yafuatayo yatafafanua kwa ufupi vipengele muhimu vilivyochambuliwa na Kamati.

**Ibara ya Pili**
Ibara hii inaelezea madhumuni ya Mkataba wa FAO - PSMA kuwa ni kuzuia, kudhoofisha na kutokomeza uvuvi haramu usiotolewa taarifa na usiodhibitiwa ili kuhakikisha uhifadhi na matumizi endelevu ya rasilimali za baharini na kulinda ikolojia.

**Ibara ya Nne**
Ibara hii inaelezea uhusiano wa Mkataba wa FAO - PSMA na Sheria za Kimataifa pasipo kuathiri sheria za nchi husika. Hivyo Mkataba huu hautazuia nchi kujiamulia mambo yake.

**Ibara ya Tano**
Inaelezea ushirikiano na uratibu katika ngazi ya Kitaifa katika utekelezaji wa Mkataba wa FAO - PSMA.

**Ibara ya Sita**
Inaelezea ushirikiano katika kubadilishana taarifa zinazohusu usimamizi wa rasilimali za uvuvi baharini kati ya nchi wanachama, FAO na mashirika ya Kikanda na Kimataifa.

**Ibara ya Saba**
Inaeleza wajibu wa nchi wanachama kubainisha bandari zenye sifa stahiki ambazo zitatambulika kwa ajili ya shughuli za ukaguzi katika utekelezaji wa Mkataba wa FAO - PSMA.

**Ibara ya Nane na Tisa**
Zinaelezea utaratibu unaopaswa kuzingatiwa na meli za uvuvi za kigeni kupata kibali cha kuingia bandarini na kukaguliwa. Iwapo itathibitika kuwa meli inayoomba kibali cha kuingia bandarini imehusika na uvuvi haramu haitaruhusiwa kuingia wala kupata huduma yoyote.

**Ibara ya Kumi**
Inaeleza mazingira ambayo meli inayohusika na uvuvi haramu itaruhusiwa kuingia bandarini na kupata huduma za dharura hususan zile zinazohusu afya/ uhai wa binadamu.

**Ibara ya Kumi na Moja**
Inaeleza huduma ambazo hazitapaswa kutolewa bandarini kwa kuzingatia sheria na kanuni za nchi husika na sheria za kimataifa kwa meli ambayo taarifa zake za ukaguzi zitathibitishwa kuwa inajihusisha na uvuvi haramu.

**Ibara ya Kumi na Mbili, Kumi na Tatu, Kumi na Nne, Kumi na Tano na Kumi na Sita**
Ibara hizi zinaeleza taratibu za kuzingatia katika kufanya ukaguzi wa meli kwa mujibu wa Mkataba wa FAO - PSMA, taratibu za uandaaji wa ripoti na namna ya kubadilishana taarifa za ukaguzi baina ya nchi wanachama.

**Ibara ya 17 na Ishirini na Moja**
Zinaeleza kuhusu kujengewa uwezo kwa wakaguzi wa meli, kubadilishana uzoefu baina ya nchi wanachama, kupata misaada ya kitaalam na kuwezesha utekelezaji wa Mkataba wa FAO - PSMA.

**Ibara ya Ishirini**
Inaeleza wajibu wa meli inayopeperusha bendera ya nchi mwanachama kutoa ushirikiano, kufuatilia na kuhakikisha vyombo vyao vinafuata masharti kwa mujibu wa sheria za nchi na za Kimataifa.

**Ibara ya Ishirini na Mbili**
Inaeleza kuhusu upatikanaji wa suluhu pindi nchi wanachama zinapoingia katika migogoro.

Aidha, Mkataba umeruhusu migogoro inapojitokeza kutatuliwa kwa njia ya majadiliano kabla ya kufikia ngazi za mahakama za Kimataifa.

**Ibara ya Thelathini na Tatu**
Ibara hii inatoa fursa kwa nchi mwanachama kupendekeza mkataba kufanyiwa marekebisho endapo kuna haja ya kufanya hivyo.

**Ibara ya Thelathini na Tano**
Inaeleza kuhusu nchi mwanachama kujitoa katika Mkataba wa FAO - PSMA. Mktaba huu unatoa fursa kwa nchi mwanachama kujitoa muda wowote baada ya mwaka mmoja tangu tarehe ya kuridhiwa kwa mkataba husika.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya Kamati kufanya uchambuzi kwenye Ibara hizo za msingi, Kamati ilitaka kujiridhisha kwenye maeneo yafuatayo: -

(i) Idadi ya nchi wanachama wa FAO waliokwisha ridhia Mkataba wa Kimataifa wa Kuzuia Uvuvi Haramu.

(ii) Sababu zilizopelekea nchi yetu kuchelewa kuridhia Mkataba huu.

(iii) Kwa nchi yetu kutoridhia Mkataba huu, Je hakuna namna yoyote nchi yetu inatekeleza makubaliano yaliomo kwenye Mkataba huu? Ikiwa ni pamoja na kuzifuatilia na kuzikagua meli za kigeni zinazokuja kwenye bandari zetu? Kama ndio kuna madhara gani?

**Mheshimiwa Spika,** napenda kuliarifu Bunge lako kuwa, hoja zilizoibuliwa na Wabunge zilipata maelezo ya kuridhisha kutoka kwa Serikali na Wadau kama ifuatavyo: -

(i) Tanzania haina sababu ya kutoridhia kwa kuwa kipindi cha *Ratification* kimeshapita baada ya idadi ya Wanachama wa FAO wa kuridhia ilipotimia. Hivyo Tanzania *by Default* haiwezi kukwepa kutekeleza Makubaliano hayo kwani kwa kutofanya hivyo kunaiondolea sifa Tanzania na kuonyesha ni nchi

inayosaidia kuendelea kuwepo kwa uvuvi haramu na uharamia mwingine baharini.

(ii) Pamoja na kwamba nchi yetu bado haijaridhia makubaliano hayo, hata hivyo imeendelea kutekeleza makubaliano hayo kwa vitendo kwa kufuatilia na kufanya ukaguzi wa meli za nje zinazokuja kwenye bandari zetu ili kuhakikisha kuwa ni meli halali na mizigo iliyobeba ni ile iliyoruhusiwa kimataifa.

(iii) Kwa muda mrefu hatua za kuridhia zilikwama kutokana na ukweli na ugumu wa kupata maoni ya wadau kutoka pande zote mbili za muungano.

Kwa sasa pande zote mbili za Muungano zimejiridhisha faida zinazoambatana na Mkataba huu na hivyo zimekubaliana nchi yetu iridhie Mkataba wa FAO - PSMA.

**Mheshimiwa Spika**, mbali na ufafanuzi huo uliotolewa, faida zingine zinazoambatana na kuridhiwa kwa Mkataba wa FAO-PSMA ni pamoja na:-

- Nchi yetu itanufaika kwa kutolipa kwa gharama zozote zinazoambatana na uanachama ~ (*Accession ni costless*);

- Wataalamu wetu watapatiwa mafunzo bure kwenye Idara mbalimbali zinazojihusisha na shughuli za uvuvi na mazao ya uvuvi kama Bandari, Askari wa Majini kupitia Jeshi la Wanamaji, Idara ya Uvuvi, Shirika la Viwango Tanzania, Mamlaka ya kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu;

- Nchi yetu kupitia mwamvuli wa FAO itapata misaada mingine mingi inayopitia Umoja wa Mataifa hususan misaada inayoendana na udhibiti wa uharamia kwenye maji yote yaliyoko eneo la Tanzania.

## 4.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kufanya uchambuzi wa Mkataba wa Kimataifa wa FAO - PSMA wa kuzuia uvuvi haramu kupitia bandari za nchi Wanachama, Kamati

inakubaliana na mapendekezo ya Serikali kulingana na dhamira njema ya Mkataba huu kwa Taifa.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio yatakayopatikana, Kamati ina maoni na ushauri ufuatao: -
Ili nchi iweze kunufaika ipasavyo na Mkataba wa Kimataifa wa FAO – PSMA na kuwezesha utekelezaji wa mapendekezo yaliyomo kwenye mkataba ni vyema Serikali: -

- Ikaziwezesha ipasavyo Wizara za Uvuvi na Mifugo za Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar kwa kutenga bajeti zinazowezesha Wizara hizi zitekeleze majukumu yake ipasavyo, ikiwa ni pamoja na kuiwezesha kifedha na kuipatia rasilimali watu ya kutosha Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu;

- Kuimarisha Shirika la Uvuvi Tanzania Bara (TAFICO) na Shirika la Uvuvi Zanzibar (ZAFICO);
- Kujengwa kwa Bandari za Uvuvi;

- Kuanzishwa kwa viwanda vya kuchakata samaki katika ukanda wa bahari na

- Ununuzi wa meli za kitaifa kubwa zenye uwezo wa kuvua eneo la Ukanda wa Bahari na hivyo kuwezesha uvuvi wa kibiashara.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaamini kuridhiwa kwa Mkataba wa FAO - PSMA pamoja na kuimarisha uwekezaji kwenye Ukanda wa Bahari Kuu kutawezesha nchi yetu kuzifikia, na kuzimiliki rasilimali za uvuvi katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari Kuu kutokana na ushirikiano wa nchi wanachama kudhibiti uvuvi haramu na hivyo kunufaika na rasilimali hizo zilizopo eneo la Tanzania.

**Mheshimiwa Spika,** vile vile Pato la Taifa litaongezeka kutokana na upatikanaji wa fedha za kigeni na hivyo kukuza uchumi wa Taifa, kuhakikisha upatikanaji wa uhakika wa malighafi kwa ajili ya viwanda vya samaki, kuongezeka kwa fursa za uwekezaji katika sekta ya uvuvi na hivyo kutoa fursa za ajira na kuongeza upatikanaji wa chakula na lishe na hatimae kuijengea nchi uwezo wa kulinda rasilimali za uvuvi.

## 5.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji.

**Mheshimiwa Spika**, napenda pia kumpongeza na kumshukuru Waziri wa Mifugo Mhe. Luhaga J. Mpina, (Mb) na Naibu Waziri Mhe. Abdalla Ulega (Mb), Katibu Mkuu Uvuvi Dkt. Rashid Tamatama pamoja na Wataalamu wote wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa ushirikiano walioipa Kamati wakati ikichambua na kujadili Mkataba wa FAO - PSMA.

**Mheshimiwa Spika,** kipekee nawashukuru wadau wote waliotoa michango yao kwa maandishi na kwa kufika mbele ya Kamati. Michango yao ilisaidia kuijengea uwezo Kamati na hivyo kuwawezesha Wajumbe kuwa na uelewa kuhusiana na Mkataba huu.

**Mheshimiwa Spika**, kwa dhati kabisa napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano na michango yao waliyoitoa wakati wa kupitia na kuchambua Mkataba huu pamoja na kuandaa taarifa hii hadi kukamilika kwake. Naomba kuwatambua kwa kuwataja majina kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Mahmoud Hassan Mgimwa, Mb - Mwenyekiti
2. Mhe. Dkt. Christine G. Ishengoma, Mb - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Dkt. Mary Michael Nagu, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Prof. Sospeter M. Muhongo, Mb - Mjumbe
5. Mhe. Eng. Edwin A. Ngonyani, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Katani Ahmad Katani Mb - Mjumbe
7. Mhe. Khadija Hassan Aboud, Mb - Mjumbe
8. Mhe. Haroon Mulla Pirmohamed, Mb - Mjumbe
9. Mhe. Ritta Enespher Kabati, Mb - Mjumbe
10. Mhe. Mattar Ali Salum, Mb - Mjumbe
11. Mhe. Lucy Simon Magereli, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Justine Joseph Monko, Mb - Mjumbe
13. Mhe. Omar Abdallah Kigoda, Mb - Mjumbe
14. Mhe. Anna Richard Lupembe, Mb - Mjumbe

15. Mhe. Pascal Yohana Haonga - Mjumbe
16. Mhe. Salim Mbaraku Bawazir Mb - Mjumbe
17. Mhe. Deo Kasenyenda Sanga, Mb - Mjumbe
18. Mhe. Devotha Methew Minja, Mb - Mjumbe
19. Mhe. Haji Ameir Haji, Mb - Mjumbe
20. Mhe. Haji Khatib Kai, Mb - Mjumbe
21. Mhe. Sikudhani Yasini Chikambo, Mb - Mjumbe
22. Mhe. Juma Ali Juma, Mb - Mjumbe
23. Mhe. Emmanuel Papian John, Mb - Mjumbe
24. Mhe. Kunti Yusuph Majala, Mb - Mjumbe
25. Mhe. Anthony Calist Komu, Mb - Mjumbe
26. Mhe. Jitu V. Soni, Mb - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika,** mwisho napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndg. Stephen Kagaigai, Ndg. Michael Chikokoto Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge kwa kuisaidia na kuiwezesha Kamati hii kutekeleza majukumu yake kwa weledi mkubwa.

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya kipekee nawashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge wakiongozwa na Sekreterieti ya Kamati ambao ni Ndg. Virgil Mtui na Ndg. Rachel Nyega pamoja na msaidizi wa Kamati Ndg. Mwimbe John kwa kuihudumia Kamati ikiwa ni pamoja na kukamilisha taarifa hii kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo, naliomba sasa Bunge lako lipokee, lijadili na liridhie Mkataba wa Kimataifa wa FAO-PSMA wa kuzuia uvuvi haramu kupitia bandari za nchi wanachama.

**Mheshimiwa Spika**, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

Mahmoud Hassan Mgimwa, (Mb)
**MWENYEKITI,**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO,**
**MIFUGO NA MAJI**

14 NOVEMBA, 2019

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt Ishengoma kwa kupitia taarifa ya Kamati vizuri sana na kuweza kutusomea hapa mbele sasa nimuite Msemaji Rasmi wa Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Mifugo na Uvuvi Mheshimiwa Dkt Sware Semesi karibu tafadhali

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika**,** nashukuru kwa nafasi. Naomba kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu azimio la kuridhia mkataba wa Kimataifa wa *FAO* wa kuzuia uvuvi haramu kupitia bandari za nchi wanachama *(Agreement on Port State Measures Prevent, Deter and Eliminate Illegal, Unreported and Unregulated Fishing – PSMA).*

Mheshimiwa Spika, kwasababu ya muda naomba nianzie Aya ya 5, lakini vyote naomba viingie kwenye *hansard*. Mkataba huu unatoa suluhisho kwa nchi wahusika kukomesha na kutokomeza uvuvi haramu, usiotolewa taarifa na usiodhibitiwa ili kuhakikisha uhifadhi na matumizi endelevu ya rasilimali za baharini.

Mheshimiwa Spika, mkataba huu una maana pana inayohusisha na kuangalia maeneo yafuatayo:-

(i) Meli na shughuli za uvuvi zinazokinzana na sheria ya kitaifa, kikanda na kimataifa,

(ii) Meli zisizotoa au kutoa taarifa pungufu na zisizosahihi,

(iii) Meli zisizo na usajili wa taifa zinazotokea *(status versols),*

(iv) Uvuvi wa meli za nchi zisizowanachama katika maeneo yaliyondani ya mikataba ya usimamizi wa uvuvi ya taasisi za kikanda, na

(v) Shughuli za uvuvi usioratibiwa kisheria na nchi husika ambao ni vigumu kuufuatilia na kuudhibiti.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatambua kuhusika kikamilifu kwa nchi yetu kupitia wataalamu wetu wa pande zote mbili za Muungano kama wanachama wa *FAO* katika maandalizi ya makubaliano ya Kitaifa ya udhibiti uvuvi haramu na biashara haramu ya samaki na mazao yake kupitia bandari na za nchi wanachama *(PSMA).*

Mheshimiwa Spika, Pia naomba kuwatambua Shirika la *WWF* wamekuwa wakiweka kipaumbele katika masuala haya.

Mheshimiwa Spika, sasa naenda kugusia umuhimu wa kuridhia *PSMA*. Pamoja na kuwepo Ukanda wa uchumi wa Bahari Kuu *(EEZ)* ambamo nchi wanachama wanalazimika kulinda kwa gharama zote rasilimali zilizomo na kuzitumia kiuendelevu bado kuna eneo la Bahari Kuu *(High Seas*) ambao ni kubwa zaidi ya ukanda wa uchumi wa bahari kuu *(EEZ)* za nchi zote na ambalo nchi zote ikiwemo Tanzania inaruhusiwa kutumia rasilimali zake zilizo hai na zisizo hai. Hata hivyo, bado imekuwa vigumu nchi zote wanachama wa *FAO* na zile ambazo si wanachama kuweza kuungana kwa pamoja kuzilinda na kuhakikisha uendelevu wake hususan rasilimali zilizo hai ambazo ni *renewable* lakini zisizo vuliwa kiuendelevu zitapotea na mazingira yake kuharibika.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hii imekuwa ni changamoto kubwa kusimamia rasilimali zetu katika ukanda huu wa bahari. Ndiyo maana kama nchi mwanachama wa *FAO* njia rahisi ya kuweza kupigana vita dhidi ya uvuvi haramu maharamia na wafanyabiashara haramu ni kupitia bandari za nchi husika. Hii ni njia rahisi sana kwani pamoja na ukweli kuwa meli zinaweza kukaa baharini zikivua kwa muda mrefu, hata miaka miwili, bado zitalazimika kurudi kwenye moja ya bandari kwa ajili ya ukarabati mkubwa na hata mdogo na hivyo kuwa rahisi kudhibitiwa.

Mheshimiwa Spika, njia nyingine rahisi na ya muhimu ni kukagua na kufuatilia mizigo ya mazao ya uvuvi yanayotolewa bandarini na meli za uvuvi, ili kubaini meli

zilizohusika na mzigo unaotolewa bandarini. Njia hii imekuwa ni bora zaidi na imesaidia sana kupunguza uvuvi haramu na pia uharamia kwani *PSMA*, inazo *protocol* zinazoelekeza nchi wanachama kuchukua hatua kabla meli haijaruhusiwa kuingia bandarini; na pia zipo orodha hakiki za ukaguzi wa meli husika .

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa Tanzania bado haijaridhia makubaliano ya *PSMA*, bado imeendelea kuyatekeleza kwa vitendo makubaliano hayo kwa kufuatilia na kuzikagua meli za ndani na za kigeni zinazokuja kwenye bandari zetu ili kujihakikishia kuwa ni meli halali na mizigo yake ni ile inayoruhusiwa Kimataifa. Meli hizo huja bandarini kwetu kwasababu mbalimbali; kwa mfano kushusha mabaharia wagonjwa au waliomaliza mikataba yao, meli mbovu ama kuja kwa ukaguzi wa awali kabla ya kupatiwa leseni Utekelezaji na makubaliano hayo ya *PSMA* kwa vitendo ni moja ya sababu ya msingi ya kuridhia makubaliano hayo.

Mheshimiwa Spika, kimsingi Tanzania haina sababu ya kutoridhia makubaliano haya kwani kipindi cha uridhiwaji kilishapita baada ya idadi ya wanachama wa *FAO* kuridhia ilipotimia. Hivyo Tanzania haiwezi kukwepa utekelezaji wa makubaliano hayo kwani kutofanya hivyo kunaiondolea sifa na kuonesha ni nchi inayosimamia uvuvi haramu na uharamia mwingine baharini

Mheshimiwa Spika, Tanzania ikiwa mwanachama wa *Indian Oncean Tuna Commission (IOTC),* wanachama wake waliamua kukubali *FAO-PSMA* kama IOTC *binding resolution* na hivyo na Tanzania italazimika kuutekeleza mkataba huu wa *PSMA* kwa upande wa uvuvi wa samaki aina ya Jodari (*tuna*) na aina zinazofanana au kuhusiana na Jodari kwa upande wa Bahari ya Hindi.

Mheshimiwa Spika, ni muhimu kwa Tanzania kuridhia makubaliano haya kwa kuwa haitawajibika kwa malipo, gharama au mchango wowote kwa *FAO* au popote katika utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, Tanzania kwa pande zote mbili za Muungano imekuwa ikikosa misaada mbalimbali kwa mfano fursa za mafunzo yanayofadhiliwa na *FAO* na pia *UN* kwa wataalam wake wa idara na taasisi mfano bandari, *navy,* polisi, idara za uvuvi, mamlaka za udhibiti wa viwango vya chakula, dawa na vifaa tiba, mamlaka ya kusimamia uvuvi wa bahari kuu na mamlaka za usajili wa meli ili kuwawezesha kupata mafunzo mbalimbali ya kufanya udhibiti halisi kwenye bandari zetu kama timu moja. *FAO* inatoa fursa za mafunzo nchi zilizoridhia makubaliano hayo tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuridhia azimio hili nchi chini ya mwamvuli wa *FAO* Tanzania itapata misaada mingine mingi inayopitia Umoja wa Mataifa katika kudhibiti uharamia kwenye maji yetu yote na sio bahari peke yake. Tanzania kwa miaka yote imekosa misaada ya fedha, mali na utaalam kutokana na kutoridhia mkataba huu. Pia tumeshindwa kushirikishwa kikamilifu katika mipango ya hali ya juu na ya kiteknolojia za hali ya juu katika udhibiti wa uvuvi haramu na mapambano ya uharamia baharini. Tukiridhia maana yake Tanzania itanufaika na yale yanayopangwa kwenye nyanja mbalimbali kimataifa chini ya mwamvuli wa Umoja wa Mataifa na *FAO. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi nyingine zote za ukanda wa magharibi wa Bahari ya Hindi na nchi za *South West Indian Ocean Commission* zimeridhia isipokuwa Tanzania na Comoro tu.  Hali hii haipendezi kwa nchi yetu ambayo ni kubwa na yenye sifa kubwa ukilinga na Comoro. Aidha, inaonesha kwa kiwango fulani udhaifu wa kutokwenda pamoja na wenzetu katika masuala nyeti na hususan vita vya kimataifa dhidi ya mambo mabaya kama uvuvi na biashara haramu, uharamia, usafirishaji haramu wa silaha, madawa ya kulevya, binadamu na maliasili mbalimbali kupitia meli.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia kuwa Tanzania ni Mwenyekiti wa *SADC* ambayo ina *protocol* maalum ya kuongoza sekta ya uvuvi kwa pamoja na kutambua kuwa nchi zote za *SADC* zenye bahari zimeridhia makubaliano

haya, ni vema tusirudi nyuma na kuacha maswali mengi sana kwa nchi wenzetu wa *SADC* bila sababu yoyote ile.

Mheshimiwa Spika, mapitio ya baadhi ya ibara katika mkataba. Mkataba wa *PSMA* una sehemu 10 na ibara 37 na viambatanisho vitano. Ibara ya 6 inaelekeza ushirikiano katika kubadilishana taarifa zinazohusu usimamizi wa rasilimali za uvuvi bandarini kati ya Nchi Wanachama na *FAO* na mashirika ya kikanda na kimataifa. Kambi inaishauri Serikali kuizingatia hii na kuwezesha Wizara husika kutekeleza jukumu hili.

Mheshimiwa Spika, licha ya kuwa Kambi Rasmi ya Upinzani kwa mara kadhaa imekuwa ikisistiza kwa Bunge lako umuhimu wa kuwa na bandari ya uvuvi katika mwambao wa nchi yetu, lakini mapendekezo na mipango hiyo imebakia kwenye makabrasha ya Serikali. Bado kambi inasisitiza umuhimu wa kuwekeza katika sekta ya uvuvi wa bahari kuu kwa kuwa na bandari ya uvuvi kwani Serikali imekuwa ikikosa mapato yake halali inayostahili kutoka uvuvi wa bahari kuu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mkataba wa *PSMA* unahusika na meli zote za kigeni za uvuvi zinazotaka kuingia katika bandari zilizochaguliwa na nchi husika na kwa kuzingatia Ibara ya 7 ya mkataba ambayo inahusu wajibu wa Nchi Wanachama kubainisha bandari zenye sifa stahiki ambazo zitatambuliwa kwa ajili ya shughuli za ukaguzi katika utekelezaji wa mkataba wa *PSMA*, ni muhimu sasa Mheshimiwa Waziri akawaeleza Watanzania ni bandari zipi ambazo kwa sasa zimekwishatambuliwa katika kuhakikisha zinatekeleza jukumu hilo.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Taifa wa Pili wa Maendeleo ya Miaka Mitano ukurasa wa 251 unaelezea kuhusu kujengwa kwa bandari ya uvuvi katika Mikoa ya Tanga, Dar es Salaam au Mtwara na bahati nzuri bajeti ya ujenzi kuanzia mwaka wa fedha 2016 – 2021 imeanishwa. Hoja ya msingi ambayo pia Waziri anatakiwa kuliezea Bunge ni kiasi gani sasa kimeshatolewa kati ya shilingi trilioni 2.5

zilizopangwa kwenye Mpango kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa bandari ya uvuvi.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 8 inaongelea utaratibu unaopaswa kuzingatiwa na meli za uvuvi za kigeni kupata kibali cha kuingia bandarini na kukaguliwa. Sharti hili linaweza kuwa jepesi na gumu kwa kuwa nchi zetu nyingi hasa za ukanda wa pwani wa Afrika Mashariki na Kusini hazina vyombo vya kufanya doria hivyo si rahisi kufahamu meli husika na mizigo iliyonayo imeipata kutoka ukanda wa nchi gani. Hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inasisitiza kuwa Serikali kuimarisha doria katika maeneo ambayo tunayamiliki ili tuweze kuwa na uhakika kwamba rasilimali zinazotoka zina manufaa kwa watu wetu na nchi yetu kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, naomba niende kwenye maoni aya ya 25. Ufanisi wa utekelezaji wa *PSMA* utapelekea mchango wa muda mrefu wa uhifadhi wa matumizi endelevu wa viumbe hai na rasilimali za bahari na mifumo ya kiikolojia. Tunaporidhia mkataba huu nchini kwetu basi hatuna budi kutekeleza majukumu yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, moja; kuandaa sheria, kanuni na taratibu zake za utawala kitaifa; Mbili, kushiriki katika mijadala ya kuandaa makubaliano, maazimio na miongozo yanayosimamiwa na Umoja wa Mataifa; Tatu, nchi zinahitaji kufuata taratibu za kusaini na kuridhia mwongozo au mkataba husika ili kuwezesha kujumuisha mwongozo huo katika sheria za kitaifa; Nne, kuanzisha utaratibu wa masharti ya bandari ambapo meli za uvuvi zitalazimika kufuata utaratibu uliowekwa ili ziweze kutumia bandari husika; Tano; chini ya Mkataba wa *PSMA* Nchi Wanachama zitalazimika kutekeleza hatua na miongozo yote kama ilivyoainishwa katika mkataba huo; na Sita, kwenye rasimu ya waraka tunashauri suala hili lipanuliwe zaidi isiwe kwa ajili ya ukanda wa uchumi wa bahari kuu *(EEZ)* yetu pekee, bali udhibiti uwe pia hadi kwenye bahari kuu *(high seas)* ambapo Watanzania wanapaswa kuwezeshwa ili wakavue *EEZ* na zaidi ya hapo. Hivyo, pale ambapo kumeorodheshwa maeneo ya bahari *yaani inner sea, territorial sea* na ukanda wa uchumi wa

bahari yaani *EEZ,* tuongezee na bahari kuu kwani na Watanzania pia wanaruhusiwa kuvua kwenye ukanda wa uchumi wa bahari kuu za nchi nyingine na pia bahari kuu katika maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, naomba nihitimishe; Kambi Rasmi ya Upinzani haioni sababu yeyote ya kupinga uridhiwaji wa mkataba huu kulingana na maudhui ya mkataba huu. Aidha, ili faida zinazoongelewa katika mkataba huu zikainufaishe nchi yetu, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inasisitiza kuzingatia ushauri ufuatao:-

Mheshimiwa Spika, moja; kuhakikisha bandari ya uvuvi inajengwa kwa haraka kama ilivyoelezwa kwenye Mpango wa Maendeleo wa Awamu ya Pili; Mbili, kuweka utaratibu mzuri wa kupata wakaguzi kulingana na matakwa ya mkataba; Tatu; kuwekeza katika vyombo vya kufanya doria kwenye ukanda wa uchumi na bahari kuu; na Nne na mwisho kuimarisha masoko yetu ya ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MAONI YA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KUHUSU AZIMIO LA KURIDHIA MKATABA WA KIMATAIFA WA FAO WA KUZUIA UVUVI HARAMU KUPITIA BANDARI ZA NCHI WANACHAMA (*AGREEMENT ON PORT STATE MEASURES TO PREVENT, DETER AND ELIMINATE ILLEGAL, UNREPORTED AND UNREGULATED FISHING*-PSMA) KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI**

*"Yanatolewa kwa Mujibu wa Kanuni ya 53(6)(c) ya Kanuni ya Bunge, Toleo la Mwaka 2016)"*

## I. UTANGULIZI

**1. Mheshimiwa Spika,** Tanzania ni mwanachama wa Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO) tangu mwaka 1962 na mwaka 2001 FAO kutokana na ongezeko la uvuvi haramu iliandaa mpango mahsusi wa kuzuia,

kudhoofisha na kuondoa uvuvi haramu usiotolewa taarifa na kudhibitiwa *(Illegal, Unreported and Unregulated)* ambao hufanyika kwa kiasi kikubwa katika ukanda wa uchumi wa bahari kuu *(Exclusive Economic Zone - EEZ)* za nchi za pwani. Hali hii hutishia uhakika wa upatikanaji wa chakula kutoka mazao ya baharini kwa watu trakribani milioni 45 kwa Bara la Afrika, na kupelekea pia kupata hasara ya takribani dola za kimarekani bilioni 1.5 katika Bara letu kwa mwaka.

**2.** **Mheshimiwa Spika,** mkataba huu ni matokeo ya uvuvi haramu uliokithiri katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari Kuu (EEZ) na baadae meli hizo haramu za uvuvi kupata huduma wanazohitaji kwenye bandari zingine tofauti na walipokuwa wanafanya uvuvi haramu. Jambo hili limeota mizizi hasa kwa mataifa ya dunia ya tatu ambayo hayana uwezo wa kufanya doria katika eneo lake la Ukanda wa Bahari Kuu kwa ujumla wake.

**3.** **Mheshimiwa Spika,** kama azimio hili linavyosema, mchakato mzima wa uvuvi haramu unasababisha uharibifu mkubwa wa ikolojia, upotevu wa rasilimali za uvuvi na hivyo kuathiri maisha ya wavuvi wadogo ambao ikolojia ya bahari ni muhimu katika kazi zao za kila siku, sambamba na kuhatarisha usalama wa chakula na lishe kwa nchi husika na duniani kwa ujumla.

**4.** **Mheshimiwa Spika,** lengo mahususi pia la mkataba huu ni kuongeza mtandao wa ushirikiano baina ya mataifa ya kikanda na kimataifa katika kutokomeza uvuvi haramu. Katika kufikia utekelezaji huo, bandari za nchi mwanachama ndizo zitakuwa na jukumu la ziada katika kupambana na uharamia huo.

**5.** **Mheshimiwa Spika**, mkataba huu unatoa suluhisho kwa nchi wahusika kukomesha na kutokomeza uvuvi haramu usiotolewa taarifa na usiodhibitiwa ili kuhakikisha uhifadhi na matumizi endelevu ya rasilimali za baharini.

**6.** **Mheshimiwa Spika,** mkataba huu una maana pana inayohusisha na kuangalia maeneo yafuatayo:-

i. Meli na shughuli za uvuvi zinazokinzana na sheria za kitaifa, kikanda na kimataifa;

ii. Meli zisizotoa au kutoa taarifa pungufu na zisizo sahihi;

iii. Meli zisizo na usajili wa Taifa zinakotokea (*status vessel*);

iv. Uvuvi wa meli za nchi zisizo wanachama katika maeneo yaliyo ndani ya mikataba ya usimamizi wa uvuvi ya taasisi za kikanda; na

v. Shughuli za uvuvi usioratibiwa kisheria na nchi husika ambao ni vigumu kufuuatilia na kuudhibiti.

**7.** **Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatambua kuhusika kikamilifu kwa nchi yetu kupitia wataalamu wetu wa pande zote mbili za Muungano kama mwanachama wa FAO katika maandalizi ya makubaliano ya kitaifa ya kudhibiti uvuvi haramu na biashara haramu ya samaki na mazao yake kupitia bandari za nchi wanachama (PSMA)

## II. UMUHIMU WA KURIDHIA PSMA

**8.** **Mheshimiwa Spika**, pamoja na kuwepo Ukanda wa Uchumi wa Bahari Kuu (EEZ) ambamo nchi wanachama wanalazimika kulinda kwa gharama zote rasilimali zilizomo na kuzitumia kiuendelevu bado kuna eneo la BAHARI KUU (*high seas*)ambalo ni kubwa zaidi ya Ukanda wa Uchumi wa Bahari Kuu (EEZ) za nchi zote na ambalo nchi zote ikiwemo Tanzania inaruhusiwa kutumia rasilimali zake zilizo hai na zisizo hai. Hata hivyo, bado imekuwa vigumu nchi zote wanachama wa FAO na zile ambazo si wanachama kuweza kuungana kwa pamoja kuzilinda na kuhakikisha uendelevu wake hususani rasilimali zilizo hai ambazo ni '*renewable'* lakini zisipovuliwa kiuendelevu zitapotea na mazingira yake kuharibika.

**9.** **Mheshimiwa Spika**, kutokana na hali hii, imekuwa ni changamoto kubwa kusimamia rasilimiali zetu katika ukanda

huu wa bahari, na ndiyo maana kama nchi mwanachama wa FAO njia rahisi ya kuweza kupigana vita dhidi ya uvuvi haramu, maharamia na wafanyabiashara haramu ni kupitia Bandari za nchi husika. Hii ni njia rahisi sana kwani pamoja na ukweli kuwa meli zinaweza kukaa baharini zikivua kwa muda mrefu hata miaka miwili (2) bado zitalazimika kurudi kwenye moja ya bandari kwa ajili ya ukarabati mkubwa na hata mdogo na hivyo kuwa rahisi kudhibitiwa.

**10. Mheshimiwa Spika,** njia nyingine rahisi na ya muhimu ni kukagua na kufuatilia mizigo ya mazao ya uvuvi yanayoletwa bandarini na meli za uvuvi (*at Sea Trans-shipment*) ili kubaini meli zilizohusika na uvuvi na mzigo unaoletwa bandarini. Njia hii imekuwa ni bora zaidi na imesaidia sana kupunguza uvuvi haramu na pia uharamia kwani PSMA inazo protokali zinazoelekeza nchi wanachama kuchukua hatua kabla meli haijaruhusiwa kuingia bandarini na pia zipo orodha hakiki *(checklists)* za ukaguzi wa meli husika.

**11. Mheshimiwa Spika,** pamoja na kuwa Tanzania bado haijaridhia makubaliano ya PSMA, bado imeendelea kuyatekeleza kwa vitendo makubaliano hayo kwa kuzifuatilia na kuzikagua meli za ndani na za kigeni zinazokuja kwenye bandari zetu ili kujihakikishia kuwa ni meli halali na mizigo yake ni ile inayoruhusiwa kimataifa. Meli hizo huja bandarini kwetu kwa sababu mbalimbali mfano; kushusha mabaharia wagonjwa au waliomaliza mikataba yao, meli mbovu (*force majoure*) ama kuja kwa ukaguzi wa awali kabla ya kupatiwa leseni (*Pre License Inspections*). Utekelezaji wa makubaliano hayo ya PSMA kwa vitendo ni moja ya sababu ya msingi ya kuridhia makubaliano haya.

**12. Mheshimiwa Spika,** kimsingi, Tanzania haina sababu ya kutoridhia makubaliano haya kwani kipindi cha uridhiwaji kilishapita baada ya idadi ya wanachama wa FAO wa kuridhia (*ratification*) ilipotimia. Hivyo, Tanzania haiwezi kukwepa kutekeleza makubaliano hayo kwani kutofanya hivyo kunaiondolea sifa na kuonesha ni nchi inayosimamia uvuvi haramu na uharamia mwingine baharini.

**13. Mheshimiwa Spika,** Tanzania ikiwa mwanachama wa *the Indian Ocean Tuna Commission* (IOTC), wanachama wake waliamua kukubali FAO PSMA kama '*IOTC binding resolution'* na hivyo Tanzania italazimika *kuutekeleza mkataba huu wa PSMA* kwa upande wa uvuvi wa samaki aina ya jodari (*tuna*)na aina zinazofanana au kuhusiana na jodari kwa upande wa bahari ya Hindi.

**14. Mheshimiwa Spika,** ni muhimu kwa Tanzania kuridhia makubaliano haya kwa kuwa haitawajibika kwa malipo yoyote au gharama yoyote au mchango wowote kwa FAO au popote katika utekelezaji wake.

**15. Mheshimiwa Spika,** Tanzania (kwa pande zote mbili za Muungano) imekuwa ikikosa misaada mbalimbali kwa mfano fursa za mafunzo yanayofadhiliwa na FAO na pia UN kwa wataalam wake wa Idara na Taasisi mbalimbali mfano: Bandari, ***Navy***, Polisi, Idara za Uvuvi, Mamlaka za Udhibiti wa Viwango vya Chakula, Dawa na Vifaa Tiba, Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu na Mamlaka za Usajili wa Meli ili kuwawezesha kupata mafunzo mbalimbali ya kufanya udhibiti halisi kwenye bandari zetu kama timu moja. FAO inatoa fursa za mafunzo nchi zilizoridhia makubaliano haya tu.

**16. Mheshimiwa Spika,** kwa kuridhia azimio hili, chini ya mwamvuli wa FAO Tanzania itapata misaada mingine mingi inayopitia Umoja wa Mataifa (UN) katika kudhibiti uharamia kwenye maji yetu yote na siyo Bahari pekee. Tanzania kwa miaka yote imekosa misaada ya fedha, mali na utaalam kutokana na kutoridhia mkataba huu. Pia tumeshindwa kushirikishwa kikamilifu katika mipango ya hali ya juu na ya kiteknolojia za hali ya juu katika udhibiti wa uvuvi haramu na mapambano ya uharamia Baharini. Tukiridhia maana yake Tanzania itanufaika na yale yanayopangwa kwenye nyanja mbalimbali kimataifa chini ya mwamvuli wa Umoja wa Mataifa (UN) na FAO.

**17. Mheshimiwa Spika**, nchi nyingine zote za ukanda wa Magharibi wa Bahari ya Hindi na chini za ***South West Indian***

***Ocean Commission*** zimeridhia isipokuwa Tanzania na Komoro tu. Hii ni haipendezi kwa nchi yetu ambayo ni kubwa na yenye sifa kubwa kulinganisha na Komoro. Aidha, inaonesha kwa kiwango fulani udhaifu wa kutokwenda pamoja na wenzetu katika masuala nyeti na hususani vita za kimataifa dhidi ya mambo mabaya kama uvuvi na biashara haramu, uharamia, usafirishaji haramu wa silaha, madawa ya kulevya, binadamu na maliasili mbalimbali kupitia meli.

**18.** **Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia kuwa Tanzania ni Mwenyekiti wa SADC ambayo ina protokali maalum ya kuongoza sekta ya uvuvi kwa pamoja; na kwa kutambua kuwa nchi zote za SADC zenye Bahari zimeridhia makubaliano haya; ni vyema tusirudi nyuma na kuacha maswali mengi sana kwa nchi wenzetu za SADC bila sababu yoyote ile.

## III. MAPITIO YA BAADHI YA IBARA KATIKA MKATABA

**19.** **Mheshimiwa Spika**, Mkataba wa PSMA una sehemu 10 na Ibara 37 na viambatisho 5. **Ibara ya 6** inaelezea ushirikiano katika kubadilishana taarifa zinazohusu usimamizi wa rasilimali za uvuvi bandarini kati ya nchi wanachama wa FAO na mashirika ya kikanda na kimataifa.

**20.** **Mheshimiwa Spika**, licha ya kuwa Kambi Rasmi ya Upinzani kwa mara kadhaa imekuwa ikisisitiza kwa Bunge lako umuhimu wa kuwa na bandari ya uvuvi katika mwambao wa nchi yetu, lakini mapendekezo na mipango hiyo imebakia kwenye makabrasha ya Serikali. Bado Kambi inasisitizia umuhimu wa kuwekeza katika sekta ya uvuvi wa bahari kuu kwa kuwa na bandari ya uvuvi kwani Serikali imekuwa ikikosa mapato yake halali inayostahili kutoka uvuvi wa bahari kuu.

**21.** **Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa Mkataba PSMA unahusika na meli zote za kigeni za uvuvi zinazotaka kuingia katika bandari zilizochaguliwa na nchi husika, na kwa kuzingatia **Ibara ya 7** ya Mkataba ambayo inahusu wajibu wa nchi mwanachama kubainisha bandari zenye sifa stahiki ambazo zitatambuliwa kwa ajili ya shughuli za ukaguzi katika utekelezaji wa Mkataba wa PSMA; ni muhimu sasa

Mheshimiwa Waziri akawaeleza watanzania ni bandari zipi ambazo kwa sasa zimekwisha tambuliwa katika kuhakikisha zinatekeleza jukumu hilo.

**22.** **Mheshimiwa Spika,** Mpango wa Taifa wa II wa Maendeleo wa Miaka Mitano ukurasa wa 251 unaelezea kuhusu kujengwa kwa Bandari ya Uvuvi katika Mikoa ya Tanga ama Dar es Salaam au Mtwara na bahati nzuri bajeti ya ujenzi kuanzia mwaka wa fedha 2016/2017 hadi mwaka 2020/2021 imeainishwa. Hoja ya msingi ambayo pia Waziri anatakiwa kulieleza Bunge ni kiasi gani hadi sasa kimeishatolewa kati ya shilingi trilioni 2.53878 zilizopangwa kwenye mpango kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa bandari ya uvuvi.

**23.** **Mheshimiwa Spika, Ibara ya 8** inaongelea utaratibu unaopaswa kuzingatiwa na meli za uvuvi za kigeni kupata kibali cha kuingia bandarini na kukaguliwa. Sharti hili linaweza kuwa jepesi na gumu kwa kuwa nchi zetu nyingi hasa za ukanda wa pwani ya Afrika Mashariki na Kusini hazina vyombo vya kufanya doria hivyo si rahisi kufahamu meli husika na mizigo iliyonayo imeipata kutoka Ukanda wa nchi gani. Hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inasisitiza kwa Serikali kuimarisha doria katika maeneo ambayo tunayamiliki ili tuweze kuwa na uhakika kwamba rasilimali zinazotoka zina manufaa kwa watu wetu na nchi yetu kwa ujumla.

**24.** **Mheshimiwa Spika**, ni ukweli kwamba kwa kila ukaguzi wa meli husika, mkataba haukuweka wazi pale meli itakapokuwa imejaza shehena ya samaki, zipimwe na kuilazimisha meli husika kulipa mrahaba kulingana na sheria, kanuni na taratibu za nchi husika. Kama hili lingezingatiwa, tunaamini ingekuwa ni fundisho, kwani hata wakifanya uvuvi haramu na kukimbia bado wangelazimika kulipa kulingana na mavuno waliyopata. Hii ni kutokana na ukweli kwamba mkataba huu unalenga kukomesha na kutokomeza uvuvi haramu unaofanywa katika ukanda wa kiuchumi kwenye bahari kuu na hilo lingekuwa ni fundisho stahiki kwa vyombo vyote vitakavyo kamatwa katika kadhia hiyo.

## IV. MAONI

**25. Mheshimiwa Spika,** ufanisi wa utekelezaji wa PSMA utapelekea mchango wa muda mrefu wa uhifadhi na matumizi endelevu wa viumbe hai na rasilimali za bahari na mifumo ya kiikolojia.

**26. Mheshimiwa Spika,** tunaporidhia mkataba huu nchini kwetu, basi hatuna budi kutekeleza majukumu yafuatayo:-

i. kuandaa sheria, kanuni na taratibu zake za utawala kitaifa;

ii. kushiriki katika mijadala ya kuandaa makubaliano, maazimio, miongozo yanayosimamiwa na Umoja wa Mataifa;

iii. nchi zinahitaji kufuata taratibu za kusaini na kuridhia mwongozo au mkataba husika ili kuwezesha kujumuisha mwongozo huo katika sheria za kitaifa;

iv. kuanzisha taratibu na masharti ya bandari ambapo meli za uvuvi zitalazimika kufuata utaratibu uliowekwa ili ziweze kutumia bandari husika;

v. chini ya mkataba wa PSMA, nchi wanachama zitalazimika kutekeleza hatua na miongozo yote kama ilivyoainishwa katika mkataba huo; na

vi. Kwenye rasimu ya waraka tunashauri suala hili lipanuliwe zaidi isiwe kwa ajili ya ukanda wa uchumi wa bahari kuu (EEZ) yetu pekee bali udhibiti uwe pia hadi kwenye Bahari Kuu (*high seas*) ambako Watanzania wanapaswa kuwezeshwa ili wakavue *EEZ* na zaidi ya hapo. Hivyo, pale ambapo kumeorodheshwa maeneo ya bahari yaani *Inner Sea*, *Territorial Sea* na Ukanda wa Uchumi wa Bahari Kuu (*EEZ)* tuongezee na Bahari Kuu kwani Watanzania pia wanaruhusiwa kuvua kwenye Ukanda wa Uchumi wa Bahari Kuu (EEZ) za nchi nyingine na pia Bahari Kuu.

Kambi rasmi ya Upinzani Bungeni inaisisitizia Serikali kuwawezesha Watanzania katika kuhamasishwa kwenye

uwekezaji na pia kuwezeshwa kwenda Ukanda wa Uchumi wa Bahari Kuu (EEZ) na Bahari Kuu kama vile ambavyo wenzetu wa nchi nyingine wanavyovua kwenye EEZs zao, EEZs za nchi nyingine na pia Bahari Kuu.

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ina maoni kuwa uanzishwaji wa Shirika la Uvuvi - TAFICO na kuendeshwa na Serikali ***is a non starter project*** bali tunaamini kuwa njia yenye tija ni kuiwezesha sekta binafsi kuingia kwenye uvuvi wa Bahari Kuu ama kwa Watanzania wenyewe kuwezeshwa au kuingia ubia au vyote viwili.

**V. HITIMISHO**

**27.** **Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani haioni sababu yoyote ya kupinga uridhiwaji wa mkataba huu kulingana na maudhui ya mkataba huu. Aidha, ili faida zinazoongelewa katika mkataba huu zikainufaisha nchi yetu, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inasisitiza kuzingatia ushauri ufuatao:-

i. Kuhakikisha bandari ya uvuvi inajengwa kwa haraka kama ilivyoelezwa kwenye Mpango wa maelendeleo awamu ya pili;

ii. Kuweka utaratibu mzuri wa kupata wakaguzi kulingana na matakwa ya mkataba;

iii. Kuwekeza katika vyombo vya kufanya doria kwenye ukanda wa uchumi na bahari kuu; na

iv. Kuimarisha masoko yetu ya ndani.

**28.** **Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo naomba kuwasilisha.

**.........................**

**Dr. Sware I. Semesi (Mb)**
**Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani-Wizara ya Mifugo na Uvuvi**
**14/11/2019**

**SPIKA:** Ahsante sana Dkt. Sware Semesi, Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Sasa naomba nimuite Mheshimiwa Waziri wa Nishati ili awasilishe Azimio la Bunge la Kuridhia Kuanzishwa kwa Ushirikiano wa Kimataifa wa Nishati ya Jua, Mheshimiwa Dkt. Kalemani, karibu tafadhali.

**Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Kuanzishwa kwa Ushirikiano wa Kimataifa wa Nishati ya Jua *(The Framework Agreement on the Establishment of International Solar Alliance)***

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Kuanzishwa kwa Ushirikiano wa Kimataifa wa Nishati ya Jua *(The Framework Agreement on the Establishment of International Solar Alliance).*

Mheshimiwa Spika, KWA KUWA Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Nchi Mwanachama wa Jumuiya ya Umoja wa Mataifa *(UN)* na kwa kuwa Mkataba wa kuanzishwa kwa Jumuiya ya Umoja wa Mataifa ina hamasisha Nchi Wanachama kushirikiana katika utafiti, uendelezaji na utumiaji wa rasilimali mbalimbali za nishati ikiwemo nishati ya jua katika kuzalisha umeme,

NA KWA KUWA Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeamua kushirikiana na nchi nyingine duniani hususan zilizopo katika ukanda wa tropiki ya kansa na kaprikoni ambazo zinapata nishati ya jua kwa wingi kuendeleza tafiti pamoja na matumizi ya nishati yakiwemo umeme.

NA KWA KUWA Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilishiriki katika Mkutano wa 21 wa *Conference of Parties* uliofanyika Jijini Paris, Ufaransa mwezi Novemba mwaka 2015 sambamba na kongamano la Umoja wa Mataifa kuhusu mabadiliko ya tabianchi *(The United Nations Frame Convention of Climate Change)* ambapo pamoja na mambo mengine, kulikuwa na makubaliano kuwa kiundwe chombo cha pamoja *(alliance)* kitakachowezesha nchi

mbalimbali duniani hususan zilizopo katika ukanda wa kitropiki kukuza tafiti katika kuzalisha nishati ya safi ambapo ni *clean energy* inayotokana na nguvu ya jua.

NA KWA KUWA, katika utekelezaji wa maamuzi yaliyofikiwa wakati wa Mkutano wa 21 wa *Conference of Parties* mwezi Novemba, 2016, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilisaini Mkataba wa *ISA* Mjini Marrakesh, Morocco na KWA KUWA Mkataba huo umetambua na kuzingatia Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Paris kuhusu mabadiliko ya tabianchi (*Paris Agreement on Climate Change);*

NA KWA KUWA Ibara ya 13 ya Mkataba inaeleza kuwa Mkataba wa *ISA* utaanza kufanya kazi siku 30 baada ya tarehe ambayo hati ya kuridhia mwanachama 15 itakuwa imekubalika na utaanza kutumika katika nchi husika baada ya kuridhiwa na sheria kupitia taratibu za wanachama;

NA KWA KUWA kutokana na mkataba huu Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itapata faida na manufaa yafuatayo:-

(a) Kuimarika kwa upatikanaji wa nishati ya umeme nchini hususan katika maeneo ya vijijini utakaochochea ukuaji wa shughuli za kiuchumi na hatimaye kukuza mapato ya wananchi;

(b) Kuongezeka kwa matumizi ya nishati safi na bora nchini na hivyo kupunguza uchafuzi wa mazingira kutokana na uwepo wa hewa ya ukaa;

(c) Kukua kwa teknolojia hasa ya umeme jua nchini na hivyo kuboresha upatikanaji wa nishati hapa nchini;

(d) Kuongezeka kwa utaalam na ujuzi wa Watanzania kutokana na fursa za mafunzo;

(e) Kuimarika kwa uwekezaji katika miradi ya nishati ya jua hususan kutoka sekta binafsi; na

(f) Kuimarika kwa mahusiano ya kiplomasia na kibiashara kati ya Tanzania na nchi nyingine zinazotekeleza mpango wa *ISA*.

HIVYO BASI kwa kuzingatia manufaa yatokanayo na mkataba huu kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwa mujibu wa Ibara ya 63(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Mkutano wa Kumi na Saba linaazimia kuridhia Mkataba wa Kuanzishwa kwa Ushirikiano wa Kimataifa wa Nishati ya Jua *(The Framework Agreement on the Establishment of International Solar Alliance - ISA*).

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono, tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Dkt. Kalemani kwa uwasilishaji mzuri sana wa Azimio hili la Bunge la Kuridhia Kuanzishwa kwa Ushirikiano wa Kimataifa wa kuhusiana na Nishati ya Jua.

Sasa naomba nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini, karibu sana Mheshimiwa Mwenyekiti mwenyewe, Mheshimiwa Dunstan Kitandula.

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuwasilisha taarifa hii kwa niaba ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa 53(6)(b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu Azimio la Kuridhia Mkataba wa Kuanzishwa kwa Ushirikiano wa Kimataifa wa Nishati ya Jua *(Framework*

*Agreement on The Establishment of the International Solar Alliance - ISA*).

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipata fursa ya kujadili mkataba huu na kufanya mapitio mbalimbali baada ya kupokea hoja hiyo kutoka Serikalini. Aidha, Kamati ilipata fursa ya kuwaalika wadau mbalimbali ili waweze kutoa maoni yao juu ya mkataba huu, vikao hivi vilifanyika hapahapa Dodoma. Niseme tu tunawashukuru sana wadau ambao walishiriki kutoa mawazo yao kwa Kamati kwa sababu maoni yao yameisaidia sana Kamati kuweza kufanya uchambuzi kuhusu makubaliano ya Mkataba wa *ISA*.

Mheshimiwa Spika, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilishiriki katika Mkutano wa 21 uliofanyika Paris ambao ulijadili mambo haya.

Mheshimiwa Spika, Mkataba wa kuanzishwa Jumuiya ya Umoja wa Mataifa unaohamasisha Nchi Wanachama kushirikiana katika utafiti na uendelezaji wa utumiaji wa rasilimali mbalimbali za nishati ikiwemo nishati ya jua unalenga katika kuziwezesha nchi hizi kuweza kupata manufaa ya matumizi ya nishati ya jua, kupunguza gharama za nishati hiyo na mambo mengine kadhaa.

Mheshimiwa Spika, katika kuuchambua mkataba huu Kamati ilitumia nyaraka mbalimbali ikiwemo Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini vilevile tafiti mbalimbali zilizofanywa na shirika letu la umeme *TANESCO* kuhusu rasilimali jua katika nchi yetu. Kamati ilitafakari na kujiridhisha juu ya faida zinazoweza kupatikana kutokana na kuridhia mkubaliano ya mkataba kama ulivyo. Faida hizo ni pamoja na hizi zinazofuata:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, ni kuimarika kwa upatikanaji wa nishati ya umeme nchini hususan katika maeneo ya vijijini utakaochochea ukuaji wa shughuli za kiuchumi na hatimaye kukuza vipato vya wananchi. Vilevile kuongezeka kwa matumizi ya nishati safi na bora nchini na hivyo kupunguza uchafuzi wa mazingira na kutoa uwepo wa hewa ya ukaa. Vilevile, mkataba huu utawezesha kukua kwa

teknolojia hasa ya umeme wa jua nchini hivyo kuboresha upatikanaji wa nishati hiyo hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, vilevile nchi itafaidika na kuongezeka kwa utaalam na ujuzi wa Watanzania kutokana na fursa za mafunzo. Kubwa ni kuimarika kwa uwekezaji katika miradi ya nishati ya jua hususan katika sekta binafsi na vilevile kuimarika kwa mahusiano ya kidiplomasia na kibiashara kati ya Tanzania na nchi nyingine zinazotekeleza mkataba huu.

Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa umeme wa jua kwa teknolojia ya *solar PV* hapa nchini upo katika kiwango cha chini sana, inakadiriwa kuwa ipo katika *megawatt* chini ya tano. Changamoto zinazochangia hali hiyo ni pamoja na kuwepo kwa utaalam mdogo, gharama kubwa za uwekezaji na ukosefu wa mitaji kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya umeme.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ushirikiano wa *ISA* unajielekeza katika kupunguza gharama za uzalishaji wa nishati na kuongeza wigo wa upatikanaji wa nishati safi, bora na endelevu ili Tanzania iweze kunufaika ipasavyo, kwa hiyo ni maoni ya Kamati kwamba ni bora nchi yetu ikaridhia mkataba huu.

Mheshimiwa Spika, aidha, katika upande wa hasara Kamati ilijielekeza kuona kama zipo hasara zozote ambazo nchi inaweza kupata kwa kuingia kwenye ushirikiano huu. Baada ya Kamati kupitia vipengele vyote 14 ilijiridhisha bila wasiwasi wowote kwamba mkataba huu ni mzuri na hauna chagamoto/hasara kwa upande wa nchi yetu. Aidha, Ibara ya 11 ya Mkataba inatoa fursa vilevile kwa nchi itakapoona hainufaiki kuweza kujitoa katika mkataba huu.

Mheshimiwa Spika, maoni na ushauri wa Kamati; Mkataba wa *ISA* unalenga kuhamasisha Nchi Wanachama kushirikiana katika utafiti, uendelezaji na utumiaji wa rasilimali mbalimbali za nishati ikiwemo nishati ya jua katika kuzalisha umeme. Kwa kuzingatia sera na azma ya Serikali yetu ya Awamu ya Tano ya kuelekea katika uchumi wa viwanda,

kama nchi tunahitaji kuwepo kwa nishati ya uhakika katika uzalishaji wa umeme. Baada ya Kamati kumaliza uchambuzi wa Azimio hili, inatoa maoni na ushauri ufuatao:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Nchi Wanachama zinaelimishwa na kuhamasishwa kuanzisha mtandao wa ushirikiano kama sehemu ya hatua ya kitaifa ya kukazia maendeleo, basi mchakato huu kwa hapa nchini unapaswa kujumuisha viongozi wa Serikali kuanzia ngazi za chini, mawakala wanaoshughulika na sekta ya nishati, asasi za kiraia, asasi zisizo za Kiserikali, sekta binafsi na wadau wengine wenye nia na malengo ya kuendeleza mifumo ya umeme hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, uanzishwaji wa mtandao wa ushirika wa *ISA* unapaswa kuzingatia taswira ya hali ya upatikanaji wa umeme wa Gridi ya Taifa hapa nchini ili uendelezaji wa uzalishaji wa umeme huu uweze kupelekwa zaidi katika maeneo ambayo hayajafikiwa na Gridi ya Taifa, Gridi ndogo na maeneo ya Visiwa na maeneo ya nje ya Gridi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia mifumo ya Serikali ya sasa katika Sekta Ndogo ya Nishati mbadala Serikali iangalie uwezekano wa Mamlaka hiyo kuunda miongozo kadhaa ambayo inaweza kujumuisha Sera, Mikakati na Mipango ya nchi hii kuendana na matakwa ya makubaliano ya mashirikiano ya Mkataba tunaouzungumzia. Aidha tunashauri Serikali kutumia Wataalam wa ndani zaidi kuliko kutumia wataalam wa nje ya Mifumo ya Serikali na siyo washauri wa nje ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, hii itaimarisha umiliki wa teknolojia na kujifunza kiufundi kwa wataalam wa ndani na hivyo kurahisisha kukubalika na kupenya kwa teknolojia ya Nishati ya jua katika pembe tofauti za nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa fedha ambazo zitapatikana kutokana na makubaliano ya Mkataba huu Serikali inapaswa kuhusisha Mashirika yake pamoja na Wadau

wa sekta binafsi katika sekta ya Nishati kama vile *AZAKI ZA KIRAIA* na Makampuni binafsi kwa kuzingatia uwezo wao, ili kuchochea zaidi uendelezaji wa maendeleo ya uzalishaji wa umeme hususan katika maeneo ya Vijijini.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali tunapendekeza Serikali kuangalia faida ya malengo ya baadaye ya nchi katika kutekeleza makubaliano ya Mkataba huu ili makubaliano haya yawe chachu ya kuendeleza maendeleo ya miaka ijayo katika uzalishaji wa umeme.

Mheshimiwa Spika, Kamati katika uchambuzi wake imebaini kuwa katika uanzishwaji wa Hisa nchi kumi na Tano za kwanza, zilizokamilisha taratibu za kusaini na kuridhia Mkataba husika zilipewa hadhi ya kuwa wanachama waanzilishi, na kwa kufanya hivyo zilinufaika na fedha zilizotengwa na Serikali ya India takribani dola bilioni kumi kwa ajili ya miradi ya uendelezaji wa miradi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, katika kiasi hicho dola bilioni mbili zilitengwa kwa ajili ya Afrika, kwa ajili ya Miradi ya Nishati Jadidifu. Kamati imebaini kuwa kutokana na nchi yetu kuchelewa kukamilisha taratibu za kuridhia Mkataba huu ilishindwa kunufaika na fursa hii.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kuwa siku zijazo ni vyema kuharakisha tathmini ya mapitio ya Mikataba ya aina hii hususan pale inapoonekana kuwa na faida za wazi na kutokidhana na matakwa ya Katiba ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru sana wewe binafsi kwa uongozi wako mahiri na kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha maoni haya ya Kamati, nimshukuru Mheshimiwa Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kuratibu na kusimamia shughuli za Bunge lako Tukufu kwa umakini na umahiri mkubwa, aidha naomba nitumie fursa hii kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Nishati na Madini kwa umahiri wao waliouonyesha katika kujadili Azimio hili, na

katika hili naomba majina yao yote yaingie katika kumbukumbu rasmi za Bunge letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitoe pia shukrani zangu za dhati kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati kwa Mheshimiwa Dkt. Medard Kalemani Mbunge Waziri wa Nishati, Naibu Waziri wa Nishati Mheshimiwa Subira Mgalu pamoja na Watendaji wote wa Wizara ya Nishati wakiongozwa na Katibu Mkuu Dkt. Khamis Mwinyimvua kwa ushirikiano wao mkubwa kwa Kamati yetu wakati wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda vilevile kumshukuru Katibu wa Bunge ndg. Stephen Kagaigai, Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndugu Michael Chikokoto, Makatibu wa Kamati Bi. Felister Mgonja na Bi. Angelina Sanga pamoja na Msaidizi wa Kamati yetu Bi. Grace Mwenye kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati yetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba Taarifa yetu yote iingie kama ilivyo, tulivyoiwasilisha naomba kuwasilisha na naunga mkono Azimio. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mwenyekiti wa Kamati hii ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Dunstan Kitandula tunakushukuru sana kwa kutusomea Taarifa ya Kamati yako vizuri kabisa na kwa umakini mkubwa.

Sasa, nimuite Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Nishati, karibu sana. *(Makofi)*

**MHE. TUNZA I. MALAPO - MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KUHUSU WIZARA YA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika Azimio la kuridhia kuanzishwa kwa ushirikiano wa Kimataifa wa Nishati ya Jua yaani *Protocol Framework Agreement on The Establishment of The International Solar Alliance (ISA)* yanatolewa kwa Mujibu wa Kanuni ya 53(6)(c) ya Kanuni za Bunge, Toleo la mwaka 2016.

Mheshimiwa Spika, *The International Solar Alliance (ISA)* ni ushirikiano unaotarajiwa kuwa na nchi wanachama 121 ambao ulianza na India ikiwa ndio mwanzilishi wake. Nyingi ya nchi hizo ni zile zinazojulikana kama *sunshine countries*, ambazo zimelalia au katikati ya tropiki ya *Cancer* na zingine kwenye Tropiki ya Capricon. Hadi sasa Mataifa 74 tayari yameshasaini ushirikiano huo na kati ya hayo mataifa 52 yamekwisha ridhia ushirikiano huo.

Mheshimiwa Spika, lengo la ushirikiano huu ilikuwa ni kunufaika na nishati jua na hivyo kupunguza utegemezi wa matumizi ya nishati itokanayo na mafuta yaani (*fossil energy*) na hivyo kuwa nyenzo mojawapo ya kupambana na mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Spika, mbali ya lengo hilo, pia ushirikiano huu unatarajia kupunguza mahitaji makubwa ya nishati hasa kwa nchi wanachama ambazo nyingi zake ni zile zinazoendelea. Nishati ya jua ni ya uhakika kwa kuwa inapatikana popote ambapo jua linaangaza kwa muktadha wa nchi zilizopo katika ukanda wa tropiki ya *Cancer* na *Capricon*.

Mheshimiwa Spika, ushirikiano huu ni mkataba unaohusisha Mashirika ya Kimataifa ambayo wanachama wake ni Mataifa huru. Mataifa ambayo hayapo kwenye ukanda wa Tropiki ya *Cancer* au *Capricon* nayo yanaruhusiwa kujiunga na kunufaika na yale yote yatokanayo na mkataba huo ila tu hayataruhusiwa kupiga kura kwa ajili ya maamuzi yoyote yatakayotolewa kwenye vikao halali vya ushirikano huo.

Mheshimiwa Spika, mpango huu ulizinduliwa na Waziri Mkuu wa India kwenye kikao cha India Africa ambacho kilihudhuriwa na wakuu wa nchi toka Afrika, kikitangulia na kikao cha mwaka cha Umoja wa Mataifa kuhusu mabadiliko ya tabianchi kilichofanyika Paris Novemba 2015.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni mojawapo ya nchi ambazo zilishasaini makubaliano ya ushirikiano wa nchi

mwanachama wa matumizi ya Nishati Jua ambapo mkataba ulianza kuwa wazi kwa ajili ya Mataifa kusaini hapo Novemba 2016. Hili ni jambo zuri na kubwa japokuwa utekelezaji wake kwa vitendo ndio jambo ambalo kwa kiasi kikubwa linahitaji utashi wa kisiasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, India kwa kushirikiana na Ufaransa wanatoa usaidizi kwa nchi mwanachama katika kujenga miundombinu ya utekelezaji wa miradi ya nishati itokanayo na jua. Ushirikiano huu umetenga kiasi cha dola za Kimarekani trilioni moja kama fedha za uwekezaji kwa lengo la kupunguza gharama za nishati jua hasa kwa maeneo ambayo jamii zake za vijijini haziwezi kumudu gharama. Ushirikiano uliidhinisha India ili kutimiza au kufanikisha malengo ya kuzalisha nishati ya jua ya GIGA WATT 100 sambamba na GIGA WATT 175 ya nishati jadidifu yaani *Renewable energy* ifikapo mwaka 2020/2022.

Mheshimiwa Spika, taarifa zinaonesha kuwa Juni 30 2016 ushirikiano uliingia makubaliano na Benki ya Dunia ili kuweza kupata fedha kwa ajili ya kuendeleza au kutekeleza miradi ya nishati jua *SOLAR ENERGY*. Benki ilitakiwa kuwa na jukumu la kutafuta zaidi ya *US Dollar* trilioni moja kwa uwekezaji utakaohitajika hadi mwaka 2020/2030 ili kutimiza malengo ya *ISA* katika kuhakikisha uzalishaji wa nishati jua kwa gharama nafuu.

Mheshimiwa Spika, mkataba huu wa ushirikiano ambao unatakiwa kuridhiwa na Bunge hili umegawanyika katika Ibara 14 ambapo kila Ibara imejieleza kwa kifupi na kwa ufasaha.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 1 inaelezea kwa kifupi lengo la ushirikiano huu kwamba ni kutafuta suluhisho la pamoja katika kutatua changamoto zilizopo za matumizi ya nishati jua katika mataifa wanachama kwa matumizi na mahitaji yao.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaifanyia tafakari Ibara hii na kuja na muafaka kwamba ni kweli kuwa

katika kuhakikisha Tanzania inakuwa nchi ya viwanda na hivyo kupelekea kuwa nchi ya uchumi wa kati, uwekezaji katika nishati ni jambo ambalo haliepukiki.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa fursa ya sisi kuwa washirika wa *ISA* ilikuwa tangu mwaka 2016, ina maana kwamba fursa pia ya kupata usaidizi wa fedha, elimu na teknolojia katika uzalishaji umeme kwa kutumia nishati ya jua kama wenzetu wa India ambao wameweza kuzalisha umeme wa jua wa *GIGA WATT* 20 ndani ya kipindi kisichozidi miaka mitano na sasa wanatarajia kuzalisha umeme wa jua wa *GIGA WATT* 100 pamoja na *GIGA WATT* 175 kwa nishati jadidifu ifikapo mwaka 2020/2022 na sisi tulikuwa na fursa hiyo lakini tukashindwa kuitumia.

Mheshimiwa Spika, tunapofanya mambo yetu ni vizuri tukachungulia na kwa wenzetu ambao wako kwenye mazingira kama sisi ili tuweze kubadilishana uzoefu, sasa wao ndani ya miaka mitano wamezalisha umeme wa jua wa *GIGA WATT* 20 sisi tunatarajia kuzalisha umeme wa *MEGA WATT* 2100 za umeme wa maji ndani ya miaka mingapi? Hapa ndipo ule usemi unaosema kuwa ukitaka kwenda haraka tembea peke yako, lakini ukitaka kufika mbali basi tembea na wenzio. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa muktadha huo ni dhahiri ile haraka yetu ya kufua umeme wa maji kwenye maporomoko ya Mto Rufiji itatuletea matatizo makubwa kiuchumi kwa siku zijazo, kwani *ISA* inatoa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hiyo ya umeme wa jua, rejea Ibara ya 6 ya Mkataba inayohusu, *budget and financial resources*. Aidha, kama tulivyoainisha hapo awali kuwa Benki ya Dunia imeshatoa ahadi ya kutafuta fedha kiasi cha dola za Kimarekani trilioni moja kwa ajili ya kusaidia utekelezaji wa miradi ya nishati jua kwa mwanachama wa *International Solar Alliance*.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo machache kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Tunza Malapo Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Nishati nakushukuru sana kwa mchango wako pia. Sasa Waheshimiwa Wabunge tunaingia kwenye eneo la uchangiaji na tutaanza na Mbunge wa Mafia. Mheshimiwa Mbaraka Dau, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Saada Salum Mkuya.

**MHE. MBARAKA K. DAU:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa fursa hii, ili niweze kuchangia kwenye Azimio hili, awali ya yote ninaunga mkono Bunge letu kuridhia Itifaki hii ya kuzuia Uvuvi haramu.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiokuwa na shaka katika eneo letu la *exclusive economic zone (EEZ)*.

**SPIKA:** Waheshimiwa katika kuchangia mnaruhusiwa kuchangia ama mojawapo ya Azimio hili ama Maazimio yote katika uchangiaji wako. Lakini pia niwakumbushe Kamati ya Uongozi tukitoka saa saba *by* saa saba na nusu tuwe pale kwenye Ukumbi wa Spika, Kamati ya Uongozi tukutane Ukumbi wa Spika kuna kikao kidogo, Mheshimiwa Mbaraka Dau endelea.

**MHE. MBARAKA K. DAU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa ufafanuzi huo, nitachangia kwenye Azimio la Itifaki ya Uvuvi haramu, ni ukweli usiokuwa na shaka katika eneo letu la *exclusive economic zone EEZ* kumekuwa na vurugu nyingi sana ya meli za kigeni zinazoingia kwenda kuvua kule bila ya na vibali na ruhusa ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa haina uwezo, ilikuwa haina uwezo wa aina mbili, haina uwezo wa Vyombo vya kwenda kuwazuia kule kwa sababu ni mbali na bahari ni kali sana, lakini la pili tulikuwa hatuna uwezo kwa sababu Mikataba kama hii ya Kimataifa haikuwepo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Itifaki hii inakwenda kujibu swali hilo gumu kwamba sasa tunao uwezo, wale

ambao wataingia katika eneo letu la *EEZ* na tukaweza kuwaona kwenye ile *VMS Versa Monitoring System* yetu pale *DSFA*. Tunao uwezo sasa wa kwenda kuwafatilia watakapokwenda kuweka nanga meli zao katika nchi Wanachama hizi sitini, tunaweza kwenda kufatilia kule na kujua kwamba meli kadhaa iliingia katika *EEZ* ya Tanzania bila ya kibali ikavua na sasa Serikali inachukua hatua.

Mheshimiwa Spika, sasa faida kubwa inayopatikana ni hiyo, na mimi katika faida hiyo nilikuwa na maombi au nyongeza au ushauri kwa Waziri mwenye dhamana wa aina tatu, ushauri wa kwanza, twende tukafanye *overall* ya *regulation* zetu, Kanuni zetu za ile Taasisi yetu ya Uvuvi wa Bahari Kuu.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu gani? Kwa sababu sasa tunayo nyenzo ya kujua kwamba kuna meli iliingia kwenye *EEZ* yetu haina kibali ikaenda kutia nanga labda *Seychelles* tunatumia Mikataba ya Kimataifa kuikamata kule, Je, tumeshaikamata sasa tunafanya nini? Kwa sababu Sheria inataka ile meli au meli zile zije zihukumiwe kwa mujibu wa Sheria za Tanzania. Sasa ipo haja sasa ya kwenda kufanyia *overall* zile Kanuni zetu kwamba sasa je, meli ya aina hii inayokamatwa itaingia kwenye kosa lipi? Tunaitaifisha, tunapiga faini, tunafanyaje?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilikuwa naomba wenzetu wa, na nimemsikia Mkurugenzi Mkuu hapa wa Mamlaka ya Bahari Kuu yupo wenzetu wa Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka ile waende wakaanze kufanyia kazi hizo *regulation* sasa ili tuweze kunufaika na hii Itifaki.

Mheshimiwa Spika, ombi au ushauri wa pili, Bandari ya Uvuvi limesemwa hapa na Kamati, limesemwa na Taarifa ya Kambi Rasmi ya Upinzani, bila ya kuwa na Bandari ya Uvuvi na nilizungumza hapa nadhani wiki iliyopita, bila ya kuwa na Bandari ya Uvuvi faida hizi zinatutoka kwa sababu hii *EEZ* yetu kwa wakati mmoja inaweza ika-*accommodate* meli zaidi ya mia moja, zinavua wakishavua wanakwenda kwa wenye

Bandari za Uvuvi *Seychelles*, *Mauritius, Mordait* na maeneo mengine huko.

Mheshimiwa Spika, sasa sisi tunakosa haya manufaa tukiwa na Bandari yetu ya Uvuvi zile zile meli zile tutazishawishi zije huku kwenye Bandari yetu zianze kushusha ule mzigo wafanye *processing* halafu baadaye na biashara yenyewe itaanza ku-*boom* kama vile ambavyo tulishuhudia biashara ya minofu ya samaki kule Mwanza kipindi kile Ndege zinakuja kuchukua mzigo na kuondoka.

Mheshimiwa Spika, nafasi ile bado tunayo kwa kupitia Itifaki hii na kuweza kufufua au kujenga Bandari yetu ya Uvuvi ambayo itasaidia sana katika kuwavutia sasa hawa wenye meli, tunaweka *regulations* kwa mfano sasa hivi tuna *regulation* zinazowataka wale wanaovua katika Bahari Kuu waje katika Bandari zetu, lakini wanashindwa kuja kwenye Bandari zetu kwa sababu hatuna Bandari za Uvuvi, tuna Bandari za Mizigo na Sheria za Kimataifa zinakataa kushusha mzigo wa chakula kwenye Bandari ya Mizigo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naendelea kusisitiza na kumuomba Mheshimiwa Waziri ule mchakato wa kujenga Bandari ya Uvuvi hata hii ya kununua meli inaweza ikasubiri tuanze na Bandari ya Uvuvi, ikijengwa Bandari ya Uvuvi *multiply effect* yake ni kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, kutakuwa na ajira kwa vijana wetu kwa sababu inakuja na *logistics centers* zile, kutakuwa na ajira, biashara ita-*boom* kwa maana ya kwamba sasa mizigo itakuwa inakwenda ama kupitia Uwanja wa Ndege au kupitia kwenye Bandari zetu kwenda sokoni na maeneo mengine ya nchi.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia, pia nina ombi jingine dogo kwa Mheshimiwa Waziri, tumeona kwamba moja ya faida tutakazozipata hapa ni kunufaika na misaada mbalimbali inayotolewa na *FAO* kwa Tanzania. Kule Mafia eneo la Kitutia ndiyo *nursery*, ndiyo *labour* ya samaki zaidi ya asilimia 70 wanaozaliwa katika Bahari ya Hindi, lakini eneo

lenyewe la Mafia limechoka, eneo lenyewe halitunzwi, eneo lenyewe wananchi wale ambao wanaitunza ile rasirimali hawanufaiki na chochote.

Mheshimiwa Spika, ningeomba kupitia Itifaki hii na Mheshimiwa Waziri tumeambiwa kwamba kutakuwa na aina hiyo ya misaada mbalimbali, basi tuangalie namna gani lile eneo litakavyoweza kutunzwa vizuri na kuweza kuleta manufaa makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa fursa hii, na ninaridhia Bunge letu liliridhie Itifaki hii ya Uvuvi haramu katika Bahari Kuu, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, nakushukuru sana Mheshimiwa Mbaraka Kitwana Dau kwa mchango wako. Sasa nilishamtaja Mheshimiwa Dkt. Saada Mkuya Salum na atafuatiwa na Mheshimiwa Ruth Mollel. Mheshimiwa Saada, hayupo ehhe? Mheshimiwa Ruth na atafuatiwa na Mheshimiwa Jitu Soni.

**MHE. RUTH H. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii, nami niweze kuchangia katika itifaki hizi mbili. Moja, nitachangia ya *solar energy* na pia nitagusia kidogo kwenye hii ya *PSMA* ya *FAO.*

Mheshimiwa Spika, hii itifaki ya *International Solar Alliances,* tuliisaini mwaka 2015, tukiwa na ule Mkutano wa *Climate Change, Paris,* mwaka 2015 na sasa imeletwa turidhie. Tumeona kwamba baadhi ya nchi, kwa mfano India ambao pia waliridhia mkataba huu, wao wamefika mbali sana katika kutekeleza huu mkataba na kuanza kutumia *energy* hii ya *solar* ambayo ni muhimu sana; kwa sababu kwanza inafika vijijini, ambako *energy* nyingine ya umeme haifiki na vilevile ni *energy* ambayo ni safi kuliko tunavyoona kwenye *energy* nyingine ambazo zinaleta *carbon monoxide* katika mazingira.

Mheshimiwa Spika, sasa napendekeza kwamba, huu mkataba tumeusaini na ingekuwa ni vizuri vilevile kuhakikisha

kwamba tunakuwa na mpango mkakati. Tumepitisha itifaki nyingi hapa na sijui Bunge lako Tukufu ni kwa jinsi gani linafuatilia hizi itifaki ambazo tunazipitisha hapa kuona kwamba zinatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, vilevile mradi huu utaongeza tija kwa wanavijiji na kuboresha maisha yao na kuwa na umeme wa kuwasaidia kuzalisha na kuongeza pato lao la nchi. Kwa hiyo, napendekeza kwamba, kuwepo na mpango mkakati na Waziri atueleze utakuwa vipi, ni kwa jinsi gani sasa, tuna *solar energy* na tuna *REA?* Tuone ni jinsi gani atajipanga, aweze kutekeleza hizi *energy* zote kwa pamoja; ya *REA* na *Solar.*

Mheshimiwa Spika, nitafurahi sana kama atakapokuja atatupa tu taarifa ni kwa jinsi gani hizi *energy* zote zitakwenda kwa pamoja? Kwa sababu tunajua *REA* nayo inakwenda vijijini na hii *solar* pia inakwenda vijijini; na *solar* ni rahisi zaidi kwa sababu haihitaji miundombinu mikubwa *other than* hizi *solar panels* na miundombinu mingine midogo midogo na jua tunalo kila siku. Kwa hiyo, nilikuwa nafikiri kwa mawazo yangu, itakuwa ni gharama nafuu zaidi kutekeleza hili la *solar energy,* sambamba na *REA* vilevile.

Mheshimiwa Spika, nikienda kwenye suala ya ile itifaki nyingine ya kuzuia uvuvi haramu kwenye *deep seas;* ni vizuri tukaridhia huu mkataba, kwa sababu, kwanza kutakuwa na msaada, kwa sababu, bajeti yetu kama tunavyojua haikidhi mahitaji. Tutakuwa na bajeti ya msaada ambayo tutaitumia kwa ajili ya kujenga uwezo wa watu wetu na vilevile kulinda rasilimali yetu ambayo ni muhimu kama Wabunge wengine wengi walivyochangia. Siyo hivyo, kulinda rasilimali pia. Hata meli zinazokuja, zita-*generate income* ambayo itaingia katika mzunguko wa fedha.

Mheshimiwa Spika, tunajua jinsi ambavyo uvuvi haramu umekithiri. Kwa hiyo, kwa kuridhia huu mkataba, tutasaidia kulinda rasilimali zetu zisiweze kupotea na badala yake tuweze kupata fedha zika-*generate revenue* ambayo

tutaweza kuendelea katika maisha yetu na kujenga uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, ninaipongeza Serikali kwa kuleta hizi itifaki hapa mbili tuziridhie na tuwe na *monitoring system;* hiyo ndiyo *concern* yangu kubwa. Tuna-*monitor* vipi sisi Bunge, kwamba hizi itifaki tunazopitisha hapa kila siku, zinafuatiliwa na zinafikia wapi? Maana yake, tunapimaje utekelezaji wa hizi itifaki? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Ruth Hiyob Mollel. Kwa wasiomfahamu Mheshimiwa Ruth Mollel, alikuwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira na alihudhuria hizi *coup* kadhaa zilizopitisha baadhi ya maazimio makubwa makubwa ambayo baadhi yake ndiyo haya tunayoyapitisha hapa. Hongera sana Mheshimiwa Ruth Mollel. *(Makofi)*

Sasa namwita Mheshimiwa Salum Rehani na atafuatiwa na Mheshimiwa Anastazia Wambura na Mheshimiwa Mussa Mbarouk, ajiandae.

**MHE. SALUM MWINYI REHANI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru nami kupata nafasi hii ya kuchangia kwenye itifaki hii. Kwanza niseme kwamba naunga mkono na ninaomba Wajumbe mbalimbali tuweze kuiridhia itifaki hii ya *FAO* ambayo sasa inatupeleka na sisi kutuunga miongoni mwa nchi ambazo zinanufaika katika itifaki hii kwa wale waliokuwa wameanza kuridhia. Sisi tumechelewa.

Mheshimiwa Spika, hasara ya mwanzo ambayo inatokana na kutokuridhia kwetu, Tanzania imekosa siyo chini ya dola za Marekani 184,000 ambazo zilikuwa ni fedha maalum za nchi ambazo zinapitiwa na bahari upande wa mashariki na hasa zile ambazo zinatumika kupitishia meli kubwa zinazomwaga dawa na sumu mbalimbali katika eneo letu. Kwa hiyo, eneo letu limekuwa linaathirika sana na watu ambao wanafanya biashara ya kutupa uchafu mbalimbali hasa wa sumu katika eneo letu, lakini sisi kwa kutokuridhia

mkataba huu, tumeshindwa kutetewa au kulindwa kwa pamoja na wale waliokuwa wameridhia mkataba huu.

Mheshimiwa Spika, la pili, tunaingia miongoni mwa nchi ambazo zitakuwa zina ule mpango, *routine research* na *monitoring* ya meli zile ambazo zinaingia katika mkumbo wa meli ambazo zinaitwa za eneo la *Indian Ocean and Pacific,* ambapo tutakuwa tunapata takwimu sasa za *fish stock* karibu kila baada ya miaka mitatu katika eneo letu hili la bahari kuu.

Mheshimiwa Spika, lingine mabalo linanufaisha; Tanzania pamoja na kuwa na ukubwa wa eneo la mita za mraba laki mbili, tulizoziongeza hizo la uvuvi wa uvuvi wa bahari kuu, lakini tumeomba tena eneo lingine tuongezewe la zaidi ya *nautical miles* 150,000. Kwa hiyo, tunakwenda kuwa na eneo kubwa zaidi la uvuvi wa bahari kuu au eneo la bahari kuu ambalo tunatakiwa sisi wenyewe tuweze kulilinda, tuweze kulitumia na litunufaishe kama ni sehemu ya rasilimali.

Mheshimiwa Spika, sasa huwezi kuwa na eneo kubwa kama hili halafu ukasema kwamba wewe huungi mkono wenzako ambao wanatumia vyombo mbalimbali kuweza kulilinda eneo hilo. Kwa hiyo, tukiridhia, hizo ni moja kati ya faida ambazo tutazipata.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo linakwenda kutupeleka sasa hivi, ni kwamba Serikali na mtazamo wa watu mbalimbali, tumeomba hapa kwamba, nchi hii iwekeze kwenye uvuvi wa bahari kuu. Tukiwekeza kwenye uvuvi wa bahari kuu na sisi sasa tunakuwa miongoni mwa nchi ambazo zinaingia kwenye ile wanaita *Tuna World Market;* Soko lile la Japani, kuna Soko la China na Soko lile la *Norway,* ambapo nasi tutapata fursa ya kuweza kuuza samaki wetu katika masoko ya nje.

Mheshimiwa Spika, faida nyingine ambayo imejitokeza hapa, ni kwamba zile meli ambazo tutazikamata zikichafua mazingira katika eneo letu la bahari kuu, tutaweza kupiga faini au kuweza kuzilipisha faini za uchafuzi wa

mazingira pale kisheria, kuliko kusema kwamba tunatumia sheria zetu za ndani, kitu ambacho wale wanaotumia sheria za nje, hatuwezi kuwabana na baada ya kufanya huo uchafuzi wanakwenda zao, kwa sababu hakuna kitu au hakuna mkono wa sheria unaowakamata na kuweza kuwaadhibu kwa vitendo ambavyo wanatufanyia.

Mheshimiwa Spika, la mwisho katika faida ambazo zinapatikana, ni kulindwa katika ile wanaita *Ocean Biological Weapons,* ambapo katika eneo letu la bahari kuu huweza kutumika kwa uhalifu wa kibiolojia. Katika njia mbalimbali ambazo wenzetu nchi za nje zinatumia uharamia huo, eneo letu litakuwa linalindwa na vifaa maalum, zile *VMS,* maalum za Kimataifa kupita *satellites* na chochote kitakachopita katika eneo hilo kwa nia ya kufanya uhalifu wa kibiolojia, kisheria zitaweza kuchukua mkondo wake.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nawamba Waheshimiwa Wabunge wa Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, turidhie, kwa sababu tukiridhia na sisi tutapata faida ya kuwemo miongoni mwa hao watu ambao ni wanufaika wa mkataba huu.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, nawaomba Serikali kwa upande mwingine, tuweze kushiriki baadhi ya mikutano na makongamano ambayo yanakwenda kutunufaisha na miradi mbalimbali ya kimazingira katika eneo letu. Bado tu tuendelee kuwakumbusha Watanzania kwamba, asilimia 67 ya *tuna* ambao wanaliwa duniani au wanaoingia katika Soko la Dunia, wanatoka katika *belt* hii ya Tanzania ambapo ni eneo lile la Kizimkazi mpaka Kitutio kule Mafya.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, fursa hii iliyokuweko duniani mwote, tunaweza kusambaza samaki duniani, tuweze kuilinda na kuitunza. Ni kitu ambacho kwa kweli hakiwezi kupatikana, yaani faida yake haiwezi kupatikana kwa miradi mingine yoyote. Bado tuikumbushe Serikali kwamba eneo hili tukiwekeza, hakuna cha dhahabu, hakuna cha bidhaa nyingine yoyote itakayoweza kuishinda hii *blue*

*sea* kwa kipato. Kwa hiyo, nawataka wadau mbaimbali, wawekezaji mbalimbali, waje tukae na Serikali, tuangalie uwezekano wa kuwekeza katika eneo hili la uvuvi wa bahari kuu.

Mheshimiwa Spika, siyo hilo tu, fursa nyingine ambayo tunaipata sasa Tanzania, baada ya kuondoa ile 0.4, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa hatua kubwa aliyoifanya na kuridhiana na wenzie wa Zanzibar na kuweza kumaliza tatizo lile la 0.4, sasa tunakwenda kurudisha leseni za uvuvi wa bahari kuu, na kuifanya Mamlaka ile ya Uvuvi wa Bahari Kuu kuwa na kipato cha ajabu sasa hivi. Kwa sababu, *pending* ya meli ambazo zinakaa zinagoja kufanya uvuvi wa bahari kuu ni zaidi ya 200 zinangoja leseni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *issue* ilikuwa ni 0.4, Serikali imesikia kilio cha wadau, imekiondoa kwa muda hivi. Nami nasema kwamba, tukiweke pembeni, ili tuweze kupata faida ya meli zile ku-*land* katika maeneo yetu au kubaki katika maeneo yetu, ambapo kila meli itaweza kuacha zaidi ya shilingi milioni 40, ikija kutua katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Spika, vilevile tusisahau; tujiandae sasa na kufaidika na *by-catch* ambazo zitakuja katika maeneo yetu, ambazo zitaziba *gap* lile la upungufu wa samaki, ambao wanahitajika kwa kupunguza lishe na utapia mlo uliokuweko hapa nchini. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Rehani, Mheshimiwa Anastazia Wambura, atafuatiwa na Mheshimiwa Mbarouk.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hoja zetu za maazimio mawili. Kwanza, niseme naunga mkono hoja za maazimio yote mawili ambayo ni Azimio la Nishati ya Jua na Azimio la Mkataba wa Kimataifa wa *FAO*.

Mheshimiwa Spika, nitazungumzia zaidi Azimio hili la Mkataba wa Kimataifa wa *FAO*. Nianze tu kwa kusema

kwamba, Azimio hili linahusu sana vipengele vitatu, ambapo kimojawapo kinahusu *illegal,* ambayo ni uvuvi usiozingatia sheria na cha pili ni *unreported* na cha tatu ni *unregulated*. Sasa katika hiki cha tatu cha *unregulated fishing,* niseme tu kwamba, katika suala zima la udhibiti hatuwezi tukaepuka kufanya *resource assessment,* kama nchi.

Mheshimiwa Spika, huwezi ukadhibiti kama hujui una kiasi gani cha rasilimali au aina gani ya rasilimali ya mazao ya bahari. Kwa hiyo, naomba sana Serikali, katika kutekeleza suala zima la udhibiti, iweke nguvu zake katika utafiti ili kusudi tuweze kujua ni kiasi gani ambacho tunacho katika bahari yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zipo hoja na dhana tofauti tofauti katika suala hili. Kwa sababu kuna wengine ambao wanasema kwamba, aina kubwa ya samaki bahari yetu kuu ni jodari; na hawa jodari wana-*move* sana, wana-*move faster*, hawakai katika eneo moja la nchi yetu. kwa hiyo siyo wetu. Pia, wanasema kwamba ufanyaji wa *resource assessment* ni kitu kigumu sana, lakini mimi niseme tu kwamba hii siyo hoja kubwa sana kwa sababu hata kama tutakuwa tumemsikia vizuri mchangiaji aliyetangulia, ametueleza wazi kwamba asilimia 70 ya jodari inatokea Mafia, katika eneo la Kitutia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni kwamba hawa samaki ni wetu na tuna kila sababu ya kufanya *resource assessment.* Hata ukiangalia katika mbuga yetu ya Serengeti, utaona kwamba wale nyumbu, pundamilia na wanyama mbalimbali huwa wana-*move* kutoka eneo letu la Tanzania na wanaenda Kenya, lakini *resource assessment* huwa inafanyika. Tunajua tuna kiasi gani cha nyumbu, tunajua tuna kiasi gani cha pundamilia na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hili suala naomba Wizara isilikwepe, itilie maanani, iwezeshe vituo vyetu vya utafiti *(TAFIRI)* na hata Chuo chetu cha Mbegani ili waweze kushirikiana kufanya *resource assessment,* ndipo tutakapoweza kudhibiti vizuri.

**SPIKA:** Mheshimiwa Anastazia, nilitaka kukwambia tu, hawa nyumbu ambao wanazunguka Kenya, Masai Mara kurudi Tanzania na kurudi Kenya tena, zaidi ya 90% wanazaliwa Tanzania. Endelea tu namchango wako. *(Makofi)*

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa taarifa.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo naependa nizungumzie ni kuhusiana hasa na faida kubwa ambayo tunapewa na huu mkataba. Tunapewa fursa kubwa sana na hasa kupitia ile *United Nations Conversions on the Law of the Sea,* ambapo kuna kifungu kimoja ambacho kinazitaka hizi nchi wanachama wahakikishe kwamba wanatumia rasilimali hizi za bahari wao wenyewe na ile ziada ndiyo wanawapa nchi nyingine na hasa kipaumbele kiwe kwa zile nchi ambazo hazina bahari.

Mheshimiwa Spika, hapa napenda tu kusisitiza kwamba Serikali yetu sasa inatakiwa iangalie suala zima la ustawi wa wananchi na hasa kwa kuzingatia upatikanaji wa samaki kama lishe kwa wananchi. Kwa kweli hili ni muhimu sana na hasa ukiangalia kwamba katika nchi yetu matumizi ya samaki ni madogo sana, lakini ni muhimu sana kuliko hata nyama na vyakula vingine. Samaki ni muhimu sana kwa afya, lakini tunatumia kilo karibu saba hadi kumi kwa mwaka na wakati mahitaji hasa yanatakiwa tupate takribani kilo 20 kwa mwaka. Kwa hiyo, tunachotakiwa sasa kufanya ni kuwawezesha wavuvi wetu wadogo waweze kupata hawa samaki kwa ajili ya kuwawezesha wananchi wapate lishe bora.

Mheshimiwa Spika, kuna suala zima la Sheria ya *DSFA* pamoja na kanuni zake. Kumekuwepo na malalamiko ambayo tumeyashuhudia hasa kutoka Zanzibar, kwamba, kulikuwa na kanuni ambayo inawataka wale wavuvi waweze kuleta *by-catch* katika nchi husika. Wanapokuwa wamevua na kupata wale samaki ambao hawakuwa wamepewa ruhusa yake kuwavua, basi wawalete katika nchi husika. Sasa

kilichokuwa kinatokea ni kwamba, wanawaleta wale samaki, halafu wanauza. Kwa hiyo, kilio kwa wavuvi ni kwamba bei ya samaki inashuka na wakati wao wametumia gharama kubwa katika kuvua.

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kupendekeza hapa ni kwamba, hii Sheria ya *DSFA* pamoja na kanuni zake, irejewe ili kusudi suala zima la *by-catch* pale ambapo tutakuwa tumeziruhusu sasa meli nyingine za nchi za nje kuja kuvua samaki, suala la *by-catch* liwekewe utaratibu maalum ili kusudi wale wavuvi ambao wanavua karibu karibu waweze kuwapata hawa *by-catch* angalau waweze kushusha bei ya samaki kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba, sheria au ule Mkataba wa *UNCLOS* unasema kwamba hawa *by-catch* ni mali ya nchi husika, siyo mali ya wale wavuvi wakubwa. Kwa hiyo, ni makosa makubwa sana wanapokuwa wakileta samaki halafu wanawauza wao wenyewe kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo ningependa nisemee, unapofanya *regulation* au udhibiti, huwezi kuepuka suala zima la kuwa na bandari. Bandari ya Uvuvi ni lazima, lakini vilevile *dry-dock,* sijui inaitwaje kwa Kiswahili. *Dry-dock* ni muhimu sana ili kusudi kuweza kuzihudumia zile meli ambazo zinakuja pale. Badala ya kusema kwamba wanaenda nchi jirani, waende Mauritius au waende Kenya, basi wafanyie pale pale matengenezo ambapo inaweza ikahakikisha nchi yetu inapata kipato kikubwa ukichanganya pamoja na tozo za leseni na mambo mengine basi hata *dry-dock* inaweza ikachangia kukuza uchumi.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii ya kuchangia, ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana, nakushukuru sana. Mheshimiwa Anastazia Wambura alikuwa ndio Mwenyekiti wa Kamati yetu Maalum kwa ajili ya masuala yanayohusiana na uvuvi wa bahari kuu.

Nilishakutaja Mheshimiwa Mussa Mbarouk, nawe ukichangia kwa kifupi nitafurahi. Atafuatiwa na Mheshimiwa Ally Saleh.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Spika, ahsante; na mimi niungane na wenzangu kwanza kuunga mkono kuridhia nchi yetu kujiunga na itifaki hizi ambazo zilizotajwa hapa ambazo ni *FAO* na masuala ya umeme wa jua yaani *solar power*. Mimi nianze kuzungumzia kwenye suala hili la mkataba wa *FAO*.

Mheshimiwa Spika, wazungumzaji waliopita wamezungumza lakini ni ukweli usiofichika; ni kweli kwamba meli nyingi za nje zinavua katika bahari yetu bila sisi wenyewe kufaidika, na hili tuliligundua tulipokuwa kwenye ile Kamati Maaluma. Tukaona kwamba kuna meli zinakuja zinatumia bendera yetu lakini wanavua halafu mapato sisi hatupati kodi wala hatupati hao *bycatch* wanaotajwa.

Mheshimiwa Spika, labda Mheshimiwa Mwenyekiti wangu wa Kamati hakuifafanua vizuri hiyo *bycatch.* Ni samaki wale ambao wanaovuliwa hasa kuna Kanuni za kiuvuvi kwamba lazima katika ile nchi ambayo mmevua mpeleke samaki kwa ajili ya lishe kwa matumizi mbalimbali, labda kwa mfano kama kwenye watoto au shule au magereza ni Kanuni inatakiwa samaki wale washushwe hapo, na wasiuzwe.

Mheshimiwa Spika, lakini sasa kama alivyose aliyekuwa Mwenyekiti wetu; wamekuwa wakishushwa hapa; kwanza hatuna bandari ya uvuvi, kwa hiyo wanaposhushwa wajanja wachache wananufaika wanawachukua wale samaki halafu wanawuza; sasa hili Wizara nalo iliangalie. Mimi, si kwa kujipendelea, lakini niseme hii bandari ya uvuvi ni vizuri ikajengwa haraka na nilikuwa napendekeza basi kama kuna sehemu ya kujengwa basi ingejengwa Tanga kwa sababu hakuna msongamano mwingi kwa masuala ya uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na hilo mimi niseme tu kwamba tu kwamba tumeona kwamba katika masuala mazima ya uvuvi...

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbarouk ijengwe Tanga sio Kongwa? *(Kicheko)*

**MHE. MUSSA B. MBAROUK**: Mheshimiwa Spika, Kongwa hakuna bandari, kwa hiyo hili jambo ni vyema tukalifanya.

Mheshimiwa Spika, pia tumeona faida zinazopatikana kutokana na kuridhia hii mikataba tumeona kumbwa tunapata fedha za mafunzo za kujenga uwezo lakini tunapata pia misaada ya vifaa vya doria. Kwenye nchi zetu tumejifunza kwamba nchi kama *Seychelles*, *Mauritius* na kwingineko wanazo meli za doria, sisi hapa hatuna. Sasa Serikali nao baada ya kuridhia hili jambo la uvuvi lakini iangalie namna ya kupata hizi meli za doria ambazo tukijiunga tutapata misaada lakini na sisi wenyewe pia tujipange kuwa nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine hata meli za uvuvi zitatusaidia tutapata ajira kwa vijana wetu lakini na Serikali itapata fedha za mapato mengi kutokana na uvuvi wa bahari kuu. Kama alivyosema msemaji mmoja, kwamba kama tukisimamia uvuvi wa bahari Kuu vizuri tunaweza tukapata fedha nyingi kuliko kwenye dhahabu na almasi; hili sasa tulifanyie bidii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo napenda kulishauri Bunge letu na Serikali kwa ujumla; kwa wale wenzetu ambao wamefanikiwa katika masuala haya, Serikali isione tabu katika kutumia fedha, kwa mfano ama kupeleka Waheshimiwa Wabunge kwenda kujifunza ama kupeleka wataalam wetu wakajifunze. Wanafarsafa wanasema, ukitaka kula lazima uliwe, kwa hiyo na sisi tuhakikishe kwamba tunapeleka watu wetu kwa kutumia fedha zetu ili tuweze kukusanya mapato vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini nikija kwenye suala hili la umeme, nimeona hapa kwenye huu mkataba wa *Solar* kuna mambo mengi ambayo sisi Tanzania tunaweza kusema sio kisiwa. Wenzetu wengi wamefanikiwa kutokana na umeme wa *solar* kwa sababu kwanza ni umeme wa bei rahisi, lakini

hata bidhaa za viwandani zinashuka bei kwasababu gharama za uzalishaji zinakuwa ni ndogo na umeme wa *solar* ndio umeme wa bei rahisi zaidi duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, niseme tu kwamba Serikali isisite kutoa elimu hii ya manufaa ya umeme wa *solar* kwa sababu wengine wanatia dosari, wanasema umeme wa *solar* kama ni *fridge* la futi tano haligandishi vizuri, umeme wa *solar* kwenye nyumba hauna nguvu vizuri, sijui kwenye *welding* haufanyi vizuri; kumbe tumeona baadhi ya nchi wanautumia huu umeme katika kila jambo.

Mheshimiwa Spika, nilibahatika kwenda Denmark, tukakuta wenzetu wanautumia umeme wa *solar,* wametega kila maeneo wameweka *panel* zinachukua umeme unakwenda magerezani, viwandani, shule, na kwenye vyuo. Wenzetu wananufaika, sasa sisi sasa kwa hili naomba na sisi tusibaki nyuma, tutumie umeme wa *solar* kuendeleza maslahi ya wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine, kuna mwekezaji mmoja kule Kigoma, yeye huyu anazalisha umeme wa *megawatt* tano; kuna sehemu inaitwa Kisenzi. Sasa *TANESCO* watu kama hawa iwasogeze karibu, iwe inasaidia, kwa sababu *TANESCO* haiwezi ikasambaza umeme nchi nzima bila kuwa na washirika. Sasa watu kama hawa nao watumike kuwasaidia maeneo ya vijijini kuwasambazia wananchi wetu umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho niseme tu, napo hata hapa katika masuala ya umeme wa *solar* tujitahidi sasa katika vyuo vyetu kama *VETA*, katika mafundi wetu hawa wanaotumia umeme huu wa *TANESCO,* nao wapewe elimu kwa ajili ya kujifunza kutumia umeme wa *solar* ili kuepusha gharama za umeme, na ili kuyafanya maisha ya wananchi wetu yawe rahisi zaidi. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mbarouk, Mheshimiwa Ally Saleh atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Anna Kajumulo Tibaijuka.

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Mimi nitabaki katika hili suala la *solar power agreement* ambayo imesainiwa miaka michache tuliyopita, lakini nimefurahi kwamba nchi yangu ilikuwa katika nchi za mwanzo na leo hata muda haujapita sana linaletwa Bungeni turidhie. Kwa kweli tumekuwa tukipitwa na maazimio mengi ya kimataifa lakini hili limekuja haraka sana. Nitafurahi *spirit* hii ya kukipitisha maazimio haraka inavyowezekana ikiendelea.

Mheshimiwa Spika, la pili ni kwamba jana na juzi nilisema kwamba Mungu ameiweka Tanzania kwa makusudi yake. Katika mfano huu wa *solar* ni kwamba ametuweka katika maeneo kati ya *tropical of cancer* na *tropical of Capricorn* ambayo inatajwa katika mkataba huo na katikati inapita IKweta. Kwa maana tumewekwa kwenye *sunshine state* kama inavyotajwa, na kama anavyosema Narendra Modi wa India. Kwamba tuko katika eneo ambalo jua ni 12 *seven*, lakini tunalitumiaje? Jua liko wakati wote na liko takriban nchi nzima; sasa tunalitumiaje ndiyo muhimu; kwa hivyo tumekuwa katika pahala ambapo sasa hivi tuna fursa nzuri sana. Nchi ambazo jua si wakati wote kama Ujerumani bado ni katika nchi 10 duniani ambazo zinaongoza kwa *solar*.

Mheshimiwa Spika, nchi kama ya *Norway* jua ambalo si siku zote lakini bado inaongoza kwa *solar,* sembuse sisi ambapo asubuhi mpaka jioni jua.

Mheshimiwa Spika, kikundi hiki cha *International Solar Power Agreement* sasa hivi ni kundi kubwa la pili la nchi za Kimataifa zinazokutana baada ya Umoja wa Mataifa. Kwa hivyo ni eneo ambalo linakua haraka sana na nafikiri takwimu za mwisho labda kama *signatories* kama 121 tayari mpaka hivi sasa, kwa hivyo ni kundi kubwa. Hata hivyo si kundi kubwa kwa jina tu, ni kundi kubwa kwa dhamira; kwa sababu kuna mipango mingi ya kufanya ili kuiokoa dunia, linalofanywa hapa ni kujaribu kuiokoa dunia. Ndiyo maana wanataka tufanye kila njia ili tuache kutumia *fossil energy* badala yake tutumie *energy* ambayo ni *renewable*, kwa hivyo sisi tusiiache fursa hii.

Mheshimiwa Spika, nasema tusiiache kwa sababu nina *experience,* kwamba labda pengine kwa hii sasa kutakuwa na mabadiliko; na ningependa Mheshimiwa Waziri wa Uwekezaji anisikilize katika hili.

Mheshimiwa Spika, na narudia tena hapa Bungeni niwahi kupata ofa ya wawekezaji ambao wako tayari kuwekeza *three billion dollar's* kwa ajili ya *three thousands* megawati za umeme nikataabishwa, nikasumbuliwa mpaka yule muwekezaji akakata tamaa. Hivi sasa nasema, pengine Mheshimiwa Waziri ananisikia, kwamba nina *offer* nyingine ya mtu ambaye yuko tayari kuwekeza vituo zaidi ya 50 vya *solar* kwa ajili ya magari, kwa ajili ya vyombo vya umeme, kwa pesa zake; *I mean* ni *self financing*. Kwa hiyo kama Serikali watakuwa tayari huu ndio mwanzo mzuri, tunaanza kidogo kidogo ku-*phase* kwenye *petroleum* tunaingia katika vitu vingine. Kwa hiyo ningependa baadaye nikae nizungumze na Mheshimiwa Waziri tuone tatafanya kitu gani.

Mheshimiwa Spika, lakini pia ni njia nzuri ya *energy mix* tunalalamika kila siku juu ya *energy mix.* Wengine tulisema sana hapa juu ya umeme wa Julius Nyerere; lakini kusema kweli tulikuwa na ushindani. Wengine tunasema kwamba umeme wa *solar* ni rahisi zaidi, wengine wanasema umeme wa maji rahisi zaidi, lakini namna ya uwekezaji wenyewe. Sasa hivi kumepatakana *solution,* hawa walioko mbele, kwa mfano India, wao wametenga *three fifty billion dollar's* kwa ajili ya kuzisaidia nchi kufanya kazi hii. Pia *World Bank* wao wanatarajia kuhamasisha uwekezaji wa takriban bilioni 1000 mpaka kufikia 2030 ili nchi zote ambazo zina fursa zipo katika *sunshine area* ziweze kunufaika. Kwa hiyo sisi tusikae nyuma sasa maadam tulishaingia katika uwanachama huu na tuna fursa.

Mheshimiwa Spika, Dodoma peke yake hapa ikitumika, maeneo ambayo hayafai kwa kilimo, maeneo ambayo hayaoti miti basi tunaweza tukatoa megawati kwa mamia kabisa sembuse nchi nzima, kwa hiyo tutumie fursa hiyo kwa vizuri.

Mheshimiwa Spika, lakini pia sasa hivi kuna nchi; kwa mgano Venezuela, ambazo tayari zinaweza kufikia *100 percent* sasa ya mahitaji yao. Kwa hivyo sisi tusiona kwamba Julius Nyerere kama tumefika kwa zile megawati 2000 na ushehe. Bado nchi hii kama tunataka kweli kwenda kwenye viwanda tuondokane na dhana, kama alivyosema Mheshimiwa Mbarouk, ya kuona umeme wa jua si umeme kitu. Umeme wa jua ni umeme kama umeme mwingine na unaweza kuuzalisha viwandani na unaweza ukatumika sehemu nyingine nyingi hata hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, *imagine* hapa jua linalopiga kutwa nzima katika paa la nyumba hii na namna paa yaliyopo humu ndani kiasi ambacho pengine tukiweka *solar* tu humu ndani ya Bunge tunaweza tukakoa mamilioni ya fedha. Kama vile ambavyo tumeokoa karatasi kwa kwenda kwenye *tablets* na huku tunaweza tukaokoa pesa tukatumia *renewable energy* lakini pia tukaokoa fedha nyingi kwa kuitandika *solar power* eneo lote la Bunge au eneo lolote lingine ambalo umeme wake utakuja mpaka Bungeni. Kwa hiyo mimi nasema katika hili Tanzania tusikae nyuma...

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Saleh nilitaka kukubaliana na wewe katika eneo la Bunge kutumia *solar powe*r. Niliwahai kutembelea Bunge la Israel wanatumia 1005 umeme wao kwenye Bunge la Israel *solar power*. Endelea tu Mheshimiwa. *(Makofi)*

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Spika, fahari kubwa kukubaliwa wazo langu. Kwa hivyo mimi nafikiri Bunge lioneshe mfano kwamba hiki kinawezekana na taasisi za Kiserikalia kwa mfano Mji wetu wa Mtumba utandikwe *solar,* inawezekana kufanya, ili Serikali iwe mfano na ili tuwe tunaweza kujiendesha wenyewe kidogo mpaka hapo ambapo wakubwa wa dunia watakapotuona na kuweka katika maeneo haya; kwa sababu umeme utaendelea kuhitajika kwa sababu tunasema tunataka Tanzania ya viwanda ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana nilishakutaja Mheshimiwa Anna Tibaijuka karibu nisikie mchango wako.

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Mimi pia naomba niungane na waliotangulia kuwapongezeni Waheshimiwa Mawaziri wote wawili waliotuletea mikataba hii ya Kimataifa kusudi na sisi tuweze kuiridhia. Katika uchangiaji wangu, ni jambo zuri na wote kama ilivyosema, hasa ule mkataba wa *FAO,* nataka kusema kwamba ni mkataba umekuwepo kwa muda mrefu mimi nimeushuhudia wakifanyiwa kazi bado niko huko Umoja wa Mataifa. Sasa niseme kwamba labda ni muhimu sana kusema, kwamba kwa kuwa tumechelewa kidogo kuridhia mikataba hii mimi nimefarijika sana kuona kwamba katika Bunge hili Tukufu inaonekana pande zote tunakubaliana kwamba turidhie, kwa hiyo naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa katika kuridhia hilo na Serikali katika kutupa taarifa nina mambo mawili ya kusema. Kwanza naomba Mheshimiwa Waziri wetu wa Mifugo na Uvuvi ajaribu kuangalia kwa wenzake hali tuliyo nayo huko katika bahari kuu. Maana ninachofahamu mimi ni kwamba sisi Tanzania tuna haki ya kupewa eneo zaidi katika bahari kuu ambayo bado tunalidai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kazi hiyo imekwama kule Umoja wa Mataifa na nadhani sasa Mheshimiwa Waziri Mpina wewe ndiwe mhamasishaji, wewe ndiwe mwenye samaki, wewe ndiwe mwenye viumbe kule baharini. Nadhani ni muhimu kuangalia mchakato wa kudai *extended continental shelf* ya Tanzania umefikia wapi. Kazi naifahamu kwa sababu mwaka 2012 nikiwa Waziri wa Ardhi niliwakilisha Umoja wa Mataifa New York kwenye kamati husika ya *International Convention on the Taw of The Sea,* kudai eneo letu. Sasa tusipoangalia tunaweza tukaridhia mikataba hii lakini kuna sheria zinazotawala utawala wa maji duniani, *International Law of the Sea.* Labda ingekuwa ni vizuri kulijulisha Bunge hili mchakato huo umefikia wapi.

Mheshimiwa Spika, labda kwa kufafanua zaidi; ni kwamba tumesikia hapa, na kamati imezungumza vizuri, kwamba *exclusive economic zone* ni nautical mile 200 unapewa baada ya maji yako *(territorial waters).* Lakini Tanzania kwa sababu ya mito yetu, hususan Mito ya Rufiji, Pangani, Wami; ndiyo inalisha viumbe baharibini. Kwa sababu hiyo tunastahili kupewa *nautical mile* 150 zaidi ndani ya bahari.

Mheshimiwa Spika, sasa hiyo ni hazina kubwa ya Taifa, na ninadhani kwamba Mheshimiwa Waziri wa Uvuvi aangalie na wenzake wanaohusika hususani Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje na Waziri wa Ardhi kwamba hatupotezi hazina hiyo, kwa sababu unapopeleka maombi Umoja wa Mataifa kuna muda usipofatilia unaweza ukaondolewa kwenye orodha. Kwa hiy ni jambo ambalo nimeona kwamba niliseme na huu ni wakati wake.

Mheshimiwa Spika, tunaporidhia mkataba huu pia tujue utawala wa bahari duniani na tutaweza kudhibiti huo uvuvi haramu katika bahari zetu. Suala la uvuvi haramu nadhani ni suala ambalo wote tunakubaliana kwamba ni suala hatari lakini pia ni suala la teknolojia na sisi kama nchi inayoendelea wakati mwingine tufaidike kwa kuomba misaada pale tunapohitaji. Kwa sababu uwezo pia wa kudhibiti hizi meli kubwa, gharama inayohitajika na teknolojia inayohitajika unaweza kukuta kwamba hatuna. Tukisharidhia mkataba kama huu na sisi basi; na imesemwa na wengine; tunaweza pia kuomba msaada wa wataalamu, vifaa na fedha za kutusaidia kuhakikisha kwamba hapa kwenye bahari yetu kuu si inakuwa shamba la bibi, kwamba kila mtu anafanya anachotaka na hasa uchafuzi wa sumu zinazotupwa katika bahari yetu.

Mheshimiwa Spika, ilifikia kuna mahali pale wala siendi mbali pale Kawe Beach waliwahi kutupa magunia ya sumu hatari kwa hiyo unakuta vitu kama hivi wanaendelea kwa sababu hatujajua...

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Spika, taarifa

## T A A R I F A

**SPIKA:** Ndio taarifa tafadhali Mheshimiwa Zungu

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Spika, naomba kumpa taarifa Mheshimiwa Profesa. Kwanza nimpongeze kwa kazi kubwa aliyoifanya ya kuhakikisha *extended ya continental shelf* ya Tanzania na kupata hizo km 150. Juzi mimi nilikuwa umoja wa mataifa tumelifatilia hili suala tuko katika namba 59 ya shauri la Umoja wa Mataifa na limekaa vizuri. Tatizo vikao vya Umoja wa Mataifa havikai kutokana nchi wanachama ambao wako kwenye *commission* ile wanatakiwa walipiwe gharama zao za kuhudhuria vikao na nchi zao kwa vile nchi zao hazilipi gharama ile *commission* haikai. Kwa kutokukaa *justice delayed justice denied* tunakosa haki yetu.

Mheshimiwa Spika, vilevile Kenya nao wana shauri na Somalia na shauri lile linaweza likatuathiri kama Somalia wakishinda kutokana na mpaka kati ya Kenya na Pemba. Kwa hiyo nilitaka nimpe taarifa tu kwamba suala liko vizuri Serikali wanalifuatilia na kamati tuko karibu nao kuhakikisha haki ya Tanzania inapatikana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Asante sana ni kweli Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje alikuwa UN kwenye *General Assembly* akifatana na Waziri wa Mambo ya Nje hivi juzi tu. Mheshimiwa Profesa Tibaijuka endelea na mchango wako.

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana kwa Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nchi za Nje na nimefarijika kusikia kwamba suala hilo linafatiliwa ni muhimu sana. Sasa nikirudi kwenye uwezo wetu wa kutekeleza hii mikataba tukishasaini. Sisi ni nchi inayoendelea, bado tuna haki ya kupata msaada wa hao wenzetu waliotangulia. Kwa kweli wenyewe kwa sababu ya teknolojia zao ndio wana uwezo wa kuchafua na kutumia hizi mbinu haramu ambazo zinakuwa na athari kubwa. Kwa hiyo tusibaki nyuma, Mheshimiwa Waziri usibaki nyuma katika kuweka sasa ufatiliaji ambao ni chanya. Kuna ufatiliaji

mwingine ni urasimu tu mtu hana vifaa atakaa anasumbua meli anaweza akaleta kero.

Mheshimiwa Spika, mimi nafikiria kwamba tufanye kazi kwa weledi kwa sababu tunaposema tuweke watu wa kudhibiti, je, wana uwezo wa kudhibiti? Wanakuja kufanya juhudi au kama Mwalimu Nyerere alivyosema, kwamba ni juhudi bila maarifa. Suala hili ni muhimu sana hasa katika vyombo tunavyojiwekea kudhibiti.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili nirudi sasa kwa haraka kwenye suala la mkataba wa umeme wa jua. Umeme wa *solar* huu na umeme wa jua ni kitu kizuri sana. Naomba kusema kwamba sisi kitu kimoja kinachotukwaza kama taifa linaloendelea na kama taifa lenye vijana na vijana ambao hawana ajira ni kushindwa kuweka utaratibu kwa vijana kuunda kampuni za *solar* zitakazoweza kuleta teknolojia katika nyumba na kutoa huduma.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, nirudi sasa kwa haraka kwenye suala la mkataba wa umeme wa jua. Umeme wa *solar* huu na umeme wa jua ni kitu kizuri sana. Naomba kusema kwamba lakini sisi kitu kimoja kinachotukwaza kama Taifa linaloendelea na kama Taifa lenye vijana na vijana ambao hawana ajira ni kule kushindwa kuweka utaratibu kwa vijana kuunda makampuni ya solar yatakayoweza kuleta teknolojia katika majumba na kutoa huduma. Kutegemea *TANESCO* bila kutumia *solar* ni kutwanga maji kwenye kinu kwa sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, nafikiri ingekuwa ni bora Mheshimiwa Waziri akatueleza sasa anavyojaribu kusaidia vijana wetu hawa ambao tunawaambia wajiajiri wakati sisi tumeajiriwa, lakini hatuwawekei utaratibu wa kwa mfano kuunda kampuni mahususi ambazo zitaweza kueneza umeme wa *solar;* vijana wanamaliza *Engineering* wapo kule mijini hawana kazi.

Mheshimiwa Spika, nadhani tunaposaini mkataba kama huu ni fursa muafaka pia kuwapatia teknolojia, lakini

na huduma inayotakiwa maana yake unaposambaza kitu kipya kina ukakasi, ukiwaambia watu tukufungie *solar* yeye anaona nyaya za *TANESCO* zinapita juu anaona unamsumbua kama unamfanyia shamba la majaribio, kwa hiyo mtu anataka kitu ambacho ana uzoefu nacho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tukiwa na vijana ambao wanaweka makampuni ya kuhakikisha kwamba yanapata soko, sasa kazi yetu nini? Kazi yetu ni halmashauri, kuweka sehemu ili ziwape masoko inaitwa *public procurement* ambayo ni lazima iwezeshe *dissemination* ya teknolojia, teknolojia mpya haiwezi kusambaa kama haina *Public Procurement Policy* inayoi-*support* yaani kwamba kule kununua kwa upendeleo kabisa kampuni za vijana, ndiyo tutaweza kuondokana na hii ngonjera ya umeme wa *solar* umeme wa *solar*, lakini watu hawapo tayari kuwa kwenye majaribio, tuwawekee uwezeshaji.

Mheshimiwa Spika, huo ndiyo mchango wangu, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Profesa. Sasa Waheshimiwa Wabunge ili twende vizuri tuwaruhusu sasa Waheshimiwa Mawaziri waweze kupitia michango yetu mbalimbali na tumekubaliana kila mmoja atasoma robo saa ili tuweze kumaliza asubuhi mambo yote ili jioni Waheshimiwa Wabunge muweze kufanya mambo mengine muhimu zaidi.

Sasa kama tulivyowasilisha mwanzoni naomba nimwite Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Luhaga Mpina ili aweze kupitia michango mbalimbali ya Waheshimiwa Wabunge na uzuri wa mambo haya mawili kwa kweli Wabunge wameunga mkono sana na wametoa ushauri wa namna gani Serikali itekeleze. Mheshimiwa Waziri Karibu sana.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana kwa nafasi uliyonipa tena, lakini pia nimshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge wa Kilimo Mifugo na Maji, lakini na Msemaji wa Kambi ya Upinzani

anayesimamia masuala ya Mifugo na Uvuvi wa hotuba zao nzuri sana walizozihutubia hapa Bungeni na vile vile michango ya Waheshimiwa Wabunge wote. Nichukue nafasi hii kuwashukuru sana kwa mchango ambayo mliyoitoa na sisi tumenufaika sana na michango yenu mliyoitoa.

Mheshimiwa Spika, Azimio letu hii la *PSMA,* bahati nzuri sana Wabunge wote waliopata nafasi wameunga mkono na wametoa ushauri. Kwa ujumla kwa masaa na dakika ulizonipa, ni ngumu sana kupitia maswali ya Waheshimiwa Wabunge, lakini pia na ushauri walioutoa, lakini itoshe kusema kwamba ushauri wote ambao Waheshimiwa Wabunge wametupatia tumeuzingatia na utatusaidia sana katika utekelezaji wa majukumu yetu ya maeneo haya ya uvuvi wa bahari kuu.

Mheshimiwa Spika, la kwanza, labda ambalo Wabunge wameliongelea sana na limezungumzwa miaka mingi suala la Bandari ya Uvuvi, nataka niwaambie Wabunge kwamba hii Serikali ya Awamu ya Tano inaenda kutanzua huu mtego wa miaka mingi ambao umekuwa kilio kikubwa kwa Taifa. Bandari hatua ambayo tumefikia mpaka sasa hivi tuliliambia Bunge lako wakati wa Bajeti kwamba, tunafanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya kujenga bandari ya uvuvi hapa nchini. Nataka nilitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Mshauri Mtaalam Mwelekezi wa kampuni ya Italy amekamilisha *report* yake ya upembuzi yakinifu.

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa hivi maeneo yaliyopendekezwa kwa ajili ya kuijenga hiyo bandari ni Bagamoyo, Kilwa Masoko na Lindi. Kwa hiyo, kati ya hayo maeneo hayo tutachagua sasa eneo imebaki sasa kwenye maamuzi ya ku-*decide* kama Serikali kwamba tutajenga bandari ya uvuvi kati ya maeneo haya mawili. Kama hiyo haitoshi Serikali tayari iko kwenye hatua za mwisho kabisa na Serikali ya Jamhuri ya Korea Kusini kwa ajili ya kuanza ujenzi wa bandari ya uvuvi hapa nchini. Kwa hiyo ninachotaka kusema kwa sasa ni kwamba kilichobaki kwa sasa hivi ni maamuzi ya bandari ijengwe wapi na baada ya hapo katika mwezi huu jambo hili litaamuliwa na mwezi unaofuata wa

Desemba ni matarajio kwamba Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Korea zitasaini makubaliano tayari kwa kuanza bandari ya uvuvi wa bahari kuu.

Mheshimiwa Spika, swali la pili lililoulizwa, ni bandari zinazotambuliwa ni bandari zipi zinazotambuliwa sasa ambazo zitahusika huu Mkataba wa *PSMA*. Bandari zinazotambuliwa na ambazo zimeingia na ambazo zitahusika na *PSMA* ni Bandari ya Dar es Salaam kwa sasa, Bandari ya Zanzibar, Bandari ya Mtwara na Bandari ya Tanga, hizi ndizo zitakazohusika katika utekelezaji wa makubaliano yetu na Mkataba wetu huu wa *PSMA*.

Mheshimiwa Spika, suala lingine lililozungumzwa hapa na Waheshimiwa Wabunge ni suala la udhibiti wa uvuvi haramu kwenye eneo la *high seas* kwamba hivi sasa hakuna udhibiti na hata hii *PSMA* tunayoazimia haifiki katika eneo hilo la *high seas*. Nataka nitoe taarifa kwamba tayari *UN* wameanza kuandaa *legal instruments* za usimamizi za *resource* katika *high seas,* yaani *biodiversity beyond national jurisdiction,* tayari inaandaliwa na mara hii *instrument* itakapokuwa imekamilika, sasa mfumo huu wa *PSMA* utaenda mpaka *high seas*. Kwa hiyo, huu ulinzi wa rasilimali wale waliokuwa wanafanya uvuvi haramu kwenye maeneo hayo hawatapata *excuse* tena.

Mheshimiwa Spika, suala la marekebisho ya Sheria ya Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu ya mwaka 1968 pamoja na kanuni zake za mwaka 2007 ambazo zilifanyiwa marekebisho mwaka 2016, hivi sasa tuko kwenye marekebisho ya Sheria yenyewe pamoja na kanuni zenyewe. Katika marekebisho hayo eneo hili la *PSMA* ambalo tunalozungumza litaingizwa, lakini pia tutazingatia maombi mbalimbali ambayo yatawezesha ruhusa ya uvuvi yaani *authorization to fish* kwa meli zenye bendera ya Tanzania kuweza kuvua katika maeneo ya *high seas* na *EEZ* za nchi nyingine. Kwa hiyo katika hizi kanuni ambazo kanuni na sheria ambazo tunazifanyia mapitio kwa sasa na zingine zitaingia Januari kwenye Bunge lako Tukufu, tunawaahidi Waheshimiwa

Wabunge kwamba maboresho mengi yatakayohusika na Kanuni ya uvuvi wa bahari kuu yatazingatiwa katika haya marekebisho ambayo tunafanya kwa sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambao Waheshimiwa Wabunge wamelizungumza ni suala la eneo la kitutia Mafia kwamba ni muhimu sana kwa mazalia ya samaki, lakini halilindwi ipasavyo, nataka nitoe taarifa kwamba hili eneo linalindwa ipasavyo na liko chini la *MPRU*, linalindwa uvuvi hauruhusiwi eneo hilo kwa sababu ni eneo ambalo lina mazalia ya samaki, kwa hiyo eneo letu hili tunalilinda na tunatambua umuhimu wake kwamba ni eneo mahususi sana kwa ajili ya mazalia ya samaki.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge hapa walizungumza sana na wakaomba sana kwamba hii kuondolewa kwa tozo ya dola za Kimarekani 0.4 kwa kilo ya samaki inayovuliwa na kusafirishwa nje ya nchi hasa na meli hizi za *foreign vehicles* kutoka nje ya nchi zinazofanya uvuvi katika ukanda wetu wa uchumi wa uvuvi wa bahari kuu. Waheshimiwa Wabunge walisema na waliomba sana Serikali kwa muda iondoe tozo hii ili kuwezesha uvuvi uweze kufanyika kwa sababu meli zilizokuwa zinakuja kuvua zilishindwa kabisa kuvua baada ya kuweka hii tozo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusema kwamba na kama wewenyewe walivyosema ni kweli kabisa sisi Serikali tumeridhia kwa kipindi hiki cha mwaka mmoja wakati tunatafakari njia bora ya kunufaika na rasilimali zetu zilizoko katika ukanda wa bahari kuu ili tuweze kunufaika kwa hiyo, hii tozo tumeiondoa na Waheshimiwa Wabunge tayari tumeshasaini nadhani *GN* itatoka muda wowote, lakini wavuvi wetu wako ni rurksa sasa hivi kuvua na kwamba 0.4 haitatozwa ila watatozwa zile gharama zingine ikiwemo kulipia leseni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ilikuwa ni suala la kuwekeza kikamilifu katika utafiti; ni kweli kabisa kwamba hakuna mtu anayeweza kukubali ku-*risk investment* yake katika eneo ambalo halina utafiti. Hakuna Taifa ambalo

linaweza kuwa na mipango mizuri kama hakuna taarifa za kiutafiti za kutosha kwenye eneo husika na sisi kama Serikali tunakubaliana na ushauri wa Waheshimiwa Wabunge na wamekuwa wakitushauri mara kwa mara na kwa sasa tumeanza. Kwa mfano sasa hivi hii Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu *(DSFA)*, tumeshaipatia fedha kupitia Mradi wa *SWIOFISH.* Jumla ya shilingi milioni 457.7 ambazo hizi tunaanza sasa kufanya utafiti wa kujua rasilimali zetu zilizoko katika eneo la uvuvi wa bahari kuu.

Mheshimiwa Spika, tutafanya hivyo kuhakikisha kwamba zipatikane taarifa zote za uhakika ambazo wananchi wetu wanazitaka, wawekezaji wetu wanazitaka ili sasa tuweze kuhakikisha tunaweka mipango madhubuti yenye taarifa za uhakika za kiutafiti juu yake na sisi tunaamini kwamba tunazo *resources* katika eneo letu la *EEZ* ambazo haziko maeneo mengine yote na kwamba pia sisi katika usimamizi wa rasilimali na katika mapambano juu ya uchafuzi wa bahari, pamoja na usimamizi wa uvuvi haramu tunafanya vizuri Waheshimiwa Wabunge, sisi kimataifa eneo letu linatambulika kuwa eneo ambalo bado ni *clean,* maeneo mengi katika sehemu nyingi duniani watu wameshachafua sana mazingira, lakini maendeleo haya ...

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naongeza nusu saa ili tuweze kumaliza mambo yetu. Haya Mheshimiwa Waziri malizia.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, nataka kusema kwamba nchi yetu inazidi kupata sifa kubwa kimataifa katika usimamizi wa rasilimali hizi na tulivunja rekodi kubwa sana tulipokamata ile meli maarufu inaitwa meli ya Magufuli, lakini baadaye majuzi, tukaja kukakamata meli ya *Buhanaga One*, sisemi ya Mpina, lakini hiyo ni ya *Buhanaga One*. Ile meli tulipoikamata tumepata sifa kubwa sana duniani katika kuhakikisha kutuma *message* kubwa sana ya ulinzi wa rasilimali hizi za Taifa.

Mheshimiwa Spika, nataka niwaambie Waheshimiwa tuko vizuri sana tunapongezwa kila kona kwa jinsi ambavyo

tumesimama kidedea katika kuhakikisha kwamba hizi rasilimali zinalindwa sana. Hivi majuzi kuna baadhi ya viongozi tuliwaambia wanaotaka kutumia rasilimali hizi za Taifa kujipa sifa za ziada katika kuchaguliwa, kiongozi anashindwa kutaja sifa zake za kuchaguliwa anaanza kuwaambia wananchi wakafanye uvuvi haramu au anaanza kusitisha zoezi la doria linalolinda rasilimali kwamba kwa sababu hiki ni kipindi cha uchaguzi. Tunazidi kusisitiza Watanzania wasimamie sheria rasilimali hizi za uvuvi zitalindwa muda wote, bila kuzingatia majira ya mvua au ya jua, uchaguzi hauwezi kuwa na mahusiano na ulinzi wa rasilimali hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka kusema kwamba viongozi wote wanaohusika wahakikishe kwamba na leo tunaunga mkono hili Azimio hii kubwa la dunia ambalo litaleta mchango mkubwa katika kusimamia kwa dhati hizi rasilimali tulizonazo ili tuendelee kuzivua kwa uendelevu kwa leo na siku zijazo.

Mheshimiwa Spika, sitaki niende nje sana ya muda huu ulionipa, lakini nizungumzie suala la *by-catch,* suala hili tunaangalia changamoto zake katika haya marekebisho ya kanuni ambayo tunayazungumza ili kuweka utulivu na kuondoa malalamiko yaliyoko hivi sasa ya *by-catch.*

Mheshimiwa Spika, mwisho suala la ku-*extend* ile *continental shelf* ambayo imezungumzwa hapa, nimshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje ametoa ufafanuzi mzuri, lakini na Mheshimiwa aliyezungumzia hoja hii naye alizungumza vizuri. Sisi kama Serikali tunaendelea kufuatilia kwa karibu kuhakikisha kwamba tunafikia haya malengo yetu.

Mheshimiwa Spika, nalishukuru sana tena Bunge lako katika kuunga mkono hii hoja iliyoko mbele yetu kwa sasa baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, hoja imetolewa na imeungwa mkono. Tunakushukuru sana kwa uhitimishaji kuwa hoja hiyo.

Sasa Waheshimiwa Wabunge naomba niwahoji kuusiana na Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa *FAO* wa Kuzuia Uvuvi Haramu Kupitia Bandari za Nchi Wanachama.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**SPIKA:** Wote wameafiki. Nawashukuruni sana Waheshimiwa Wabunge, tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri, tunaishukuru sana Serikali kwa ujumla wake pamoja na wataalam wetu kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kazi nzuri ambayo mmekuwa mkifanya. Tunawaunga mkono tuendelee na doria, habari ya kufuata sheria haina cha uchaguzi wala nini na wananchi wetu wajue kabisa ili rasilimali hizi ziendelee kuwepo, lazima tufuate taratibu na sharia. Bahati mbaya ni rasilimali ambazo zikitoweka, zimetoweka jumla zilizo nyingi kwa hiyo, ni lazima tuzilinde na tuunge mkono taratibu tulizojiwekea, kwa sababu sheria zinapita kwenye Bunge hili hili, sasa ikionekana Mbunge unapinga sheria huko mtaani kwenye jimbo lako na kadhalika ni kitu cha ajabu sana. Siasa isiwe mahali pa kutia moyo wananchi katika kuharibu rasilimali zetu.

Tunawashukuruni sana, tunaamini utekelezaji wa Azimio hili utakwenda vizuri na lile suala ambalo umetuambia la kwamba huenda bandari ya uvuvi ikaanza kujengwa haraka sana hivi karibuni, kati ya kule Kilwa au Bagamoyo nadhani Bagamoyo labda ni Mbegani au *somewhere*, ni jambo jema sana sana na litatusaidia sana katika kuongeza mapato yetu yanayotokana na uvuvi wa bahari kuu, ahsanteni sana.

Sasa nimwite Waziri wa Nishati ili na yeye aweze kuhitimisha hoja yake kwa muda usiozidi robo saa. Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Dkt. Kalemani karibu sana.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, nami napenda nitoe shukrani kwako mwenyewe pamoja na Makatibu wanaokusaidia katika meza wakati wa kuliongoza Bunge hili

Tukufu wakati wa mawasilisho Azimio hili muhimu. Niendelee kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge na kwa kuanzia Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Nishati ya Madini kwa wasilisho lake nzuri ambalo kimsingi limeunga mkono karibu kwa asilimia mia moja. Pia niwapongeze sana Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamechangia na kwa kiasi kikubwa wametoa mapendekezo lakini kimsingi wameridhia kwamba Azimio hili liungwe mkono.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo machache, yako mambo mahususi ambayo yamejitokeza ambayo Waheshimiwa Wabunge wangependa kupata uhakika wa ufafanuzi wa kina. Baadhi ya mambo ambayo ni ya msingi sana ambayo wananchi wangependa kusikia kutoka kwenye Bunge letu Tukufu ni utashi wa Serikali. Napenda niliambie Bunge lako Tukufu kwamba utashi wa Serikali wa kutekeleza Azimio hili ni mkubwa sana na ndiyo maana mmeridhia katika kikao chako hivi leo na sisi kama Serikali baada ya Azimio kuridhiwa na Bunge sisi ni kwenda kutekeleza mara moja. Kwa hiyo utashi wa kiserikali upo, niwaondoe wasiwasi Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wanaotusikiliza.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na matumizi ya *solar*, baadhi ya vyanzo vya nishati hapa nchini ni pamoja na rasilimali ya *solar*. Tunavyo vyanzo vingi sana vya kuzalisha umeme, kama ambavyo mnafahamu tuna vyanzo vya rasilimali gesi, tuna vyanzo vya rasilimali maji, makaa ya mawe, upepo na kadhalika, lakini pia *solar*.

Mheshimiwa Spika, kulingana na tafiti ambazo zimeshafanywa, na nimeshukuru sana baadhi ya Waheshimiwa Wabunge kutaka kujua mikakati. Mkakati wa kwanza uliokwishafanyika ni kufanya utafiti wa kina na kubaini uwezo uliopo wa kuzalisha nishati ya *solar.* Tafiti zilizofanywa mpaka kuishia mwaka 2015 zinaonesha Tanzania tunaweza tukazalisha umeme wa *solar* kufikia mpaka megawati 1,000.

Mheshimiwa Spika, na bahati nzuri sana, Tanzania tuna *potential* kubwa ya mionzi ya jua. *Potential* tuliyonayo

sisi ni *kilowatt-hours* 4 mpaka 7 kwa mita za mraba kwa siku ambapo kipimo cha kimataifa ni *kilowatt-hours* 3.97, kwa hiyo tuko juu sana kwa maana ya rasilimali ya jua tuliyonayo. Lakini katika mwaka pia Tanzania tunaweza tukapata mionzi ya jua mpaka takribani ya saa 2800 mpaka saa 3500 kwa mwaka kwa hiyo vyanzo vya kuzalisha umeme wa *solar* ni vingi.

Mheshimiwa Spika, nilitaka kutoa taarifa hiyo ili kuwapa uhakika kwamba baada ya azimio hili kupita na matarajio tuliyonayo ni kwamba Serikali tunakwenda kufanikiwa kwa kiasi kikubwa kuwepo na umeme wa *solar* hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine limeelezwa kwamba pengine ni muhimu kutekeleza mradi huu kuliko Bwawa la Julius Nyerere. Nataka niseme mkakati wa Serikali ni kuzalisha umeme mchanganyiko kwa kutumia rasilimali zote tulizonazo. Ni kweli zipo tofauti kutoka chanzo kimoja kwenda kingine lakini nataka niseme, chanzo cha kwanza kabisa kwa unafuu katika kuzalisha umeme ni umeme wa maji ambao unatumia shilingi 36 kuzalisha uniti moja ya umeme. (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na umeme wa pili unaofuata kwa unafuu ni huu umeme wa *solar* ambao wenyewe utazalisha uniti moja kwa Shilingi ya Tanzania 103.28, kwa hiyo bado nao ni wa nafuu. Lakini pamoja na hayo bado tunaona ni jambo la busara kuzalisha umeme kwa kutumia vyanzo mchanganyiko ndiyo maana tunaendelea kuzalisha pia vyanzo vingine.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tunasema, pamoja na mambo mengine, unapotumia umeme wa *solar* unakabiliana kwa hatua ya juu sana na uharibifu wa mazingira, lakini pia usimamizi wake nao ni mwepesi na kwa sababu vyanzo tunavyo, rasilimali ya kutosha, na tumejipanga kwa ajili ya kutekeleza jambo hilo tunadhani azimio hili likipitia itachangia kwa kiwango kikubwa sana kuzalisha umeme wa *solar* na kuingiza kwenye Gridi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge, ni kweli kwa sasa katika Gridi ya Taifa hatujaweza kuunganisha umeme wa *solar* ingawa tunao umeme wa *off-grid* katika maeneo mtambuka nje na Gridi ya Taifa chini ya *megawatt* tano. Kwa hiyo mkakati wetu ni kuzalisha walau *megawatt* 1,000 za umeme wa *solar* nazo ziingie kwenye Gridi ya Taifa, na ni kupitia azimio hili likipitishwa na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, na ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo ni muda mwafaka sana sasa kukubali azimio hili ili tuingize umeme wa *solar* katika Gridi ya Taifa na kuchangia ipasavyo katika kujenga uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge Ruth alisema tulisaini mwaka 2015, ninapenda niweke sahisho dogo tu; sisi tulisaini mwezi Novemba, 2016. Hata hivyo, mikakati ambayo Mheshimiwa Mbunge alipenda kuona tumechukua ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mkakati wa kwanza ni kuweka mpango wa kuzalisha umeme wa *solar* kwa miaka 30 ijayo ambao tumeweka walau zaidi ya megawati 1,000. Lakini mkakati wa pili ni kuendelea kutafuta fedha; napenda kuishukuru sana Serikali, katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 kupitia Mpango wa Umeme Vijijini, Serikali ilitenga shilingi bilioni 38 kwa ajili ya kuwawezesha wazalishaji wadogowadogo kuzalisha umeme wa *solar* kwa ajili ya kusambaza umeme vijijini. Hii ni hatua kubwa sana kwa Serikali ilichofanya katika hatua za kwanza za mipango mikakati ya kuhakikisha kwamba rasilimali ya jua nayo inatumika kwenye kuunganishia umeme wananchi.

Mheshimiwa Spika, hatua ya pili ni kwamba bado tunaendelea kupata fedha kwenye makampuni na mashirika ya kimataifa. Benki ya Dunia katika mwaka huu wa fedha pia imetoa dola milioni moja kwa ajili ya kusambaza umeme vijijini. Na hii ni hatua kwa ajili ya kuwawezesha Watanzania wadogowadogo kuweza kuzalisha umeme huu wa *solar* ili nao uweze kutumika katika maeneo ambako Gridi ya Taifa

haijafanikiwa kupita; hii ni mikakati ambayo Serikali inaendelea kuifanya.

Mheshimiwa Spika, mikakati mingine ambayo Serikali inafanya katika eneo hili ni kuhakikisha kwamba wazalishaji wadogowadogo wa Tanzania, hasa binafsi nao wanashiriki katika kuzalisha umeme wa aina hii. Mwaka jana mwezi Oktoba tulitangaza kwa wazalishaji wadogowadogo, na hasa Watanzania, ili waanze nao kuzalisha umeme huu wa *solar* walau kuanzia megawati 50 mpaka megawati 250. Taratibu zinazofanyika sasa ni kukamilisha uchambuzi ili kuwapata wakandarasi wa ndani ili nao waweze kuzalisha umeme huu. Huu ni mkakati muhimu sana shirikishi ambao Watanzania pia tunawashirikisha.

Mheshimiwa Spika, mkakati mwingine mahususi katika eneo hili, kama ambavyo nimeeleza, ni kuhakikisha makampuni ya Kitanzania yanashiriki. Hivi sasa – kwa kujibu swali la Mheshimiwa Profesa Tibaijuka – yako makampuni zaidi ya saba ya Watanzania; yupo *Lex Energy***,** yupo *Enzora***,** yupo Baraka, yupo ITOZ**,** yupo ZOTI**,** yote hayo ni makampuni ya Watanzania wadogowadogo na wanashiriki katika kuzalisha umeme mdogomdogo na kusambaza kwa Watanzania. Kwa hiyo, ushirikishwaji wa Watanzania uko palepale.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, bado kama Serikali tunawahamasisha Watanzania waendelee kushiriki kwa kiwango kikubwa sana katika kuzalisha umeme huu wa *solar* ili kuweka mchango mkubwa kwa ajili ya matumizi, lakini kujenga *sustainability* kwa Watanzania hata kwa miaka mingi ijayo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na maelezo niliyosema katika eneo hili, lakini ningependa tu kusema kwamba mkakati mwingine tumetenga maeneo. Yapo maeneo mahususi sana ambayo ni muhimu na yanaweza kuzalisha umeme wa jua. Baadhi ya maeneo tunayo hata hapa Dodoma, eneo la Zuzu linaweza kuzalisha megawati 50 mpaka 100; eneo la Kishapu kule Shinyanga, megawati 150 mpaka 250; eneo la Mkwese kule Manyoni, Singida megawati

100 mpaka 250 na eneo la Same kule Kilimanjaro nayo yanaweza kuzalisha umeme. Haya maeneo tumeyaainisha na kuyatenga kwa ajili ya kuzalisha umeme wa *solar.*

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge, hii ni baadhi ya mikakati tu tuliyochukua kuhakikisha kwamba umeme huu unanufaisha hasa rasilimali ya ujenzi wa uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa manufaa; pamoja na kwamba kwa sasa tunaomba kuridhiwa, lakini kwa vile tulishasaini mkataba huu yapo manufaa ambayo Serikali ilishaanza kuyapata. Hivi sasa ninapongea wapo Watanzania ambao wameshaenda kupata ufadhili wa *ISA* ambao wanakwenda kusoma kwa *level* ya *PhD* kwa ajili ya masuala hayahaya ya *solar* ili waweze kutoa mafunzo kwa Watanzania wengine. Na bado kuna nafasi ambazo tutaendelea kuzipata kwa ajili ya kutoa mafunzo kwa *levels* za chini, kati na juu ili Watanzania wengi waweze kupata elimu hii na kuweza kuwafundisha Watanzania wengi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tunaposema tutakuwa na umeme mwingi hapa nchini, umeme mwingine unatakiwa utokanae na huu utaratibu wa *solar.* Na tuna mpango huo kwa sababu unapokuwa na umeme wa kutosha na mchanganyiko, hata inapotokea dharura katika vyanzo vingine bado unaweza kuendesha nchi bila kuwa na mashaka yoyote.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo utaratibu huu wa *ISA* hadi sasa mwaka jana tulishiriki kwenye mkutano na *ISA* ime-*commit* kwa mwaka wa fedha ujao kutoa takribani Dola za Marekani milioni 385 kwa nchi yetu, na nchi yetu imekuwa-*committed* pesa nyingi kuliko nchi zote duniani ambazo zimeshiriki kwenye hii *ISA,* kwa hiyo ni mafanikio makubwa endapo Serikali yetu itaridhia.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu yaliyosemwa ni mengi, itoshe tu nawashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa kweli kwa michango yenu mizuri, lakini Serikali imedhamiria

kujenga uchumi wa viwanda kwa kutumia umeme mchanganyiko. Na mikakati na malengo yetu ni kufikisha *megawatt* 10,000 mwaka 2025 na kuwapelekea Watanzania umeme pote wanapokaa mijini na vijijini kwa zaidi ya asilimia 85 na kupeleka Gridi ya Taifa maeneo yote ya pembe nne za nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Dkt. Kalemani. Hoja imetolewa na imeungwa mkono, tunakushukuru sana kwa namna ulivyohitimisha hoja yako na jinsi Wabunge walivyokuunga mkono.

Sasa Waheshimiwa Wabunge, kama ilivyo ada inabidi tulifanyie uamuzi azimio hili linalohusu kuridhia kuanzishwa kwa ushirikiano wa kimataifa wa Nishati ya Jua.

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)*
*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Azimio la Bunge la Kuridhia kuanzishwa kwa Ushirikiano wa Kimataifa wa Nishati ya Jua lilipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, pia nitoe shukrani kwa niaba ya Waheshimiwa Wabunge wote kwa Wizara, Mheshimiwa Waziri, wasaidizi wako wote kwa jinsi mnavyohangaika na kutupatia mibadala ya vyanzo vya umeme katika nchi yetu. Na leo hapa umetuletea azimio hili linalolenga zaidi katika nishati ya jua. Nishati ya jua ni nishati ya uhakika, ni nishati ambayo ni *cheaper* kama alivyotuambia, ya nafuu zaidi.

Ninapenda kuwatia moyo Waheshimiwa Wabungewakati kwa wakati na kuwakumbusha tunapoweka majengo yetu basi ni vizuri tukawa na *solar*

*panels* hata mbili tatu kwa ajili ya matumizi fulani, labda kuchemsha maji ya moto, labda ku-*run television* na vitu kama hivyo, au kule jikoni ikatumika *solar* na vitu vya namna hiyo. Kwa hiyo inapunguza gharama za huu umeme mwingine, na kupunguza gharama ni sehemu muhimu sana ya maisha.

Pia ni aibu kwamba umeme tunaoutegemea wa Gridi ya Taifa ukikatika tu basi nyumbani kwako inakuwa giza totoro, wakati hata ukiwa na *panel* moja basi utapata vibalbu viwili vitatu vya kuweza kufanyia mambo mengine. Kwa hiyo tuelekee huko na tuzidi kuiomba Serikali izidi kupunguza kama ni kodi, kama ni nini kwenye vifaa vya umeme jua ili umeme huu uzidi kusambaa kwa Watanzania walio wengi hasa vijijini, mashambani na mahali pengine ili maisha ya watu wetu yazidi kuwa bora zaidi.

Zahanati za vijijini ambako umeme huu haujafika kwingine ziweze kutumia umeme jua, mafriji yetu yaweze kutumia umeme jua. Kwa sababu unaweza ukawa umejaza vitu vyako katika friji, nyama labda za wiki nzima, nyanya na vitu vingine, umeme huu ukakatika tunaoutegemea kwa siku nzima kwa mfano, saa 24, maana yake ni kwamba ndani ya friji humo vitakavyolika baada ya pale ni vichache sana. Lakini ukiwa na umeme jua maana yake ni kwamba huna wasiwasi wa friji hiyo *24 hours, 24/7.*

Kwa hiyo mtaona umeme jua kwa kweli una faida nyingi; ni ghali lakini Serikali izidi kuangalia na kusaidia kuona ni maeneo gani ya kupunguza kidogo gharama ili tuweze kwenda pamoja.

Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru mno kwa ushirikiano kwa kuwa shughuli za leo zote zilizopangwa tumeshazikamilisha kwa wakati unaotakiwa. Kwa jinsi hiyo basi kabla sijaahirisha Bunge niwakumbushe Kamati ya Uongozi tukutane saa saba na nusu pale Ukumbi wa Mikutano wa Spika; saa nane kamili Kamati ya Kanuni tukutane palepale mpaka saa kumi na mbili jioni na baada ya hapo Tume ya Huduma za Bunge kwenye ukumbi huohuo. Kwa

hiyo, wakati ninyi mnakwenda kidogo kubarizi sisi wengine tunaendelea na mikutano na mambo mengine mpaka saa mbili na nusu au zaidi kidogo usiku wa leo; kwa hiyo, shughuli za hapa sio rahisi jamani, ni ngumu kidogo zinataka uvumilivu.

Kwa jinsi hiyo, naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho, saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 7.08 Mchana Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Ijumaa, Tarehe 15 Novemba, 2019, Saa Tatu Asubuhi)*